ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais.
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu.
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa.
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa.
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa.
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi.
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole.
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi.
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae.
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu

49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tano – Tarehe 9 Aprili, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa heshima na ruhusa yako, naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mahakama ya Biashara Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. *(Makofi)*

Mhe. Ali Abdalla Ali (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria): Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mahakama ya Biashara Zanzibar na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 74

Ongezeko la Kesi za Ubakaji na Unyanyasaji wa Kijinsia

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Jeshi la Polisi ndilo lenye dhamana ya ulinzi wa raia na mali zao, na kwa kuwa ndilo lenye jukumu la kuwakamata wahalifu na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria, na kwa kuwa siku za hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la kesi za ubakaji watoto wadogo pamoja na zile za unyanyasaji wa akina mama ambazo huripotiwa Polisi, lakini baadhi ya kesi hizo hazifiki Mahakamani.

Je, ni sababu gani za msingi zinazosababisha kesi hizo kutofikishwa Mahakamani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74 kama ifuatavyo:-
Mhe. Naibu Spika, sababu kubwa zinazosababisha kesi za ubakaji watoto wadogo na zile za unyanyasaji wa akina mama kutofikishwa Mahakamani ni kuchelewa kufikishwa kwa mashauri hayo katika vituo vya Polisi mapema. Hali hii inatokana na kesi nyingi za aina hii kutokea katika jamii zetu ambazo zina mahusiano ya kifamilia na hivyo kufanya hatua za mwanzo kutafuta ufumbuzi kwa maelewano bila ya kushirikisha vyombo vya sheria.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi kesi kama hizo zinaposhindikana kusuluhishwa ndani ya familia ndipo huwasilishwa vituo vya Polisi, ambapo ushahidi huwa umeshatoweka na kushindikana kuchukuliwa hatua za kisheria za kupeleka kesi Mahakamani.

Mhe. Spika, serikali inachukua fursa hii kuwasihi wananchi wote kutoyafumbia macho mambo haya na kuyafikisha katika vyombo vya sheria mara yanapobainika katika maeneo yetu. Jeshi la Polisi limeanzisha Madeski Maalum ya kutoa fursa ya kupokea malalamiko yanayohusiana na ubakaji wa watoto na udhalilishaji wa kijinsia. Vile vile,

serikali imeanzisha vituo vya mkono kwa mkono, ili kuwarahisishia waathirika katika kuyapatia ufumbuzi wa kisheria matatizo hayo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kuwa katika jibu la msingi la Mhe. Waziri ameeleza kwamba kesi nyingi huwa zinachelewa kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Lakini kuna kesi ambazo huwa zinafikishwa katika vyombo vya sheria mara tu baada ya tukio kutokea kama vile kesi ya mtoto wa miaka 6 aliyebakwa anayeishi katika kijiji cha Mfikiwa katika Jimbo la Wawi.

Kwa kweli Kamati ya Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto ya Baraza hili la Wawakilishi walimuona katika Kituo cha *One Stop Centre* kilichopo Chake Chake wazazi wake wakihaha huku na kule kutaka kesi ile ichukuliwe hatua huku ikiwa imeshafika polisi. *(Makofi)*

Vile vile kesi ya Badria Moh'd Ali mkaazi wa Umangani Vitongoji yeye alibakwa na kijana na huyu ni mwanafunzi wa darasa la sita, alibakwa karibu miaka miwili iliyopita na kesi ilipelekwa mahakamani mara tu baada ya tukio lile kutokea.

(a) Je, Mhe. Waziri unapotujibu kwamba kesi zinacheleweshwa kufikishwa Mahakamani huoni kuwa unalidanganya Baraza hili.

(b) Kwa kuwa Mhe. Waziri Mabunge mengi ya Jumuia ya Madola likiwemo hili Baraza letu la Wawakilishi yametunga sheria kali za kuweza kudhibiti matendo haya ya udhalilishaji wa kijinsia pamoja na kuwabaka watoto. Kutokana na kwamba Jeshi la Polisi la nchi hii linashindwa kusimamia sheria tunazozitunga sisi huoni kwamba serikali imeshindwa kufanya kazi ya nchi hii. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, najua kwa nini anasema kwa hamasa kubwa, kwa sababu tendo la unyanyasaji wa kijinsia na udhalilishaji wa watoto ni matendo ambayo yanamuumiza kila mmoja wetu katika nchi hii na ni matendo ambayo kwa kila hali lazima sote kwa pamoja serikali na wananchi tushirikiane, ili kuhakikisha tunayapiga vita na hayatokei nchini mwetu.

Mhe. Naibu Spika, huo ndio msimamo wa serikali kutaka mambo ya namna hii yasiweze kutokea, ndio maana hatua mbali mbali zinachukuliwa kuhakikisha hilo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba serikali siku zote haiko tayari kulidanganya Baraza hili na itafanya kazi kwa uadilifu kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri. Mhe. Naibu Spika, mambo haya ya sheria yana taratibu zake, ushahidi pia una taratibu zake na lazima taratibu hizo zifuatwe. *(Makofi)*

Kwa ufupi kwenye swali (a) itabidi tuchukue maelezo ya Mhe. Mwakilishi na itabidi tuonane kwa ajili ya kunipa kwa undani zaidi ili tuweze kujua hasa kiini cha tatizo ni nini na kama kweli kuna jambo ambalo kwa makusudi watu wamefanya kusababisha kesi hizi zisifike mahakamani kwa mujibu wa utaratibu wake, basi wahusika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo. Kwa hivyo, lazima tuhakikishe kwamba mambo haya yanapigwa vita na kila mmoja anatimiza wajibu wake kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ni kweli tunapofanya muhali pale mwanzo linapotokezea tatizo kuna ushahidi pale hujifunika kwa sababu ushahidi mbalimbali wa mambo haya unatakiwa zile *evidence* za awali zote zile ziweze kwenda katika vielelezo husika, ili hatua zichukuliwe, lakini zikikaa muda vielelezo vile hupotea.

Kwa hivyo, narudia tena kuiambia jamii kwamba mara linapotokea tukio hili ni vizuri tuchukue hatua za kuzipeleka kesi hizi kwa utaratibu uliowekwa kisheria, ili matatizo haya tuepukane nayo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa serikali tutahakikisha tunafanya kila jitihada na tunaendelea kufanya jitihada kuona kwamba mambo haya hapa nchini hayafanyiki, ili kuepusha watoto wetu wasipate matatizo ambayo hatutaki kabisa yatokee.

Hivyo, napenda kulihakikishia Baraza hili tukufu kwamba serikali itaendelea kushirikiana na vyombo vyote vya ulinzi na usalama pamoja na vile vya sheria, ili kuhakikisha udhalilishaji wa kijinsia unapigwa vita nchini kwetu. *(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, ndani ya wiki hii tulishuhudia katika vyombo vya habari mtafiti yule katika masuala haya ya Haki za Watoto akitoa taarifa juu ya kesi ambazo zinawakabili watoto zisizopungua 300 ambazo huwa zinamalizwa katika mitaa na taratibu za kisheria huwa hazichukuliwi.

Je, serikali imejipanga vipi juu ya taarifa ile ya mtafiti yule Mama Najma ambayo ameitoa katika serikali kwa ajili ya kupunguza tatizo hili ambalo linatukabili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema awali kwamba serikali imejipanga kuhakikisha kuwa hatua mbalimbali zinachukuliwa za kisheria kuona kwamba watoto wetu ambao wanafanyiwa udhalimu huu jambo hili lisitokee.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana kesi ambazo zilifika katika Vituo vya Polisi zilikuwa ni 290, kesi zilizokuwa za kupelekwa mahakamani zilikuwa ni 139 na kesi ambazo hazikupata ushahidi zilikuwa ni 67. Kwa upande wa kesi walioachiwa huru ni 35, waliotiwa hatiani ni 28 na kesi ambazo bado zinaendelea na upelelezi ni 21.

Nam. 63

Kuongezeka kwa Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Januari 12 mwaka huu Rais wa Zanzibar Dr.Ali Mohammed Shein alisema watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wamefikia 6793 kutoka 5935 mwaka 2011 na waathirika wakubwa ni vijana.

(a) Serikali inachukua hatua gani za kupunguza maambukizi hayo ikiwemo kutoa ushauri, nasaha kwa vijana kujiepusha na vyanzo vya ugonjwa huo.

(b) Kampeni za kupambana na ugonjwa huo zimeanza muda mrefu. Je, zimefanikiwa kwa kiwango gani kama idadi inaongezeka kila mwaka.

(c) Kwa kuwa dawa za kulevya zimeonekana kuwa chanzo cha vijana wengi kuathirika na Virusi vya UKIMWI, serikali ina mpango gani wa kuitisha kura ya kuwafichua wauza unga na waletaji kutoka nje ya nchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hatua ambazo Serikali inaendelea kuzichukua katika kuwaelimisha vijana ili kujiepusha kupata ugonjwa huo, ni pamoja na:-

1. Kuendelea kutoa elimu kwa jamii yote kwa jumla na pia kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuambukizwa, kupitia njia mbali mbali za mikutano ya ana kwa ana, TV, Radio, Vipeperushi, Wasanii na mabango.
2. Kuendelea kusambaza vituo vya huduma mbali mbali, vikiweno vituo vya kupimia VVU, Vituo vya kutolea ushauri nasaha, vituo vya tiba, vituo vya kupimia waja wazito n.k.
3. Kuzishirikisha taasisi nyengine za Serikali na zisizo za Serikali katika kutoa elimu ya UKIMWI, zikiwemo taasisi za dini na asasi nyengine za kiraia katika kuhimiza malezi ya watoto wetu katika maadili ya Kizanzibari.
4. Kufanya kazi kwa karibu na Jumuia ya watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI kama vile *ZAPHA+* katika kuwaelimisha wengine.

(b) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa juhudi za kupambana na UKIMWI ni za muda mrefu, naomba nikiri kuwa pamoja na juhudi hizo bado changamoto zipo, lakini yapo mafanikio makubwa.

i. Tumeweza kudhibiti maambukizi ya VVU chini ya asilimia moja (1%) tangu mwaka 2002, ambapo kwa mara ya kwanza uchunguzi ulionesha kuwa kiwango cha maambukizi Zanzibar kilikuwa asilimia 0.6%. Aidha, chunguzi nyengine zilizofanyika Tanzania mwaka 2008, 2010 na ya mwisho ya 2012 zimethibitishwa kuwa bado kiwango cha maambukizi Zanzibar hakijavuka asilimia ya 0.6%.

ii. Wazanzibari walio wengi (zaidi ya asilimia 95%) wanaelewa nini UKIMWI, vipi unapatikana, athari zake na namna ya kujikinga.

iii. Wengi ya wale wanaoishi na VVU wanatumia huduma zinazotolewa na Tiba na Kinga na kufuata ushauri wanaopewa na wataalamu wanaowahudumia.

iv. Unyanyapaa, ingawa haujaondoka kabisa, lakini kasi yake imepungua kwa kiasi kikubwa.

v. Mchango wa Asasi za Kiraia zikiwemo Taasisi za Dini umekuwa ni mkubwa sana na ni wa kupigiwa mfano katika kuelimisha waumini wa dini zote kuu kwa jumla.

vi. Muamko wa watu kwenda kupima na kutumia huduma umeongezeka maradufu, kwani idadi yao imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

(c) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa dawa za kulevya ni chanzo cha vijana wengi kuathirika na Virusi vya UKIMWI na mpango wa kuwafichua wauza unga na waletaji kutoka nje na ndani ya nchi upo kisheria. Utaratibu wa kuitisha Kura za Maoni pia unaweza kutumika lakini ni suala ambalo utekelezaji wake si rahisi na endelevu na linahitaji gharama kubwa.

Kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia Usafirishaji na Matumizi ya Dawa za Kulevya (*Act No*. 9/2009) ambapo imefanyiwa marekebisho, *Act No*. 12/2011 kinaeleza wazi kwa kuainisha mpango wa kuzuia usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya.

Mtu yeyote atakayetoa taarifa zitakazopelekea kumkamata mtu yeyote anayehusika na makosa yote yaliyoelezwa na sheria hii, anaweza kuzawadiwa. Lakini pia Jeshi la Polisi lina utaratibu wa kuwazawadia watoa taarifa zinazopelekea kukamatwa kwa watuhumiwa wa makosa yote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri kukidhi swali la msingi naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Tatizo la dawa za kulevya ni chanzo cha maambukizi na sasa tumeshuhudia hivi majuzi tu baada ya kupokea unga kutoka nje, Zanzibar imekuwa inasafirisha unga kupeleka nje. Je, serikali inachukua hatua gani kuhusu kadhia hii iliyotokea.

(b) Pamoja na serikali kuendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari, tathmini gani imefanyika kujua mafanikio kupitia Sekta ya Habari.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli tumepokea taarifa za hivi karibuni na kwa kweli kwa kipindi sasa kuna taarifa zinazosema kwamba Zanzibar ni kama kituo ambacho dawa za kulevya zinapitia kwenda katika nchi nyengine. Taarifa hizo sisi tumezipata kutokana na wenzetu ambao tunafanya kazi kwa karibu katika suala hili yaani vyombo vya ulinzi na usalama vya nchi hii.

Tatizo kubwa ambalo limekuwepo katika suala hili ni jinsi ya kuweza kupambana, kwa sababu masuala haya yako katika usiri mkubwa na yanafanyika katikati ya bahari mbali, kiasi ambacho tunahitaji kuwa na vyombo vya kitalaamu tena vya kisasa na ujuzi wa kuweza kupambana, ili kuweza kuwakamata wahalifu hao wanaofanya biashara hii.

Serikali yetu inashirikiana kwa karibu sana na wadau wote na washirika wa maendeleo ambao wanahusika katika kupambana na biashara hii haramu.
Swali la pili kila baada ya muda Tume ya UKIMWI Zanzibar inafanya tathmini kwa kuangalia ni kiasi gani wadau wake mbali mbali wanaoshirikiana nao wamefanikiwa katika suala zima la kutoa elimu.

Kwa mfano, katika vyombo vya habari tathmini inafanyika na inaonekana kwamba kutokana na muamko wa wananchi wengi kuwa habari hizi zinawafikia na watu wengi wanalifahamu suala la UKIMWI. Kwa hiyo, kunaonekana kuna mafanikio makubwa katika vyombo vya habari na suala zima la kutangaza na kutoa taarifa zinazohusiana na gonjwa hilo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashkuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

(a) Mhe. Naibu Spika, katika taarifa ya suala hili ni kuwa watu ambao wanafikiriwa kuwa ni waathirika wa UKIMWI hivi sasa ni 6793. Kwa kweli naamini hii ni idadi ya watu waliokwenda kwa hiari yao kupima kutaka kujua hali yao kuhusu kuambukizwa na UKIMWI au laa. Lakini kwa sababu serikali imeweza kwa wananchi wote wanapofunga ndoa ni lazima kwanza wakapime UKIMWI na hilo suala linafanywa.

Je, kwa nini serikali haiweki mpango mahsusi hasa wa kila mtu kuweza kujua afya yake kuhusu UKIMWI na hasa katika nchi hii ilivyo hivi sasa imeingiliwa na watu kutoka kila upande ambao kwa masuala kama haya ni rahisi kuambukizwa.

(b) Kwa sababu dawa za kulevya ni moja kati ya mambo yanayoongeza kueneza UKIMWI katika nchi, na kwa sababu Zanzibar haizalishi dawa za kulevya, lakini zinatoka mbali zinakuja hapa na kusambazwa na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na uzito wa kupambana na suala hili la maradhi ya UKIMWI, kwa nini serikali haifanyi mtandao hasa wa makusudi wa kuweza kujua dawa hizi zinakotoka na zikifika hapa mtu yule aweze kukamatwa moja kwa moja badala ya kungojea watu wanaoweza kutoa taarifa na kukamatwa.

(c) Mhe. Naibu Spika, kwa sababu nchi hii ni huru kuingia na kutoka kuna wengine wanaotumia bandari kuu, uwanja wa ndege na kadhalika na wapo wengine wanapita bandari ambazo si za kawaida na wote hao wanatoka nje ya nchi wenye tabia na silka tofauti na zetu na wanasababisha sana kueneza maradhi haya.

Je, serikali kwa kushirikiana na masheha wana mpango gani wa kuweza kuwajua watu wanaoingia kila siku katika nchi hii, tabia na silka zao na kutaka kujulikana kwamba hawa ni waathirika au laa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba Baraza lako tukufu lielewe kwamba suala la kupima UKIMWI ni la hiari, yaani mpaka hivi sasa hakuna sheria inayolazimisha mtu yeyote iwe anayetaka kufunga ndoa au kuajiriwa ama kufanya shughuli nyengine yoyote na hata kuwa mgombea katika jimbo kwamba lazima apime UKIMWI, suala hili halipo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, jambo hili linatokana na Azimio la Dunia kwamba kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Haki za Binadamu. Kwa hivyo, naomba tuelewe hivyo, kwamba hilo haliwezekani na hata hilo la kupima kwa ajili ya kufunga ndoa ni suala ambalo Tume ya UKIMWI inalishajihisha kuwa lifanyike lakini halipo kisheria. *(Makofi)*

Swali la pili Mhe. Naibu Spika, ni kuwa Mhe. Mwakilishi ameuliza kwa nini hakuna mtandao ambao unaweza kuzizuia dawa zisifike hapa katika visiwa vyetu.

Naomba nimuarifu kwamba kwa taarifa tulizonazo kutoka kwenye vyombo vya ulinzi na usalama mtandao huo upo kuna suala zima la Ulinzi Shirikishi kwa kupitia *Interpol*. Kwa kweli mara nyingi dawa ambazo zilikuwa ziingizwe hapa zinakuwa *intercepted* na watu wanakamatwa katika maeneo mengine, bila ya hivyo hizi ambazo zinapitia kwenye *Airport* hapa zimekuwa ni nyingi sana kwa sababu watu wengi wameona kama hapa ni sehemu ya kupitisha kama ni *transit*, ili dawa hizi kwenda katika sehemu nyengine. Lakini katika suala hili tunapata usaidizi wa karibu wa vyombo vya wenzetu vya dola ambao tunashirikiana nao kwa karibu sana.

Mhe. Naibu Spika, swali lake la mwisho ni kama nilivyojibu swali la kwanza kwamba hatuna utaratibu mpaka hivi sasa wa kisheria wa kulazimisha kuwapima aidha tulionao ndani ya nchi au wageni wanaoingia, ili kujua afya zao kwa sababu suala la kupima UKIMWI ni jambo la hiari.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, ugonjwa wa UKIMWI katika visiwa vyetu vya Zanzibar ulianza kuonekana katika miaka ya 1980. Lakini mara nyingi sana ugonjwa huu wa UKIMWI unachukuana zaidi na masuala haya ya dawa za kulevya, kwamba ndugu zetu, watoto wetu pamoja na majirani zetu hususan vijana wanapotumia mabomba yale ya sindano kwenye kujidunga, ambayo tayari yameshatumika na yametupwa kwenye majaa na maeneo mengine yanapelekea kuweza kuchukua kwa haraka sana ugonjwa huu wa UKIMWI.

Katika visiwa vya Zanzibar tumezoea kuona utaratibu wa kukamatwa wale watu wanaohusiana na uingizaji wa dawa za kulevya, lakini hatuna kawaida ya kujua mwisho wa masuala yale ya dawa za kulevya yanavyomalizikia katika mahakama zetu za Zanzibar.

Je, Mhe. Waziri ataweza kutufahamisha katika Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, kwamba ni wahusika wangapi wa dawa za kulevya ambao kesi zao zilipelekwa mahakamani na mwisho wa habari zikaweza kufikia muafaka na hatua za kisheria na kinidhamu zikachukuliwa dhidi yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba suala la matumizi ya dawa za kulevya hasa kwa njia ya kujidunga sindano linakwenda sambamba na maambukizi ya UKIMWI kwa jinsi lilivyo.

Vile vile ni kweli katika watu ambao wanajidunga sindano maambukizi ya UKIMWI yapo kwa asilimia 16, wakati katika *population* ya kawaida ni asilimia 0.6 na ni tishio kwa nchi yetu katika maambukizi katika suala zima la UKIMWI.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba taarifa tunazo kutoka vyombo vya ulinzi na usalama na pia kutoka mahakama, kwamba wapo waliokamatwa katika suala zima la kusafirisha unga katika Uwanja wetu wa Ndege wa Zanzibar na baadhi ya kesi zimefikishwa mahakamani na hukumu zimetolewa.

Lakini namuomba Mhe. Mwakilishi anistahamilie kidogo kwa sababu hili ni suala linalohitaji takwimu sahihi na swali hili limeulizwa katika maswali ambayo nitayajibu katika kipindi hichi. Kwa hivyo, naomba avute subra kidogo ili tuje kumpa taarifa kwa ukamilifu ni wangapi waliokamatwa, waliohukumiwa na hukumu gani imetolewa. Mhe. Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wawe na imani kwamba hatua zinachukuliwa.

Nam. 27

Eneo la Bandari ya Malindi Kutokidhi Haja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Bandari ya Malindi ni kiungo muhimu sana katika uchumi wa Zanzibar, kwa hivi sasa Bandari hiyo imekuwa ndogo na haikidhi haja ya kuhudumia meli za mizigo. Kutokana na udogo wa bandari hiyo jitihada zilifanywa kuruhusu meli za mizigo kuteremsha mizigo yao hadi usiku, lakini kwa sasa utaratibu huo umeondolewa ingawa bado tatizo la ufinyu wa bandari lipo pale pale, na wenye meli wanalalamika mizigo kuchelewa kushushwa na wenye mizigo wanapiga kelele mizigo yao inakaa sana na kuharibika,

(a) Je, ni lini serikali itajenga eneo jengine kwa meli za mizigo, ili kuepusha usumbufu huo.

(b) Je, kama serikali haina uwezo wa kujenga eneo la kutosha kwa meli za mizigo, ipo tayari kuruhusu watu binafisi, katika ile dhana ya (*PPP*) au (*BOT*), kama vile ilivyofanya kwenye eneo la Bandari ya Abiria ambayo mtu binafsi amepewa na kujenga.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 27 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Lengo la serikali katika kukabiliana na tatizo la ufinyu wa Bandari ya Malindi ni kujenga Bandari mpya ya mizigo katika eneo la Maruhubi kama ilivyopendekezwa katika Mpango Mkuu wa Bandari ya Malindi (*Port Master Plan*) pamoja na Mpango Mkuu wa Usafirishaji wa Zanzibar (*Zanzibar Transport Master Plan*) katika MKUZA I na II.

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa pamoja inaendelea kufanya jitihada za kutafuta Muwekezaji au Mkopo kwa ajili ya kutekeleza lengo hilo ambapo Kampuni kadhaa zimeonesha nia ya kutaka kushirikiana na serikali kuwekeza katika mradi huo.

Majadiliano na Kampuni mbali mbali yanaendelea, ili kupata Kampuni moja itakayoweza kushirikiana na Serikali kwa utaratibu wa ujenzi na uendeshaji utakaokubalika (*PPP*, *BOT*, *BO* au nyengineo). Aidha hatua muhimu kwa hivi sasa kwa serikali ni namna ya kuona tunakamilishaje uchambuzi yakinifu, ili hatua ya pili ya kumtafuta mkandarasi iweze kupatikana.

(b) Serikali kwa kauli moja inawakaribisha wawekezaji katika eneo hilo, kama nilivyojibu katika jibu (a) hapo juu. Eneo la gati ya abiria linaloendelea kujengwa hivi sasa linajengwa kwa ufadhili wa Kampuni ya *Azam Marine*, ili kuimarisha huduma za abiria ambapo eneo hilo litabaki kuwa ni mali ya serikali na litaendeshwa na Shirika la Bandari la Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu aliyotoa Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza.
Kutokana na kukabiliana na ushindani tumeshuhudia sasa hivi nchi za Afrika ya Mashariki na Kati tukifanya kazi masaa 24 na ushahidi tosha kwamba bandari yetu ya Zanzibar imekuwa ni finyu. Hapo nyuma ricord zinaonyesha kuwa kazi hiyo ilikuwa ikifanyika usiku. Hivi sasa wafanyabiashara wetu wadogo wadogo wanaumia sana na mizigo yao kuharibika.

(a) Kuna sababu gani ya msingi kwamba isirudishwe tena huduma ile kwa kusingizia kisingizio cha Kamati ya Ulinzi na Usalama.

(b) Uzoefu unaonyesha huko nyuma shughuli hiyo ilikuwa ikifanyika mpaka asubuhi kutokana na ufinyu wa Bandari yetu, je sasa hivi kuna sababu gani za msingi kwamba zisiendelee huduma hiyo kutokana na uwezo wetu kuwa mdogo na vitendea kazi hakuna.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba nimkumbushe Mhe. Mwakilishi kwamba suala la kuteremsha mizigo kwenye meli za kigeni nyakati za usiku zinaendelea kama kawaida. Utaratibu tuliozuia ni utaratibu wa kushusha mizito katika meli zetu za ndani zile ndogo ambapo ni mwisho saa 4:00 na hii inatokana na utaratibu na mipango ya Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama ya Shirika la Bandari. Kamati hii ipo tukiona kwamba kuna hasara, kuna faida, kuna tija, au kuna sababu za msingi za kubadili utaratibu huu tutaamuru wazungumze, wajadili hali na ikiyumkinika kwamba kuna sababu za msingi za kuondoa utaratibu huo kinyume na zile sababu za msingi zilizofanya kuwepo kwa utaratibu huo basi tutaruhusu utaratibu uendelee kama tunavyoruhusu kwa meli za nje.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Fungu Nam. 37 ukurasa 27 Waziri au mjumbe yeyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo anatakiwa ajibu swali hilo kikamilifu.

Saa 4:00 hiyo shughuli watu wa Bandari hawataki kufanya Mhe. Naibu Waziri, haifanyiki, haifanyiki.

Mhe. Naibu Spika: Nadhani Mheshimiwa hukumfahamu alivyojibu amesema kwamba meli za kigeni zote zinashusha kucha kutwa, lakini meli za ndani mwisho saa 4:00 na kama utakuwa kuna tija basi itarejeshwa kama zamani. Tatizo kitu gani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi ndio naomba alifatilie hatukuja kubishana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, serikali kama ilivyoonyesha katika Master Plan inampango wa kujenga Bandari katika eneo la Maruhubi eneo la Mpigaduri kama ni hatua ya Mbadala ya kusaidia Bandari yetu ya Malindi. Kwa kuwa Wenzetu wa Tanzania Bara hivi sasa wameanzisha ujenzi wa Bandari kubwa kabisa ambayo itakuwa ni kubwa katika eneo letu la Afrika Mashariki katika eneo la Bagamoyo kwa nia ya kuipiku bandari ya Mpigaduri.

(a) Sasa kwa nia ya kuendeleza muungano wetu wa damu je, kulikuwa na juhudi gani zilizofanywa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwashawishi wenzetu ili wao watuachie siye mradi ule tujenge Bandari katika eneo la Mpiga Duri mpango ule ambao umefadhiliwa na Wachina.
(b) Lakini kwa sababu Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba mchakato unaendelea wa kufanya upembuzi yakinifu pamoja na kutafuta wabia, anawezaje Mhe. Waziri akalihakikishia Baraza hili na wananchi kwamba ni lini mchakato huo utamalizika ili na sisi tuendelee kuwa na bandari.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwakilishi ametaka kujua jitihada za serikali katika ujenzi wa bandari mpya ya Mpigaduri, lakini pia Mhe. Mwakilishi ametaka kujua jitihada za wenzetu wasijenge Bandari ya Bagamoyo.

(a) Mhe. Naibu Spika, suala la bandari miongoni mwa mambo ambayo yanasimamiwa kikatiba na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania lakini kwa bahati nzuri tumeweza kufanya Tanzania Bara kwa upande wake na Zanzibar kwa upande wake. Kumekuwa hakuna msuguwano wa aina yoyote zaidi ya ushirikiano kati ya pande mbili hizi. Hivyo basi nadhani kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hatukuwa na nafasi ya kwenda kuwazuia wenzetu wasiendeleze mradi wao. Jukumu letu sisi ni kukamilisha uchambuzi yakinifu tuendelee na jitihada zetu za kutafuta wafadhili, wahisani na washirika wa maendeleo ili nasi tuweze kujenga kama ambavyo wenzetu wanaanza kujenga.

(b) Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba mara tu tutakapokamilisha mchakato huu wa upembuzi yakinifu tutapata wenzetu wa Shirika la Maendeleo. Na lini kwamba bandari hii bandari hii itajengwa, hilo hatuwezi kuji - *commit* kwa tarehe au mwaka hadi pale utaratibu na mchakato huu utakapokamilika ikiwa pamoja na uchambuzi yakinifu na kupata wahisani, wafadhili au washirika wa maendeleo kwa ajili ya upatikanaji wa fedha.

Mradi huu ni mkubwa, gharama zake ni kubwa ikiwa pamoja na huo uchambuzi yakinifu nao pia unahitaji gharama kubwa ili kuweza kuukamilisha.

Mhe. Ali Salim Haji: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii, moja ya sababu ambazo zinachangia kucheleweshwa kwa upakuwaji wa mizigo hususan katika meli zinazotoka nje ni kutokuwa na zana za kutosha na za kisasa katika bandari yetu ya Zanzibar.
Je, ni lini serikali yetu kupitia Wizara yako Mhe. Naibu Waziri itajitahidi kukamilisha kuwa na zana za kisasa na bora katika upakuwaji wa mizigo ili kuondosha usumbufu wa kukaa muda mrefu kwa meli za kigeni.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake.

Pili ni kweli kwamba bandari imekabiliwa na changamoto kubwa ya zana za kisasa na nyepesi ambazo zinaweza kuteremsha mizigo. Lakini katikati ya mwisho wa mwezi wa Machi tuliweza kupata baadhi ya zana za kisasa, sasa

hivi kazi zinaendelea vizuri na kuna utaratibu maalum ambao tayari umeshapangwa na baadhi ya *tender* zimeshatiwa saini ili kuweza kuagiza zana kwa mujibu wa uwezo na utaratibu wa Shirika la Bandari.

Napenda nimuhakikishie mwakilishi kwamba hali ya bandari pamoja na udogo wake lakini itaweza kuwa na ufanisi zaidi muda mchache ujao kutokana na kupatikana kwa zana mpya na pia kupatikana nafasi nyengine ya makontena ambayo sasa hivi inawekwa *floor.*

Nam. 10

Usambazaji wa Umeme kwa Wananchi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Suala la umeme kwa wananchi wetu limekuwa siyo jambo la anasa kama ilivyokuwa ikidhaniwa hapo zamani, hivi sasa wananchi wanatafuta huduma ya umeme kwa ajili ya kujiletea maendeleo yao na kujitafutia riziki . Serikali imekua ikifanya juhudi kukbwa ili umeme uwafikie wananchi wote hadi vijijini na kuwarahisishia maendeleo yao na kutafuta riziki za halali. Licha ya hivyo, kumekuwa na malalamiko kwa Shirika la Umeme kushindwa au kuchelewa kuwaungia wananchi umeme licha ya taratibu zote zinazohusika kukamilika.

(a) Je, ni lini wananchi wa Unguja na Pemba watapata huduma hizi ambazo tayari wameshakamilisha taratibu zote za kupatiwa umeme kama walivyoahidiwa.

(b) Serikali ipo tayari kuwalipa fidia wananchi wamekamilisha taratibu za kuungiwa umeme mapema lakini wakacheleweshwa kuungiwa umeme kwa wakati.

(c) Je, ili kupunguza ukiritimba na urasimu wa “nenda uje” serikali haioni umuhimu wa kuruhusu taasisi nyingine zitoe huduma za uungaji umeme badala ya kuachiwa ZECO peke yake.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:

(a) Mhe. Naibu Spika, utaratibu uliyokuwepo kwa kila mwananchi aliyekwisha kulipia gharama za kuunganishiwa umeme anatakiwa aunganishiwe ndani ya kipindi cha miezi miwili. Wizara yangu itaendelea kusimamia utaratibu huu ili kuhakikisha kuwa wananchi hawapati usumbufu usiostahiki .

(b) Wizara haina utaratibu wa kulipa fidia kwa wananchi waliocheleweshewa kuungiwa umeme. Hata hivyo kama nilivyosema katika swali langu la (a) itasimamia kuhakikisha kuwa utaratibu uliowekwa unafuatwa kama nilivyojibu katika masuala mbali mbali yaliyopita.

(c) Kwa sasa wizara haiwezi kutoa ruhusa ya Makampuni mengine mbali ya ZECO kutoa huduma ya uungaji umeme. Jambo la muhimu zaidi ni kuiwezesha ZECO ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hata hivyo sheria ya ZURA tuliyoipitisha jana itasaidia kuondoa huo ukiritimba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa sana aliyenipa mzee wangu Mhe. Waziri ya kuvunja moyo. Yeye mwenyewe ni shahidi, keshakwenda Jambiani Kibigija, Mwakilishi na Mbunge wameshatoa milioni moja na leo ni mwaka wa pili, hayo maneno hayataki yata tochi na umeme haujaungwa mpaka hivi sasa.

(a) Je, sijui anatoa kauli gani kwa wananchi wa Jimbo la Muyuni hasa wa Shehia ya Jambiani.

(b) Kwa kuwa umeme ndio injini ya maendeleo je, serikali inachukua hatua gani za kuondoa urasimu katika Shirika la ZECO.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ni kweli tulikwenda Jambiani na kweli ZECO ilitoa ahadi ya kukamilisha baadhi ya vitu ambavyo zimepungua baada ya hizo pesa ambazo zimetolewa na Mwakilishi na Mbunge, lakini ilikuwa Mheshimiwa awe karibu na mimi ili nimsaidie kulisukuma hilo suala ili suala lake litekelezwe mara moja.

Suala la kuondoa urasimu Mhe. Naibu Spika, tumeshaliondoa jana baada ya kupitisha Sheria ya ZURA. Kwa hivyo urasimu utakuwa umemalizika.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa kuweza kurejesha huduma za umeme katika miundo iliyokuwa bora.

Mhe. Spika, mbali na huduma hii kurudi lakini kumekuwa kukijitokeza matatizo ya kuungua kwa transformer ikiwemo transformer ya Alabama, transformer ya Msufini katika jimbo la Rahaleo, na kusababisha kuleta shoti katika majumba ya Maendeleo ya Michenzani.

(a) Je, ni sababu gani zinazosababisha kutokea kwa matatizo haya.

(b) Ni hatua gani wizara itachukua kuondoa matatizo ambayo yamejiitokeza katika masuala haya ya umeme.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ni kwlei tangu tumeingia katika waya huu mpya wa umeme kumekuwa na matatizo ya shoti za hapa na pale. Shoti zanasababishwa na matatizo mbali mbali.

- Kwanza waya chakavu za njiani ambazo ZECO wana mpango wa kufanya rehabilitation waya zote chakavu zilizokuwepo majiani ambazo mara nyingi zinasababisha shoti za hapa na pale.

- Vifaa vya ndani ya nyumba ya mmoja wetu katika maeneo yetu vile vile huwa vinasababisha shoti vile vile. Mnajua vifaa vyetu vingi siku hizi tunavyotumia ni vya kichina mara vinasababisha shoti katika mahala popote pale na matatizo ya namna kama hiyo yanakuwa yanatokea. Najua wachina wana vifaa vyengine vipo *genuine*, lakini vyengine vina matatizo kwamba vinakuwa vipo katika *quality* mbaya.

- Wakati mwengine kuunga umeme kienyeji vile vile ni tatizo ambalo ZECO itabidi walifanyie kazi kuondoa masuala haya ya kuunga umeme kienyeji.

Hata hivyo, Mheshimiwa namuahidi kwamba mafundi wangu watapita katika maeneo waliyoyataja kwa ajili ya kutizama hizo shoti na sababu zake ili tuweze kufanya matengenezo ya mara moja. Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu spika, kwa kunipa nafasi hii ili na mi nipate nafasi ya kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kwamba utaratibu walionao kwa mwananchi ambaye ameshakamilisha taratibu za kupatiwa umeme anatakiwa apatiwe umeme ndani ya miezi miwili. Swali langu lipo hivi.

(a) Je, Mhe. Waziri utakubaliana nami kwamba utaratibu huu hautekelezeki, kwa sababu wananchi wanaokamilisha taratibu huchukua zaidi ya miezi sita kupatiwa umeme huo.

(b) Mhe. Waziri atakubaliana name kwamba wizara yake imeshindwa kusimamia utaratibu huu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, malalamiko haya tumeanza kuyasikia zamani na ndio maana Serikali imekaa kitako na kutengeneza sheria hii ya ZURA kwa ajili ya kuondoa malalamiko haya ili badala ya sasa kuwa ZECO ndio inayofanya kazi peke yake na makampuni binafsi yajichomoze katika kufanya kazi hizi ili kuondoa ukiritimba unaotusumbua sana.

Kwa hivyo sio kwamba wizara imeshinda wizara haikushindwa na ndio maana imeleta hiyo sheria ili kuuondoa huu ukiritimba uliyokuwepo hivi sasa hivi. Nina hakika kwamba sheria hii ikitiwa saini ikianza kufanya kazi na

makampuni binafsi yakijichomoza na kufanya kazi hizi za kuunga umeme katika maeneo mbali mbali nafikiri malalamiko yatakuwa mengine lakini sio haya, haya yatakuwa yameondoka.

Nam. 36

Maabara ya Wawi Kufanya Kazi Zake Kinyume na Sheria

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Maabara ya Afya ya Jamii iliyopo Wawi, Pemba inafanya kazi zake muda mrefu sasa lakini haipo katika mfumo mzuri unaotambulikana kisheria.
Je, Wizara imejipanga vipi katika kuangalia maabara ile ili iwe na mfumo mzuri unaotambulikana kisheria.
Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam. 36 kama hivi ifuatavyo:-
Mhe. Spika, maabara ya Pemba ipo katika mfumo wa *Public Private Partnership (PPP)* kulingana na makubaliano ya wadau waliotoa wazo hilo kujenga na serikali.

Uanzishwaji wa maabara hiyo ulikuwa ni wazo la daktari mmoja wa Kitaliana aliyekuja kufanya kazi ya utafiti wa matibabu wa maradhi ya kichocho Pemba, na kulikuwa hakuna maabara ya kufanyia kazi hiyo na ndipo daktari huyo alipowasiliana na *Ivo De Carneri Foundation* ya kwao Itali ili kuangalia uwezekano wa kupata msaada wa kujengewa maabara.

Ivo De Carneri Foundation na serikali kwa makubaliano yakaanzisha maabara ya jamii na serikali itowe kiwanja cha kujenga na wafanyakazi na *Foundation* kujenga maabara hiyo.

Mkataba *("Memorandum of Understanding")* ulitengenezwa na ulisainiwa baina ya pande mbili hizo na maabara ikajengwa na kwa kumbukumbu ya mchango wake maabara ikaitwa jina la Ivo De Carneri.

Kwa upande wa Zanzibar vitengo vya kichocho, minyoo na kifua kikuu vimewekeza katika maabara hiyo, na kitaifa inajulikana kama moja ya maabara za rufaa kwa kifua kikuu Tanzania na kimataifa inajulikana kupitia Shirika la Afya Duniani (*WHO*) ambapo nchi mbali mbali zinaleta watu wao kuja kufanya tafiti za maradhi yasiyopewa kipa umbele.

Maabara ina bodi ambayo ina wajumbe watano nao ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Afya na Wajumbe wawili kutoka *Ivo De Carneri Foundition* na muungalizi mmoja kutoka *WHO*.

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ivo De Carneri wameona ipo haja ya taasisi hiyo kuiwezesha zaidi kisheria ili kutoa nafasi kwa wafadhili wengine kuweza kuchangia katika maabara hiyo.

Mhe. Spika, kwa kufanikisha hilo Wizara imeupeleka mkataba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuufanyia kazi na kutupatia ushauri kuwa njia gani bora itumike kesheria itakayoiwezesha maabara hiyo kuchangiwa na wafadhili wengine mbali mbali kwa mujibu wa sheria ili kuifanya maabara yetu iwe ya kimaendeleo na ya kisasa zaidi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu hivi sasa, mwaka 2012/2013 serikali imechangia nini katika maabara hiyo ya Wawi ili kukuza jitihada za wawekezaji wale.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kama anataka pesa huwa hatutii pesa lakini tunatoa wafanyakazi, tunalipa wafanyakazi, tunasimamia hilo na tunasimamia shughuli zote zile. Huko mwanzo walipotia mkataba kulikuwa na makubaliano ya fedha lakini sasa hivi kitengo kinazalisha vya kutosha kujiendesha na pesa za ziada zinasaidia mambo mengine ya serikali. Kwa hivyo hakuna ulazima wa serikali kuchangia kwa sababu na ile ni sehemu ya serikali pia na tunachokipata tunakitumia kwa ajili ya serikali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b0 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika bajeti zote za Wizara ya Afya huzungumza fedha maalum kwa ajili ya kuisaidia maabara Pemba. Lakini Kamati yangu ilipokwenda ilipata malalamiko kwamba serikali inashindwa kuchangia fedha hiyo iliyotengwa kwa ajili ya kuendesha maabara ya jamii pale Wawi.

(a) Mhe. Naibu Waziri atwambie ni kwanini serikali wanatuomba fedha, tunaidhinisha lakini baadae wanashindwa kuingiza fedha kwenye maabara ile kama lengo la serikali.

(b) Kilio cha kupatiwa kuwekwa maabara ile kisheria ni cha muda mrefu, jambo ambalo athari yake inaweza ikasababisha madhara hata katika upande wa Kimahakama iwapo maabara ile itafanya kosa la kijinai. Ni kwa nini serikali inashindwa kuiweka maabara ile kisheria ili itambulikane duniani kote ili kuepuka gharama ambazo serikali hatimae itaingia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, mimi katika bajeti ya mwaka jana kama tulikuwa na kifungu ambacho kinasema kwamba tutachachia PHL sikumbuki hilo. Lakini hata hivyo kama nilivyosema PHL sasa hivi inajiendesha na ina uwezo mkubwa kuliko hata hiyo serikali yenyewe. Kwa sababu ina matumizi makubwa, na inatoa pesa kutupa sisi katika vitengo vyetu.

Maabara ya Pemba tukiangalia ilipo Chake Chake karibu vifaa vyote vinavyotumika katika maabara ile vinanunuliwa na PHL. Kwa hivyo kukosa shilingi milioni tatu za serikali hii sioni kwamba tunaweza tukasema kwamba maabara imeshindwa au serikali imeshindwa, isipokuwa maabara inajiendesha wenyewe na inaisaidia serikali kwa sababu ni kitengo cha serikali. Hapo mwanzo walipofanya walisema hivi, lakini kumeonekana kwamba sasa hivi hiyo serikali yenyewe inachokipata haina haja ya kukitia kule. Kwanza kinakuwa kidogo hakitutoshi, huku Wizara ya Afya kufanya yale mengine. Hiki kitengo hakihitaji pesa hizo milioni tatu, tunapata zaidi ya milioni tatu inayotupa sisi Wizara ya Afya kufanyia kazi.

Kwa hivyo sijaliona kama hilo bado ni la msingi, lakini serikali hatuwezi kusema kwamba imeshindwa kutufanyia kazi. Nimesema kwamba kisheria kitengo hichi kinafanyiwa kazi na hili suala lipo chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Mwanasheria Mkuu atakapokuja na njia iliyobora ndiyo itakayofanyiwa kazi. Kwa hivyo tunalifanyia kazi hili suala.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kwa upole sana nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa amekiri hapa kwamba hivyo Ivo De Carneri na SMZ wanaubia katika ujenzi wa ile maabara pale na kwa taarifa tulizonazo kuwa kuna wafanyakazi pale walioajiriwa na Ivo De Carneri moja kwa moja na wapo walioajiriwa na SMZ. Na kwa kuwa kuna tofauti kubwa ya malipo baina ya wafanyakazi wa Ivo De Carneri moja kwa moja kuna manung'uniko makubwa.

(a) Je, suala hili ni kweli.

(b) Mhe. Naibu Waziri anaweza akatueleza nini kuhusu mahesabu ya pale inasadikiwa kwamba SMZ haina *access* ya kuweza kujua mahesabu ya pale. Je, neno hili ni kweli na kama ni kweli na zile ni fedha za walipakodi wa nchi hii pamoja na hao wafadhili, haoni kwamba kutakuwa hakuna matumizi mazuri ya fedha za walipa kodi wa nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, pale kuna wafanyakazi wa makundi mawili, kundi la kwanza ni wafanyakazi wa Wizara ya Afya ambao wameajiriwa na Wizara ya Afya na wanalipwa mshahara na Wizara ya Afya. Wizara ya Afya ina viwango vyake kulingana na elimu waliyonayo wafanyakazi wale.

Ivo De Carneri imeajiri wafanyakazi mbali ya Wizara ya Afya na hao wengi wao wako katika masuala ya *administration* kwa hiyo nao wana viwango vyao vya mishahara. Kwa hivyo waliyopo pale kwa upande wa Wizara ya Afya hawana ulazima wa kubaki Ivo De Carneri kama wanaona mishahara ya Afya haiwatoshi, kwa sababu hicho ndicho kiwango cha Wizara. Kama wanataka sasa labda watafute utaratibu mwengine nje ya huu kwa sababu Ivo De Carneri inajukumu lake la kuajiri wafanyakazi wake na viwango vyake na Wizara ya Afya ina jukumu lake.

Ninachokijua mimi kwamba hao wafanyakazi wa Wizara ya Afya wana posho ya kutosha kujalizia kufikia kiwango ambacho wafanyakazi wa Afya wengine hawana. Kwa hiyo sio suala la mshahara ambalo linalozungumzwa hapa kwamba hizi sehemu mbili ambazo ajira ni mbili tofauti zilingane, hilo halitowezekana. Hilo la kwanza.

Lakini la pili nimesema bodi ipo ya watu watano ambayo huwa inakutana na mahesabu yote yapo pale, yanapitiwa, yanazungumzwa, kuna muhasibu pale na pia *internal auditor* wetu anayakagua mahesabu ya pale. Kwa hiyo sasa sijui *access* ipi zaidi ya hiyo, kwa sababu sisi kama wizara hizo ripoti tunazipata.

Nam. 100

Wananchi Waliohamishwa Katika Shamba la Selem Mfenesini

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-

Mara baada ya Mapinduzi Matukufu ya 1964, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliwapatia wananchi wake ardhi kwa ajili ya kuwapunguzia umasikini kwa kuitumia ardhi hiyo kwa kilimo na mifugo. Miongoni mwa eneo ambalo lilitolewa ni shamba la Selem ambalo lipo Jimbo la Mfenesini. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni wananchi wanaolitumia shamba hilo wamenyang'anywa na kufukuzwa katika maeneo yao, hali ambayo imewarejesha nyuma kimaisha.

(a) Kwa kuwa wananchi hao wameliendeleza eneo hilo kwa muda mrefu. Je, serikali ina mpango gani wa kuwapatia angalau sehemu ndogo ya ardhi hiyo ili nao waweze kuendesha maisha yao.

(b) Kuna madai kuwa eneo hilo la Selem limegaiwa kwa vigogo mbali mbali. Je, madai hayo ni kweli.

(c) Ni vigogo gani waliopewa eneo hilo na ekari ngapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-
Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 100 lenye kifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika**,** kabla ya kulijibu swali hili, naomba kutoa ufafanuzi mdogo. Serikali ya Mapinduzi ni kweli iliwagaia wananchi eka tatu tatu mara tu baada ya Mapinduzi matukufu ya 1964 kwa nia njema kabisa ya kuwakomboa wananchi hao kutokana na unyonge wa kipato katika maisha yao. Wananchi walipewa eka tatu waliotakiwa kuyaendeleza mashamba hayo kwa kazi za kilimo ingawa wengi wao hivi sasa wametawaliwa na tamaa ya kuuza viwanja katika eka hizo kutokana na ardí kuwa na bei kubwa. Hata hivyo katika shamba la Selem wengi wa wananchi waliokuwa wakilima hawakupewa eka tatu na Serikali na ndio maana hawana hati rasmi za mashamba hayo, isipokuwa waliingia kwa kulima tu, lakini bado mashamba hayo yanabaki kuwa ni ya Serikali.

   Ni kweli kuwa baadhi ya watumishi wa Serikali wakiwemo waliostaafu waliomba nao wapatiwe ardhi ili wajiendeleze kimaisha kwa kazi za kilimo, na hao pia ni wananchi wa nchi hii, lakini hata hivyo hawakupewa kwa sababu wao ni vigogo.

   Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

   Suala la kuwa wananchi waliokuwa wakilima kwa muda mrefu na kuliendeleza shamba hili halikuwa sahihi, kwa sababu wananchi hao walikuwa wakilima mazao ya chakula na sio mazao ya muda mrefu kama vile miti ya matunda au ya kibiashara. Vile vile yale maeneo waliopewa baadhi ya watumishi wa Serikali hayakuwa na mazao kwani wenyewe tayari walikwishavuna.

b) Mhe. Spika, kuhusu suala la kuwapatia maeneo ya kulima wananchi wanaohitaji ardhi tayari suala hilo linafanyiwa kazi na Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kuangalia maeneo matupu na kuyapima ili yaweze kugaiwa kwa wananchi hao japo kwa kiwango kidogo kama robo au nusu eka kwa kila mwananchi kwa vile maeneo yenyewe yaliyobaki ni madogo.

c) Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kurejea tena kusema kwamba hakuna mtu aliyepewa ardhi kwa sababu ni kigogo, isipokuwa wale waliopewa ni baadhi ya watumishi wa Serikali ambao wameitikia wito wa Serikali wa kuonesha mfano katika kuendeleza kilimo na kujipatia riziki ya kuendesha maisha. Aidha, watumishi hao hawana tofauti na mkulima yoyote katika kuimarisha kilimo ambapo jumla ya ekari 139.0 zimetolewa kwa wananchi hao huko Selem.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Katika maelezo yake Mhe. Naibu Waziri alikuwa akieleza kwamba kweli amekiri kwamba kulikuwa kuna wananchi wakilima pale mwanzo kabla ya hawa ambao wamepewa sasa.

Je, kwa nini katika kugawa kwake asiwafikirie wananchi wale kwanza waliokuwa wakilima kuwapatia japo kidogo kama ambavyo swali la msingi lilikuwa linauliza na hao wengine ndipo wakapata. Maana yake inaonekana wamenyang'anywa wale waliokua wakilima kwanza wameenda kupewa wengine. Je kwa nini usiwafikirie wananchi wale waliokuwa wakilima kwanza huu si kuonesha ubaguzi katika nchi hii.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ni kweli yapo malalamiko ya muda mrefu katika shamba la Selem kwamba kuna wananchi walikuwa wakilima pale wamenyang'anywa na mashamba wamechukuliwa na watu wengine. Hata wewe mwenyewe Mhe. Naibu Spika, ukiwa Mwakilishi wa eneo lile uliwahi kulalamika kwamba kuna mtu mmoja pale amemuhamisha mtu katika eka yake kwa sababu tu analima na amemuondosha asilime.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni Waziri wa Ardhi natoa ahadi kwamba suala hili Wizara yangu imeshaanza kulifanyia kazi na itaendelea kulifanyia kazi. Tuna utaratibu wetu kila mwananchi kama sehemu ipo anayo haki ya kupata ardhi kama ipo hiyo ardhi yenyewe. Lakini kama kuna utaratibu wananchi wa kawaida huwa wanapatiwa eka tatu, utaratibu wa zamani ulikuwa kuna viongozi maalum wanapatiwa eka 10. Hivi sasa unampatia kiongozi huyo maalum eka 5.

Kama kuna mtu yeyote au kuna mwananchi yeyote au kuna mwananchi yeyote amechukua katika shamba la Selemu zaidi ya eka 5 yaani ana eka 10, 15, 20 tutazirejesha Serikalini na kuwagaia wananchi. Hiyo ndio kazi tunayoifanya Mhe. Spika.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kwa vile ardhi yote ni mali ya serikali, je wale wananchi waliopewa kwanza kulima nao wamenyang'anywa je serikali imewatengea maeneo gani au kuwalipa fidia gani kwa kilimo chao cha miti ya kudumu na nyumba ambazo walikwisha jenga za kudumu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ardhi ni mali ya serikali, waliopewa ardhi kwa ajili ya kilimo walitakiwa waitumie ardhi ile kwa kilimo. Anaweza mtu akawa na nyumba yake moja ndani ya ardhi yake kwa sababu ni karibu na mahala ambapo analima. Lakini kumetokea matatizo kweli kwamba kuna baadhi ya wananchi wamezitumia zile ardhi kwa kuziuza viwanja hili ni kosa kubwa sana ambalo baadhi ya wananchi wameshafanya limetokezea katika maeneo yetu.

Lakini vile vile huwa ile ardhi inatakiwa kwa ajili ya kufanya kazi yoyote ya maendeleo, utaratibu ni kwamba watu wale walipwe fidia kwa yale mazao yao yaliopo ikiwa michungwa, miembe, nyumba, walipwe ndio utaratibu. Kama hawakulipwa wanayo haki ya kudai wafanyiwe malipo katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuongezea kusema kwamba mtu yoyote anayeuza ardhi ni kosa kwa sababu ardhi ni mali ya serikali. Ukitaka kwa maendeleo ulipwe fidia katika ardhi ile ambayo umepewa. Lakini kwa hawa watu waliokuwa wanalalamika kwa Selem ambapo ndiko lilipokuja swali mama nasema hatua tutakazozichukua kwa watu waliochukua maeneo makubwa ardhi hizo watarejeshewa wananchi wale waendelee kufanya kazi za kilimo huo ndio ukweli.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru pamoja na majibu na ufafanuzi wa kina wa Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Katika majibu yake katika swali la mwanzo la nyongeza amesema kwamba utaratibu uliokuwa umewekwa ni kwa mwananchi wa kawaida kwa kutumia maneno yake,

mwananchi wa kawaida kupewa eka tatu na kwa viongozi kupewa eka 10. Mhe. Naibu Spika, swali langu ni kwamba moja ya malengo ya Mapinduzi tunavyoambiwa ni kuondosha matabaka katika nchi hii.

Je, serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar inapotamka ndani ya Baraza hili kwamba ina sera mbili tofauti kwa wananchi walioitwa wa kawaida na wasiokuwa wa kawaida ambao ni viongozi wakapewa ekari 10, haioni kama inasaliti na kukiuka malengo ya Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, Zanzibar hakuna matabaka na nilisema kwamba mwanzo zikitolewa eka 10 sasa zinatolewa eka 5 huu ni utaratibu wa kawaida, tunapitana hivyo hata katika mishahara. Tukiweka mishahara huyu hapa huyu hapa sio tabaka ni heshima kwa kazi mtu anayoifanya kwa hivyo ndio maana wengine wamepewa eka 5.

.

Nam. 58

Ufundishaji wa Somo la Historia katika Skuli za Serikali

Mhe. Jaku Hashim Ayoub Aliuliza:-

Kwa kuwa vijana wengi wa kizazi kipya hawafahamu historia ya Zanzibar Serikali ina mpango gani wa kurejesha somo hilo kwa skuli za msingi na sekondari kwa manufaa ya wananchi wake.

(a) Kwa nini Serikali iliamua kuondoa somo la historia wakati nchi zote duniani zinaenzi historia za nchi zao.

(b) Katika kipindi hichi cha utandawazi Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kituo cha utamaduni na mambo ya historia ili vijana wengi na wageni wapate kufahamu historia ya Visiwa vya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake nambari 58 lenye vifungu (a) na (b). Kwanza, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza naomba kutoa maelezo mafupi ya jumla.

Mhe. Naibu Spika, Somo la Historia lina umuhimu mkubwa katika kuelimisha vijana wetu na kuelimisha umma kwa ujumla kuhusu historia ya dunia na historia ya nchi yetu hasa kwa vizazi vipya. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Somo la Historia halijawahi kuondolewa katika *syllubus* ya Wizara ya Elimu hata siku moja. Somo la Historia linaendelea kusomeshwa kuanzia darasa la kwanza hadi darasa la nne, na jengine linasomeshwa kuanzia darasa la nne hadi *form six*. Kwa darasa la kwanza hadi darasa la nne historia inayosemeshwa ni ile inayochanganywa sayansi jamii. Na kuanzia darasa la tano hadi kidato cha sita, historia inayosomeshwa ni peke yake kama ni historia. Na hapa Mhe. Naibu Spika, nimekuja na kitabu cha historia tunachokitumia makusudi kwa kusomeshea *secondary school*. Hii ni uthibitisho kwamba historia haijapata kusitishwa na inasomeshwa mpaka *form six*.

(b) Swali linakuja kwa nini serikali iliamua kuliondosha somo hilo. Kama nilivyolijibu swali (a) serikali haijaondosha swali hilo.

(c) Swali linakuja katika kipindi hiki serikali ina mpango gani wa kuanzisha kituo cha utamaduni katika mambo ya historia na kadhalika.

Vituo vya utamaduni vya historia ya Zanzibar vipo chini ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Vituo hivyo ni kama vile makumbusho mbali mbali hasa Makumbusho ya historia yaliyopo Forodhani, Beit El Ajaib na Kituo cha Uhifadhi wa Nyaraka Kilimani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri hivi sasa kidogo yamenichanganya *syllubus* ninayoijua mimi ya Wizara ya Elimu ni moja ikiwa Skuli ya Kitogani, Muyuni, Makunduchi ni moja lakini kwa masikitiko makubwa mpaka hivi sasa asubuhi, nazungumza na Skuli ya Kitogani na Skuli ya Jambiani katika Jimbo langu somo la historia darasa la kwanza mpaka la tatu halisomeshwi. Je utakuwa tayari baada ya kumaliza kikao hiki ninafikiri sasa hivi skuli zimefungwa ukawaita watendaji wako ukakaa nao hili somo halisomeshwi. Masomo yanayosomeshwa darasa la kwanza Kiswahili, Kiingereza, Hesabu, Dini na Mazingira.

Sasa sijui unaniambia vipi Mhe. Waziri kwa suala hili. Kama mimi ninasema uongo au wewe Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, *syllubus* ni moja, kuna *syllabus* ya kuanzia chumba cha kwanza mpaka cha 4, na cha 4 mpaka *form six*. Ni kweli yumkini kabisa katika Skuli moja iwe Jambiani, iwe Makunduchi, iwe Donge inawezekana kabisa walimu wanaosomesha katika skuli hiyo wakazembea kulisomesha somo la historia, kwa sababu moja inawezekana kwamba hawalipendi na pili inawezekana kwamba hawalifahamu. Lakini tatu inawezekana kwamba ni wavivu. Kwa hivyo *syllubus* ni moja inategemea ni eneo gani la Skuli au kiwango gani cha elimu kinachosomeshwa, Kwa hivyo hakuna *syllubus* ya Jambiani ikawa mbali au haipo lakini ya Makunduchi ikawepo hapana *syllubus* ni ile ile moja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii nikiwa kama Makamu Mwenyekiti Mjumbe wangu Mhe. Jaku. Tumetembelea Skuli nyingi Unguja na Pemba na ni kweli hatujaona somo la historia likisomeshwa kama Mhe. Waziri alivyosema. Kwa kuwa somo hili ni muhimu kumbe Wizara ilikusudia kuwasomesha wanafunzi somo hili la historia na kwa kuwa Mhe. Naibu Spika halisomeshwi je Mhe. Waziri atakuwa tayari sasa Mkurugenzi anayehusika na Elimu ya Msingi kuondoshwa kwa sababu kama lengo ni kusomeshwa na halisomeshwi yeye ndiye *mas-uli* sasa yeye atakuwa tayari kumuondosha Mkurugenzi wake.

Lakini Pili Mhe. Waziri anafahamu kwamba historia ya Zanzibar inapotoshwa hata watembea watalii wanadiriki kupotosha historia ya Zanzibar kwa sababu hakuna msingi madhubuti wa Serikali unosisitiza kuelezwa kwa kina historia ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, (a) Mkurugenzi huondoshwa kwa sababu mwalimu fulani hasomeshi historia skuli fulani. Nakubali kuwa hilo ni kosa la huyo mwalimu, nakubali kwamba kosa hilo tutalifuatilia na sasa kama kumuondosha ni kumuondosha mwalimu sio Mkurugenzi, Mkurugenzi hana hatia. Mkurugenzi anafuata maagizo ya Wizara na kama agizo la Wizara ni *syllubus* kusomeshwa na mwalimu hasomeshi kosa ni mwalimu si Mkurugenzi.

Swali la Pili naomba alirejee sikulifahamu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, kabla ya swali la Pili nataka kidogo utaratibu ni kwamba walimu wa Zanzibar wanasomesha masomo yote kutokana na muongozo wa serikali. Muongozo wa Wizara haujawaeleza kupitia Mkurugenzi kwamba wanafunzi wa darasa la kwanza mpaka la tatu wasomeshwe historia. Sasa kama ni kosa au si kosa la Idara yake ya Elimu ya Msingi kwamba Mkurugenzi huyu hajatoa agizo kwa maskuli yetu kwamba wasomeshwe somo la historia. Kwa hivyo Wizara isije ikafanya ujanja ikawahukumu walimu kwa sababu hawajapewa agizo hilo.

Swali langu la (b) lilikuwa kwamba historia ya Zanzibar inapotoshwa na hata watembeza utalii wanadiriki kupoteza historia ya Zanzibar kwa sababu serikali inashindwa kuweka msingi madhubuti wa kuielezea historia ya Zanzibar kama ilivyo katika historia yake tangu 1964.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, serikali imetoa muongozo tena madhubuti na ndio maana kuna hiyo *syllubus* iliyoandaliwa kwa ajili ya kusomeshea, na *syllubus* hiyo huwa inafanyiwa mapitio kila haja inapotokea. Kwa mfano hivi sasa *syllubus* tunaifanyia mapitio kuhakikisha zile kasoro tulizozigundua

ikiwemo hii kasoro ya *go slow* katika somo la historia, wakati nilipokuwa najibu jibu mama nilisema baadhi sio walimu wote, baadhi ya walimu hawalipendi somo la historia, baadhi ya walimu hawalifahamu vizuri somo la historia. Na kwa sababu hizo ndio wanakwenda pole pole au hawalisomeshi vizuri lakini hilo sio kwamba serikali haijatoa muongozo, somo la historia lisomeshwe hapana. Serikali imetoa muongozo madhubuti na ndio maana kuna *syllubus* ambayo somo la historia lipo.

Lakini zaidi ya hayo Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tunachapisha vitabu vya *primary school* kutoka *Standard One* mpaka *Standard Four* vya *secondary* vipo vya kutosha. Na vitabu hivyo hivi karibuni vitabu vya masomo matatu; Historia, Kiswahili, na *Geography* vimeshachapishwa vinafanyiwa mapitio sasa hivi a karibu tutavigawa. Vyengine viwili vinaendelea kuchapishwa lakini tenda tumeshatoa.

Kwa hivyo kama somo hili halisomeshwi kwa nini tunachapisha basi vitabu vipya, tunasomesha na wale wanao *go slow* nakubaliana na Mhe. Hija kwamba tutawafuatilia na hawa ndio watakaopewa adhabu na sio Mkurugenzi. Mkurugenzi anatimiza wajibu wake.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Mhe. Waziri katika majibu yake ya msingi alisema kwamba somo la historia linafundishwa darasa la kwanza hadi la nne pamoja na *form one* hadi *form six* kwa skuli za Zanzibar.

Mhe. Waziri kutokana na umuhimu wa somo la historia, kutokana na miongo mingi tu ya kihistoria iliyopita katika nchi yetu ya Zanzibar huoni kuna umuhimu sasa wa somo hili kufundishwa kama somo lenye kujitegemea pekee badala ya kuchanganywa na masomo mengine katika ngazi ya msingi.

Lakini (b) Mhe. Waziri Wizara yako kwa hivi sasa tumeshuhudia miaka tofauti kwamba inahimiza sana masomo ya sayansi na kutotilia maanani sana suala la walimu ambao wamejifunza masomo ya *arts* yaani ya sanaa.

Je, huoni Mhe. Waziri kitendo hiki kinapelekea kukosekana kwa walimu wengi wa somo la historia ambapo walimu hawa ni walimu wa *arts*.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, (a) amesema kwamba haoni kwamba kuna kasoro ya kulisomesha somo hili *standard one* mpaka *standard four* na halafu tusiendeleze hadi skuli za sekondari. Nataka nimjibu kwamba ni utaratibu wa Wizara ya Elimu ya sasa hivi tuna matabaka mawili ya *primary education*. Tuna *lower primary education* na tuna *upper primary education*. *Lower primary education* ni ile ya msingi kuanzia chumba cha kwanza hadi chumba cha nne. Hii somo lolote huwa linasomeshwa kwa Kiswahili. Kuanzia chumba cha tano hadi *form six* tunasomesha kwa Kiingereza.

Hiyo hiyo historia kwa upande mmoja inasomeshwa kwa Kiswahili na kwa upande mwengine inasomeshwa kwa Kiingereza inategemea upo katika daraja lipi.

Swali la Pili naomba alirejee.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Spika, swali langu la Pili lilikuwa linasema kwamba Wizara ya Elimu hivi sasa imekuwa ikitilia mkazo zaidi walimu wa sayansi. Je, kitendo hiki haioni Wizara kwamba walimu wa historia ni walimu ambao wanatokana na masomo ya *arts* Je kitendo hiki haoni kwamba ni kuwapoteza miongoni mwa walimu wa historia katika maskuli yetu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba mkazo mkubwa unaingizwa sasa katika masomo ya sayansi kuliko masomo ya *arts*. Lakini na tunafanya hivyo kwa sababu ya mahitaji ya nchi. Wizara inasomesha kutokana na mahitaji ya nchi na kutokana na mahitaji ya soko la ajira. Soko letu la ajira sasa hivi limeelemea zaidi kwenye vitengo vya sayansi kuliko vya *arts*.

(b) Kutoweka mkazo mkubwa sio kwamba hatuweki mkazo lakini kutoweka mkazo mkubwa katika masomo ya *arts* haina maana tumeitupa kwa sababu historia peke yake sio somo la *arts* kuna historia, kuna Kiswahili, kuna Geography na kadhalika. Kwa hivyo masomo ya *arts* tumepunguza kuweka mkazo mkubwa kwa sababu ya mahitaji ya nchi na mahitaji ya soko la ajira. Lakini bado masomo ya *arts* yanasomeshwa maskulini mote viwango vyote *primary* mpaka *secondary*. Ahsante.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Kutokana na umuhimu wa somo la historia na huku katika skuli za msingi somo hili linafundishwa ndani ya masomo mengine haoni kwamba Wizara yake sasa imefika wakati wa kulifanya somo hili ni somo la kujitegemea peke yake katika ngazi zile za msingi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba radhi sikulijibu swali lile, lakini nilipokuwa natoa jibu mama nilisema somo la Historia linasomeshwa kwa kulichanganya na somo la Sayansi Jamii kuanzia darasa la kwanza hadi darasa la nne tu, kuanzia darasa la tano somo la Historia linasomeshwa peke yake kama ni somo la Historia. Kwa hivyo, kuanzia daraza la tano mpaka *Form IV* somo la Historia linasomeshwa peke yake.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Mahkama ya Biashara Zanzibar (Divisheni ya Mahkama Kuu) ya 2013

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazina na tukafika hapa tukiwa katika hali ya uzima na kuendelea na shughuli zetu.

Lakini la pili napenda nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili kuzungumzia Mswada huu wa kuanzisha Mahkama ya Biashara.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu kama tulivyozungumza jana umekuwa *reprinted*, yaani tumeuchapisha upya kutokana na agizo la Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Hii ni kutokana na makosa mengi madogo madogo ya uchapaji ambayo yameorodheshwa katika *matrix* niliyoitoa mbele ya Baraza lako tukufu ambayo nilitia saini katika barua yangu ya utangulizi ya tarehe 3/4/2013. Marekebisho hayo yaliyofanywa chini ya kifungu 84(2) (a) sasa yote yamo ndani ya mswada huu uliogawiwa jana. Kwa maana hiyo, Mhe. Naibu Spika, Mswada ule wa zamani usizingatiwe bali utazamwe huu ambao umegawiwa jana na ambao umezingatia marekebisho yote kama kamati ilivyoagiza.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu umezingatia changamoto zinazotukabili za utatuzi wa migogoro ya kibiashara hapa Zanzibar chini ya mfumo wa sheria uliopo. Mfumo uliopo wa kisheria unazingatia migogoro ya kibiashara kama migogoro mingine yoyote, hii ni kusema hakuna mazingatio maalum yanayoainisha ili kuweka hatua maalum ya kukabiliana na changamoto zinazokabili maendeleo ya biashara hapa Zanzibar. Kwa maana hiyo, biashara nyingi Zanzibar zinapata misukosuko na kuwafanya wenye biashara hizo kuondoka Zanzibar na kutafuta sehemu nyengine za kufanya biashara.

Mswada huu una lengo la kukinga tatizo hilo ambapo inapokuwepo sheria kama hii basi wale wafanyabiashara wataweza kusuluhishana katika mfumo ambao umewekwa katika sheria hii na baadae kufanya shughuli zao za biashara hapa hapa Zanzibar na kwa uharaka.

Sera mbali mbali kwa pamoja za kitaifa na sekta zilizoainishwa changamoto zake ambazo ndio kikwazo cha kuimarisha maendeleo katika tasnia ya biashara Zanzibar zimeelezewa. Baadhi ya changamoto zilizoainishwa zinaonesha umuhimu wake kwa mahitajio ya uanzishwaji wa Mahkama pekee itakayoshughulikia masuala ya biashara. Vile vile kuna changamoto nyengine ambazo zinatoa muongozo wa mambo yanayohusiana na Mahkama ya Biashara inayotakiwa yafanywe kwa uhakika kwa zile changamoto kubwa ambazo zinakabiliwa katika maendeleo ya uwekezaji na ujasiriamali hapa Zanzibar.

Mswada huu wa Mahkama ya Biashara Zanzibar umeyazingatia mambo yote yanayorudisha nyuma suala la biashara hapa Zanzibar. Mswada huu Mhe. Naibu Spika, umeyatizama matatizo yote yale kwa maana hiyo basi, kutoa mwelekeo mzuri wa jinsi gani matatizo ya kibiashara yanapotokea yaweze kusuluhishwa.

Kwa hivyo, madhumuni makubwa na muhimu katika mswada huu kwanza ni kusajili hukumu za maridhiano lakini la pili ni kuharakisha kesi hizi za biashara na hivyo kuwatia moyo wafanyabiashara kuendelea kufanya biashara hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu umegawika katika Sehemu Sita na una vifungu 41. Sehemu ya Kwanza ambayo ni Masharti ya Jumla imo katika kifungu cha kwanza hadi cha tatu ambavyo ni mswada, jina fupi na matumizi pamoja na ufafanuzi.

Lakini Sehemu ya Pili inahusu masharti ya utawala na ina vifungu kuanzia cha nne hadi cha tisa ambavyo vinazungumzia kuanzishwa kwa Mahkama ya Biashara, mamlaka yake, muundo wake, kuanzishwa kwa kamati ya watumiaji wa Mahkama ya Biashara, Wafanyakazi na Mahkama pamoja na vikao vyake.

Sehemu ya Tatu Mhe. Naibu Spika, inahusu ufunguaji wa kesi katika Mahkama ya Biashara, kutunzwa kwa daftari la kesi na ugawaji wa kesi, sehemu hii inaanzia kifungu cha 10 hadi cha 12. Mhe.

Mhe. Naibu Spika, Sehemu ya Nne inahusu vikao vya kabla kusikilizwa kesi na Sehemu ya Tano ni utaratibu mzima wa usuluhishi ambayo imeanza kifungu cha 18 hadi 36. Vifungu hivyo vinafafanua utaratibu wa kupeleka kesi kwa ajili ya usuluhishi, kuhudhuria usuluhishi huo, kushindwa kuhudhuria, wajibu wa msuluhishi, muda wa usuluhishi na mwisho wa usuluhishi. Pia utaratibu umewekwa iwapo usuluhishi umeshindikana hatua gani nyengine zinaweza zikachukuliwa ili kulimaliza suala hilo baina ya wafanya biashara hao. Masuala ya ushahidi ukiwemo ule wa teknolojia, kinasa sauti na video pia umefafanuliwa jinsi ya kuutumia.

Mhe. Naibu Spika, Sehemu ya Sita na ya mwisho ni masharti ya jumla na yameanzia kifungu 37 hadi 41, sehemu hii inazungumzia uteuzi wa Naibu Mrajis na uwezo wake, matokeo ya kiapo chenye kasoro, uwezo wa Jaji Mkuu kutunga kanuni na pia imeelezea uwezo wa waziri kutunga kanuni ili kuleta utekelezaji bora wa sheria hii.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, jadweli inaonesha muundo wa taarifa ya mkutano wa awali kabla ya kesi kusikilizwa na ada zinazopaswa kutozwa katika Mahkama ya biashara.

Mhe. Naibu Spika, kwa kifupi huu ndio utaratibu mpya ambao tunahisi kwamba, sheria hii inapojadiliwa na kupitishwa basi yale matatizo ambayo hivi sasa yapo aya wafanyabiashara kwenda kwenye kesi za kawaida. Kwenye ule mdorongo wa kawaida katika Mahkama utapunguza sana shughuli za utendaji wa kibiashara. Kwa hivyo, inapopitishwa sheria hii Mhe. Naibu Spika, wafanya biashara wote kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizowekwa unaweza ukaja ukafungu kesi katika Mahkama maalum hii ya Biashara na kesi zao kusikilizwa haraka haraka na hivyo kweza kuendelea na biashara zao kwa haraka.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wanjubtaka waujadili mswada huu na waweze kuupitisha ili tuwe na sheria ya Mahkama ya Biashara kwa kusaidia suala zima la biashara. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Panya Ali Abdalla (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa Mbingu na Ardhi, kwa kutujaalia kukutana kwa mara nyengine tukiwa wazima wa afya ili tujadili masuala muhimu, likiwemo suala hili la kujadili Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mahkama ya Biashara Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi, kuhusiana na Mswada huu ambao hivi punde tunategemea kuujadili kwa kina.

Aidha, nimpongeze Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakari na watendaji wote wakiongozwa na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mdungi Makame kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupa wakati wa kuupitia na kuuchambua Mswada.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2012, kifungu cha 83 (5) ambacho kinasomeka kama ifuatavyo:

“Kamati iliyopelekewa mswada kwa mujibu wa kanuni hii inaweza, kumualika mtu yeyote afike kutoa maoni yake mbele ya kamati hiyo, kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wake kwa mswada husika”

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla vifungu hivi vinatoa fursa ya kuwaalika wadau wa sekta husika katika kutoa maoni yao kuhusiana na Mswada husika, Kamati ilifanya hivyo kama Kanuni ilivyoelekeza ambapo wadau wa Sekta ya Sheria na Sekta ya Biashara walifika na kutoa maoni yao kuhusiana na Mswada huu. Kwa msingi huo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa wadau wote walioshiriki kutoa maoni yao ambayo yameisaidia sana Kamati katika kufanya marekebisho haya na kuweza kuuboresha mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati yetu kwa michango yao ya kina waliyoitoa katika kazi zetu za Kamati pamoja na mashirikiano makubwa waliyonipa wakati wote Kamati ilipokua ikichambua na kuujadili Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	Mjumbe
5.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Mjumbe
6.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
7.	Mhe. Mohammedraza Hassanali	Mjumbe
8.	Ndg. Latifa Saleh Suleiman	Katibu
9.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	Katibu

Mhe. Naibu Spika, baada ya dibaji hiyo sasa naomba nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusiana na Mswada kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuunda Mahakama maalum inayohusika na masuala ya kibiashara. Hatua hii ni muhimu kwani itasaidia kuondosha malalamiko mbali mbali yaliyokuwa yakijitokeza yakiwemo ya ucheleweshaji wa kesi na haki kwa wanaolalamika au kulalamikiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Mswada huu, Mamlaka ya kusikiliza kesi za maswala ya kibiashara yatasikilizwa na Mahkama ya Baiashara kama Divisheni ya Mahakama Kuu na hivyo kutoa nafasi ya kupata maamuzi ya haraka kwa vile mrundikano wa kesi hizo utaondoshwa katika Mahkama Kuu. Hali ambayo italeta maendeleo makubwa katika sekta ya Biashara Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuupitia Mswada huo, Kamati yetu imependekeza kufanyiwa marekebisho kwa baadhi ya vifungu kwa lengo la kusaidia kuimarisha Mswada huo wa Sheria. Mfano wa vifungu hivo ni kama ifuatavyo:- Katika sehemu ya kwanza ya Mswada, kifungu cha 2 (2) mstari wa pili kutoka juu neno “Suraq” liliopo baina ya neno “madai” na “ya” lisomeke “Sura”, katika tafsiri, kifungu cha 3 (j) mstari wa kwanza kutoka juu neno “ya” liliopo baina ya neno “uamuzi” na “Mahkama” lisomeke “wa” , katika tafsiri ya neno mapitio ya Mahkama mstari wa kwanza kutoka juu neno “miendendo” baina ya neno “yanajumuisha” na “ya” lisomeke “mienendo” katika tafsiri neno “Mrajisi” lisomeke “Naibu Mrajis”.

Mhe. Spika, Kamati imependekeza pia katika sehemu ya sita katika kifungu cha 40(1) mstari wa kwanza kutoka juu yaongezeke maneno “kwa kushauriana na kamati ya watumiaji wa Mahakama ya Biashara” baina ya neno “Mkuu” na “atakuwa”.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa majadweli Kamati imependekeza Jadweli la kwanza I, lisomeke jadweli la II na maelezo yanayoeleza Ada za Mahakama, yasomeke kama Jadweli la I.

Mhe. Naibu Spika, kimsingi huo ndio muhtasari wa Kamati kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mahakama ya Biashara Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo na mengine yataonekana katika waraka wa marekebisho uliowasilishwa mbele ya Baraza hili. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili nao wauchangie Mswada huu kwa madhumuni ya kuuimarisha zaidi na hatimae kuukubali na kuupitisha.

Mhe. Naibu Spika, natamka bayana kuwa mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi asubuhi ya leo kuweza kutia Baraka hizi kwa Mswada huu wa Sheria ya kuanzisha Mahkama ya Biashara unaotokana kwa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Kwanza nimshukuru yeye pamoja na watendaji wake kwa kuona hiki kitu kuwa kina umuhimu hasa kwa maslahi ya Wazanzibari wote wale ambao wanaendesha biashara.

Mhe. Naibu Spika, kama tutakuwa na kumbukumbu hasa kitu hiki mimi nimewahi kukisema katika bajeti na wengi wao waangalie *hansard* yangu, sema itakuwa tafsiri ya neno hili na lile langu mimi ni tofauti kidogo lakini lengo ni lile lile nililokusudia.

Mhe. Naibu Spika, katika bajeti iliyopita ilikuwa sana ninawatetea wale wawekezaji wanaofanya biashara Zanzibar kwa misingi mikuu zaidi ambayo tunayowafanyia wao kutowatendea haki, kuwanyang'anya mali zao na nikasema ni bora serikali iangalie kutafuta sheria ambayo itakuwa *independent* na mchanganyiko na Mahakama nyengine ili ipate ufafanuzi mzuri iende kesi kwa utaratibu kuliko hivi sasa zinavyokwenda kesi hizo zinachukua muda mrefu yule mtu atakuwa amekopa pesa mabenki ya nje hatimaye anapata *penalty* anafilisika, kwa kweli tunamtia majozi. Lakini leo Mhe. Naibu Spika, Mwenyezi Mungu ameleta Baraka zake kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, mawaziri wa aina kama hii ambao wanakuwa wanaona lazima nchi yetu iende na wakati na sheria basi mimi husema siku zote Dr. Ali Mohammed Shein anakuwa hakukosea kuwachagua watu kama hao. Kwa sababu ni watu ambao wana upeo na wakilala wakiamka wanatuletea vitu ambavyo vitaweza kuiwezesha nchi yetu iwe katika mkondo wa sheria kwa mujibu wa hivi tunavyokwenda.

Mhe. Naibu Spika nina furaha kubwa sana na ndio maana najitahidi kusema kidogo kidogo kwa sababu hiki ni muhimu sana kuwekwa sheria hii ya biashara Mahkama hii kuwepo hapa Zanzibar ni kitendo cha kupigiwa mfano kabisa katika kupatikana na sisi sasa tumefikia malengo makubwa sana. Lakini pia katika sheria hii kuna mambo inapaswa lazima nimuulize Mhe. Waziri ili kupata ufafanuzi zaidi hasa nikienda katika ukurasa wa 367 kifungu (k)

Kifungu hicho kinasema kwamba, "mwenendo wa mashauri ya kibaharia". Hapa ningemuomba Mhe. Waziri anitafsirie hii lugha ya kifungu hiki, kila nikijaribu kutaka kufafanuza kwa upande wangu kwa sababu kila mtu akili anazo na mtazamo wake. Nina historia nzuri tu, labda nikieleza Mhe. Waziri atakuja kuniweka sawa, mabaharia na wao nilisema labda ni miongoni mwa wafanya biashara au wanafanyiwa biashara. Kwa sababu wanaajiriwa kwenye vyombo na wao na wafanya biashara. Sasa hapa tafsiri itaingia na wao ni wafanya biashara au wao wanafanyiwa biashara? Kwa sababu na wao wana mizozo na wenye vyombo huajiriwa na halafu wakatelekezwa hata mikataba wanakuwa hawapewi na pengine wanajua wapi waende sasa hizi sheria sijui itakuwaje, waelekee kwenye sheria za kazi au waelekee katika sheria hii ambayo tunataka kuipitisha hapa ya biashara?

Sasa hapa namuomba sana Mhe. Waziri atutafsirie haya mambo yasije yakagongana. Huo ndio mtazamo wangu kwa sababu ikiwa nao wataingia katika Mahkama hii ya biashara basi niseme ni pahali pazuri kwa sababu na wao mpaka sasa hivi kesi zao bado zinasuasua kwa sababu kunakuwa na kesi nyingi za wafanyakazi wa Zanzibar wakiwemo na wao hatimaye hakuna kinachokuwa na wao kupata faida, vyombo vinauzwa, haki zao hawapati mabaharia hao. Sasa naomba sana Mhe. Waziri akija hii sentensi aniwekee vizuri sana ili niweze kuja kumpitishia kifungu hiki kwa vizuri kabisa.

Lakini nikishuka chini hapo kwa kuendelea na kifungu hiki hiki anasema kuna migogoro ya biashara maana yake ni migogoro inayojumuisha mambo ambayo yataonekana na Mahkama kuwa ni muhimu kibiashara kama yalivyoainishwa katika sheria hii. Nayo hii ningemuomba vile vile Mhe. Waziri tafsiri hii ya kifungu hiki kuna

migogoro ya aina nyingi sana, kuna migogoro ya ardhi ikiwemo ndani ya biashara, kuna migogoro ya biashara mbovu kuletwa, sasa hapa napo ningemuomba sana Mheshimiwa ajaribu kunisaidia hii migogoro ya aina ngapi. Na sio vibaya hata akaweza kutwambia kwamba mgogoro wa kwanza una hivi, wa pili uko hivi, wa tatu uko hivi inategemea mwenyewe atavyoona kuwa migogoro hiyo iko ya aina nyingi.

Mhe. Naibu Spika, nikiingia katika ukurasa wa 368 hapa inavyoonesha kuanzia hapa ndio hiyo Mahkama yenyewe sasa ndipo tunataka kuanza kuiunda. Mhe. Naibu Spika, mimi nawauliza wakubwa wangu tuko *serious* na sheria hii? Tumeangalia kwa uangalifu sheria hii?

Mhe. Naibu Spika, kutunga ni kutunga tutaitunga hapa sheria *In shaa Allah* Mwenyezi Mungu akitujalia tutaipitisha hakuna tatizo lolote, Mhe. Rais wetu kwa mambo kama haya halilali atatia saini tu, utekelezaji je. Sasa hapa mimi nawaambia sheria hii jamani kama wapo viongozi wameshaanza kunyang'anya watu sheria hii itawabana. Tuwarudishie haraka sana mali zao hao wawekezaji wetu jamani vyenginevyo vyovyote sheria hii itatukumba. Wale viongozi tuliojikumbia maardhi yale tuliofuta futa tukawanyang'anya wawekezaji kwa kutaka kufanya biashara zao tumejitia ndio sisi sheria hii sasa ipo haraka sana urejeshe. Mhe. Naibu Spika, haraka sana wayarejeshe maeneo ya watu ya biashara walioyachukua kwa kuwanyang'anya wawekezaji na ndio maana nikasema sheria hii tunaiunda Mhe. Waziri aliona hilo amefanya *study* kubwa sana maana yake ameanzia kupitia katika Mabaraza huko akazunguka kwenye maeneo gani ndio akaona hii sasa ni wakati wake kuundwa sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa hali ngumu wafanyabiashara wengine tunawadhalilisha wananyang'anywa vitu vyao vinavurugwa vurugwa tu na watu wa Manispaa bila ya kutumia utaratibu, bila ya kuchukua haki ya kwenda kuwapeleka Mahkamani wao wanavuruga. Mhe. Naibu Spika, nacheka kiuchungu sicheki kwa furaha, si mchezo sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi niipongeze sana Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar ina wataalamu wazuri sana, ina wanasheria wazuri sana, lakini inakuwa utaalamu wao hatuutumii Mhe. Naibu Spika, kiipasavyo hasa katika kurekebisha sheria na kutunga. Sasa inakuwa ni sawa sawa kuja hapa sisi kazi yetu kupiga kofi na kuondoka. Lakini nakuambieni Waheshimiwa wenzangu wa Baraza hili la Wawakilishi sasa tubadilike tuwe wakali sana na maana ya kuwa wakali sana sisi ndio tulinde na tutetee hizi sheria tunazopitisha vyengine vyovyote kiapo mlichokula pale mkasema *Wallahi Laadhim* na kila kitu tutatetea utatuhukumu, si kitu cha masihara Mhe. Naibu Spika, msahafu ule mbaya sana kwa sababu wewe unapotoka nyumbani unatia udhu kwa kwenda kuapa na unakamata msahafu wenye majina ya Mwenyezi Mungu, unamshirikisha Mwenyezi Mungu halafu leo tunatunga sheria hii haifanyi kazi, jamani mimi mwenzenu ninasema Mwenyezi Mungu atanihukumu kwa mengine tu lakini nitajitahidi mpaka ninamaliza kwa kuwatetea wananchi na nitalinda hii ambayo miswada inayopitishwa hapa. Sasa nimeifuta kabisa, nitakwenda sambamba na miswada hii tunayoipitisha hapa Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nikenda ukurasa 370 mkutano kabla ya kusikiliza kesi kwenye kifungu cha 14 (1) Mahakama inayoweza wakati wowote kabla ya kusikiliza kesi kuelekeza wadau kuhudhuria katika mkutano wa kabla kusikilizwa kesi kuhusiana na mambo yaliyojitokeza katika kesi na mwenendo. Mhe. Naibu Spika, mimi ninakubaliana nacho kifungu hiki. Ni uungwana huo kwa sababu kabla ya kesi malalamiko yanayopelekwa kwanza utaitwa na kuambiwa kuna hili shauri limeletwa Mahakamani lina moja mbili tatu, jee wewe una maoni gani. Mimi ninakubaliana nacho kifungu hiki.

Huyu aliyeona hivi ni mjuzi sana Mhe. Abubakar ningekuwa na uwezi mimi ningesema niletee mimi nimpandishe cheo kwa sababu kuna mambo ambayo tunatunga sheria lakini hazina za kupoozea, lakini Mahakama hii ina kipoozeo kwanza, halafu ndio unafikishwa kule Mahakamani. Hata ukifika huko tena umeshakuwa sugu wewe, na sheria hii itawalinda sana wakubwa kwa sababu kwanza ataitwa pale, ataambiwa wewe kwa nini ukamnyang'anya huyu ardhi, kishindo ndio hapa kwenye kifungu hiki, tushawastiri hapa sawa sawa, akitaka ataacha hukutaka atapelekwa mbele ya safari. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 371 kifungu 17 (1) kesi zote za biashara zitasikilizwa kwa kumalizwa ndani ya miezi 10 tokea kuanza shauri. Mheshimiwa hii ndio raha, tuwe na muda wa kumaliza hizi kesi kwa sababu leo nikikwambia kuna watu wamenyang'anywa hapa ardhi wazungu wanahangaika hivi sasa, wana miaka mitatu mpaka minne hawajui kesi yao itakwisha lini. Lakini leo tutakuwa na muda atajua kuwa kesi yangu kwa mufa fulani imekwisha kupata na kukosa. Mheshimiwa hii nzuri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hili jambo mimi limenifurahisha sana. Lakini kifungu cha 100 kinasema kuna uwezekano vile vile wa kuongeza lakini sio mbaya, inategemea na ule uzito wa kesi yenyewe. Mhe. Naibu Spika, ninashukuru sana kwamba Wajumbe wangu wananielewa na ndio maana wakawa wanapiga kofi kwa kufurahikia hiyo na kuogopa Msahafu. (Makofi).

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa wa 374 kwenye neno linaloitwa usiri. Mawasiliano yoyote katika vikao vya usulushi na kumbumbu, mheshimiwa nalo kama nilivyosema kwamba miswada mingi ya sheria ambayo tunapitisha lakini huu ni modern wa aina yake. Kuna vifungu ambavyo mimi sijapata kuviona machoni mwangu hata kuvipitisha.

Sasa hapa Mhe. Naibu Spika, nimeona na hasa hili neno la usiri. Mhe. Naibu Spika, mimi ninakubaliana nacho kifungu hiki chenye neno usiri na wala sina tatizo nacho.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutaka kumalizia ili kuashiria kuwapitisha wenzangu niende kwenye kifungu cha moja kwa moja kifungu cha Mahakama itakuwa ya Kiswahili ama kiingereza, mimi ninakubaliana nacho. Mhe. Naibu Spika, mimi mara nyingi sana huwa ninapiga kelele suala la lugha, kwa sisi Zanzibar wengi tunatumia lugha yetu ya Kiswahili. Lakini wengi hivi sasa wafanyabiashara ambao wanafanya kazi ndani ya Zanzibar ni wote ni watalamu ambao tayari wana lugha ya kigeni.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninakubaliana nacho sana wala sina pingamizi nacho na ikiwezekana kabisa kwa sababu wengi hivi sasa tuna Wataliana nao wanafanya biashara ndani ya Zanzibar hii, si vibaya Mhe. Abubakar ukaongeza na Kitaliana, kwa sababu wapo na ipo haja hata Jaji mmoja ukenda kumsomesha naye akajua lugha ya Kitaliana hujapoteza kitu. Kwa sababu wengi hawa na hasa ndio wengi tunaowanyang'anya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, wanapata shida sana tafsiri zile wanapata taabu. Sasa na hii Mahakama yako si vibaya nayo ukamuweka Jaji mmoja akajua lugha ya Kitaliana ili kwa kuleta ufanisi mzuri na sheria yako ikawa nzuri ukaileta hapa. Tunaomba sana hilo Mhe. Naibu Spika, lifikiriwe.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema hapo mwanzo kuna mambo mengine itabidi nitake nipate tafsiri nzuri ili baadae niweze kupitisha vizuri. Kwa kuwa mimi sina dosari nao mswada huu, kwa vile huku nyuma nilisema kwamba lazima tuwe na *special* mahakama hizo ambazo zinazoleta usumbufu kwenye mahakama za jamii na mambo mengine.

Sasa leo nishukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mambo kama haya watu wa Jimbo la Kitope wanapenda sana na ni mambo ni muhimu na wananchi wangu ni wafanyabiashara na wao, sasa wanajua na wao tutawapeleka wapi matatizo yao yanayotokezea ili tukapata sheria ambayo itakayowasaidia wao.
Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, naomba niunge mkono mswada huu asilimia mia kwa mia.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mshimba kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe nina jina moja Mhe. Ussi Jecha Simai, kwa hivyo naomba anayetaka kuchangia alete ili tuweze kwenda uzuri.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada uliopo mbele yetu hapa, lakini pia niwapongeze watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuandaa mswada mzuri sana ambao leo mimi naamini utapita bila ya matatizo yoyote kutokana na umakini uliotumika kwenye kuandaa mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, pia niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi ikiwemo kuzitengeneza na kurekebisha sheria mbali mbali kwa ajili ya kuleta ufanisi.

Baada ya utangulizi huo Mhe. Naibu Spika, awali ya yote ningeliomba kwamba Mahakama ya Ardhi nayo ingeliondolewa kule iliko ikaletwa katika divisheni ya Mahakama Kuu ili kuweza kuleta ufanisi zaidi kutokana na kuona kuwa uhalisia Mahakama hii haipo pahala pake panapostahiki, kwa sababu imo katika sehemu ya serikali kwa upande mmoja.

Mhe. Naibu Spika, tukija moja kwa moja kwenye mswada huu, mimi kwanza ningeliomba kifungu cha 3 ambacho kinazungumzia tafsiri tungelitoa maana ya watumiaji wa Mahakama ambapo kamati yake hii imeoneshwa katika kifungu cha 7 imetaja watu hawa.

Basi ingekuwa ni vyema kwamba tukatoa maana ya watumiaji wa mahakama. La pili vile vile katika kifungu cha 16 na maeneo mengine pia yamo kuna neno "mdawa" na neno jengine "wadawa". Neno hili halipo maarufu sana hasa kwa watu ambao hawajui lugha za kisheria. Kwa hivyo lingelitolewa tafsiri ambayo inafahamika vizuri ikajulikana hili neno mdawa au wadawa ina maana gani hasa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kifungu cha 8 kinazungumzia wafanyakazi wa Mahakama. Huku nyuma uzoefu uliopo kwamba baadhi ya wafanyakazi wa Mahakama Kuu kwamba wao wanakuwa sio sehemu ya Mahakama. Tume ya Utumishi wa Mahakama haiwatambui kama ni sehemu ya Mahakama jambo ambalo kwa kiasi kikubwa sana linawapelekea kuwanyima haki zao nyingi za msingi hasa yakiwemo masuala ya maslahi. Sasa sijui hapa Mhe. Waziri atatueleza hawa watumishi wa Mahakama wao kwa mujibu wa sheria hii watakuwa ni sehemu ya Mahakama ambapo zile haki na fursa wanazopata watendaji wa Mahakama na wao watazipata ama laa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kifungu cha 35 kinazungumzia maandishi madogo ya pembeni yanazungumzia suala la katazo la vinasa sauti. Sijui hapa hekma yake ni nini kwa sababu tunajua Mahakama hii itakuwa ni miongoni mwa Mahakama huru na za haki ambapo watu watakuwa na haki na fursa ya kupata zile taarifa kwa ajili ya kuzitoa. Basi hekma yake ni nini kuweka lile katazo na ikatoa masharti pengine mpaka ipatikane ruhusa ya Mahakama.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa leo mchango wangu ningelifikia hapa na niseme moja kwa moja tu kwamba naunga mkono mswada huu, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chaani ambapo miongoni mwao wengi ni wafanyabiashara kwa ajili ya kuwasaidia sheria hii katika kufikia malengo ya kuzipata haki na fursa zikatolewa na Mahakama hiyo.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi asubuhi hii kupata nafasi ya kutoa mawazo yangu machache juu ya mswada huu uliopo mbele yetu.

Kwanza Mhe.Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha asubuhi hii kufika katika kazi yetu kuendelea katika majukumu yetu ya kawaida. Aidha nikushukuru wewe binafsi, Waziri wa Sheria na Katiba na watendaji wake kwa kutuletea mbele yetu leo mswada huu ambao kama ukipita utakuwa ni sheria ya Mahakama ya Biashara.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwenye tafsiri na nichukue neno moja tu ili nimshauri katika kifungu cha 3, naomba nisome hilo neno lenyewe mshauri. Mshauri maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Kamati ya Utumiaji Mahakama ya Biashara ili kukaa na Jaji katika kuamua kesi za biashara. Sasa huyu mshauri Mhe. Naibu Spika, ningependekeza na yeye kwa kiasi Fulani awe na taaluma ya sheria. Kwa sababu yeye atakaa pamoja na Jaji katika kutengeneza kesi.

Mhe. Naibu Spika, huko nyuma niliwahi kuziona kesi za kawaida, kuna Jaji au Hakimu na Washauri wake wanaokaa, bahati wote hawana taaluma ya sheria. Mara moja nilishuhudia kesi ya wizi wa muhogo, mwizi kapelekwa pale Mahakamani, limesomwa kosa lake, kalikataa. Kwa bahati njiani kapita mtu Jaji kaamuru yule wa barabarani aitwe, alipoitwa akaambiwa yule mshtakiwa kwa nini huyu hayupo hapa ndipo pale aliposhtakiwa, Hakimu akajibu mwenyewe kwa sababu hajaiba, kwa hivyo wewe upo hapa kwa sababu ulikuwa umeiba.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ilibidi lile shina la muhogo aliloiba lihesabiwe lina vipande vingapi. Shina lile lilikuwa na vipande vya muhogo kwa hivyo kila kipande kilimfunga mwaka mmoja na mshauri naye akaongeza miezi yake sita. Hawa ndio waliokuwa washauri wa jadi. Kwa hivyo sasa tutokane huko tusiwe na washauri ambao wa aina hiyo, kwa sababu Mahakama inakwenda kisheria na hawa washauri wawe ni watu ambao wanaoelewa sheria.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa Mahakama zitakuwa nyingi, kila siku zinaongezeka. Tuna Mahakama ya Kazi, Mahakama ya Watoto, Mahakama ya Ardhi na leo inakuja hii ya biashara. Huko nyuma tulikuwa na Mahakama za

kawaida, kuanzia Mahakama ya Mwanzo, Wilaya, Mkoa hadi kufikia Mahakama Kuu. Jee, nimuulize Mhe. Waziri anao Mahakimu wa kumudu Mahakama zote hizi, kwa sababu zote hizi zinahitaji kuwepo na Mahakimu na Majaji mahiri kabisa watakaoweza kutoa huduma za kimahakama, isiwe kama huo mfano nilioutoa wa shina moja la muhogo mtu kumfunga zaidi ya miaka niliyoitaja.

Sasa vile vile Mhe. Naibu Spika, hii Mahakama ya Biashara kwa kiasi fulani ina mipaka ya hizi kesi ambazo inashughulikia. Kwa sababu niende kwenye kifungu cha 5(1) ukurasa wa 368, unasema hivi "Bila ya kujali sharti lolote la sheria hii Mahakama ya Biashara haitokuwa na mamlaka ya pekee katika kutatua migogoro ya biashara.

Ina maana Mahakama hii ina *limit*, kwa hivyo kwa kiasi fulani haina mamlaka. Ina maana kuna baadhi ya kesi za biashara Mahakama hii inabidi wasiweze kushughulikia. Jee, kama wao, sheria tunataka kuianzisha leo lakini tayari ina mipaka maalum iliyopangiwa. Jee, ni kesi zipi ambazo Mahakama hii ambayo inaanza leo iwe haiwezi kuzimaliza migogoro yake. Mahakama ndio kwanza inaanzishwa lakini ndio mwanzo inapewa hiyo mipaka. Kwa hivyo hili nalo ningemuomba Mhe. Waziri kadhalika anisaidie, kwa nini kukawa kuna mipaka hiyo na kesi hizo zinahusu kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, kadhalika katika kifungu cha 17 (1) ambacho pia Mhe. Mshimba alikizungumza ukurasa wa 371, kesi zote za biashara zitasikilizwa na kumalizwa ndani ya miezi 10 tokea kuanza lakini hazitozidi miezi 12. Hili ni suala zuri kwa sababu hivi sasa katika Mahakama zetu kuna kesi kadhaa ambazo zimerundikana bila ya kupatiwa ufumbuzi. Kwa hivyo kama Mahakama hii ya Biashara imeekewa mipaka kesi mpaka muda, kwa hivyo ni vyema Mahakama nyengine zote nazo zitungwe sheria ya kuimaliza zile kesi ili kupunguza msongamano au mrundikano wa kesi katika Mahakama zetu.

Mhe. Spika, ingawaje kifungu kilichobakia chini kimetoka inaweza ikaongezwa muda huo pindipo mmoja kati ya wanaohusika ataomba kuongezwa kwa muda na Mahakama itaweza kuzingatia kulingana na kesi yenyewe ilivyo. Kwa vyovyote hii ni rai nzuri ya kuweka muda lakini ningeomba huo muda uliopangwa uzingatiwe, tusipange muda hatimaye ikawa ni kikwazo ikawa bado bado.
Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema machache naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa na mimi kuuchangia mswada huu muhimu uliopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, na pia baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba nimpongeze Waziri kwa kutuletea kitu hiki muhimu, mswada huu wa kuanzishwa Mahakama ya Biashara. Kwa kweli huu mswada ni muhimu sana na utatusaidia katika kuendesha nchi yetu na watu wetu.

Mhe. Naibu Spika, Mahakama hii ya Biashara kama nilivyozungumza ni muhimu hasa ukizingatia kama sheria zote za nchi zinahimiza kama anatakiwa mtu yeyote yule anapofanyiwa kitu asichukue sheria mikononi mwake ila aende kwenye vyombo vya sheria. Vyombo vya sheria ni hizi Mahakama. Kwa hivyo hii Mahakama itatusaidia.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, tunaona katika nchi yetu hii ya Zanzibar kila siku tunapiga kelele kama serikali inapunguza umaskini kuwaletea wananchi wake kuwaweka katika hali nzuri ya kimaisha lakini Mhe. Naibu Spika, kila siku huwa ninapata mashaka sana kama sisi katika kuwasaidia wananchi umaskini basi tunawakandamiza na kuwapa umaskini.

Mhe. Naibu Spika, vyombo vya sheria vipo lakini siku zote hatuchukui kwenda kwenye vyombo vya sheria, tunachukua sheria mikononi mwetu, tunaanza sisi viongozi kuchukua sheria mikononi mwetu badala ya kwenda kwenye vyombo vya sheria.

Mhe. Naibu Spika, wafanyabiashara wanajikomboa au wanajiondoa kupunguza umaskini, wanapofanya kosa vyombo vya sheria vipi, kwa nini tunachukua sheria mikononi mwetu kuwakandamiza. Mhe. Naibu Spika, jana kwa masikitiko wafanyabiashara wanaojisaidia wamekwenda watu wakachukuliwa vitu vyao vikapondwa pondwa na kuvurugwa vurugwa, wengine wakachukuliwa vitambaa vyao, tende zao. Kwa nini sheria zipo kama mtu kafanya makosa asifikishwe kwenye vyombo vya sheria, lakini leo tunawapokonya wananchi vitu vyao, kule ni kuwarudisha nyuma, mtu anapovunja sheria basi afikishwe kwenye vyombo vya sheria, unapomnyang'anya vitu vyake ukavichukua na kuvifanya kuwa ni vyako wewe, kule ni kumnyang'anya.

Sasa tunapoanzisha Mahakama hii nafikiri itatusaidia, kwa sababu siku zote mimi huwa nasema tunakuwa na mambo mazuri lakini utekelezaji wake unakuwa ni matatizo makubwa. Mhe. Naibu Spika, inasikitisha wafanyabiashara wanakopa pesa za watu tutawafunga wengi kwenye sheria hii, kwa sababu mtu ameshakwenda kukopa vitu vya watu, halafu serikali au taasisi inakwenda kuchukua vitu vya watu inavivurugavuruga, halafu mtu anafikisha Mahakama akafungwe bure.

Kama jana wafanyabiashara vitambaa vyao vyote vimechukuliwa, wale wa tende zao zimechukuliwa. Tunawapeleka wapi watu wetu. Mimi kila siku huwa nasema kwa masikitiko, anapovunja sheria mtu afikishwe kwenye vyombo vya sheria, tusiwachukulie vitu vyao tukawavurugia, tuwaelimisheni watu kwa utaratibu tuwapangie, kavunja sheria apelekwe kwenye vyombo vya sheria, lakini tusiwanyang'anye Mhe. Naibu Spika, kama hivyo ni makosa, tusiwafanye hivyo watu wetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo sasa nije kwenye mswada wenyewe. Mhe. Naibu Spika, miswada yote tunayopitisha labda Mhe. Waziri anieleze kwa sababu kifungu cha kwanza ni jina fupi hili, anasema sheria hii itajulikana kama ni sheria ya Mahakama ya Biashara ya Zanzibar Divisheni ya Mahakama Kuu ya 2013, na itaanza kutumika tarehe ambayo waziri ataitangaza katika gazetu rasmi au gazeti rasmi la serikali.

Sasa mimi nilikuwa nataka ufafanuzi tu kwa sababu sheria zote ninavyoona mimi ni kwamba inaanza kutumika mara tu anapoitia saini Rais huanza kutumika. Sasa hii waziri katueleza kama waziri atakapotangaza kwenye gazeti rasmi itaanza kutumika.

Sasa mimi nafanya wasi wasi labda sheria hii haikutiwa saini na Rais, akitangaza waziri tayari, kwa hivyo angetufafanulia kama itaanza kutumika atakapotia saini Rais na kutangazwa katika gazeti rami na waziri. Lakini kwa hivi inavyoekwa ni kwamba itatangazwa bila ya Rais kutia saini. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri labda atufafanulie zaidi atuweke sawa kwa sababu sheria zote tunazopitisha hapa zinakuja hivyo, kama itaanza kutumika mara tu Rais atapoweka saini.

Suala jengine Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri anisaidie ukusara wa 376 kifungu cha 36 kuhusu "Hukumu ya Mkato". Naomba Mhe. Waziri Mhe. Naibu Spika, anisaidie. Hapa bila ya kujali masharti ya amri, sasa hapa kuna nambari mimi sizielewi sijui wenzangu watanisaidia, naona kuna xx moja x. Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa sisi tuliokuwa hizi nambari hatuzielewi hatujui zimekusudiwa nini hapo. Kwa hivyo tungeomba Mhe.Naibu Spika, akija hapa atusaidie, kama ni nambari ambazo zimo kwenye sheria ambayo ni sheria mama iliyopita basi angetuwekea kwenye mabano akatuwekea hizo nambari tukajua, lakini kwa hapa mimi siambulii kitu, sijui wenzangu.

Kwa hivyo, naomba na hapa Mhe. Waziri atusaidie na atupe ufafanuzi zaidi.

Lakini na ukurasa wa 377 kifungu nambari 39 na hapo kinasema

> "Iwapo Naibu Mrajis atakuwa na maoni kwamba kiapo kinachoungwa mkono ombi au majibu ya kiapo kwa amri",

Kuna nambari kama zile zilizokuwepo pale. Walio wengi nafikiri hatuwezi tukazielewa kama zimekusudiwa nini. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atufafanulie zaidi au kama nambari hizi zimo kwenye sheria basi atuwekee na nambari kwenye mabano, ili tuweze kufahamu kama kakusudia nini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli sheria hii kama tulivyotangulia kuisifu kwamba ni nzuri na imekuja wakati ndio itatusaidia kuondoa matatizo mengi sana. Kwa maana hiyo mimi mchango wangu ni mfupi, naomba majibu kwa hayo ninayomueleza Mhe. Waziri, mara tu nikipata majibu basi naunga mkono mia juu ya mia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia kidogo mswada huu muhimu ambao Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ametuletea hapa mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuweza kufikiria jambo hili muhimu la kuandaa utaratibu huu wa sheria juu ya masuala yanayohusiana na biashara, eneo la kuandaa utaratibu huu wa sheria juu ya

masuala yanayohusiana na biashara, eneo ambalo tunalitegemea. Kwa sababu kama unavyojua visiwa vyetu hivi vya Zanzibar moja kati ya maeneo ambayo wananchi wengi wanajishughulisha ni maeneo ya biashara, visiwa hivi vinaendeshwa kwa misingi mikubwa sana ya kibiashara, na hasa uchumi wetu wa nchi pato lake moja kubwa nalo linategemea kodi inayotokana na biashara. Kwa hivyo, ni vyema sehemu hii ya eneo hili la wananchi nalo basi likawekewa utaratibu wa kisheria, ili liweze kwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu wa sheria uliopo mbele yetu unakusudia kuanzishwa kwa mahakama ya biashara ambayo itakuwa ni divisheni ya mahakama kuu ya Zanzibar. Jana tu tulipitisha mswada ambao unakusudia kufanya utanuzi wa Mahkama Kuu. Kwa hivyo, baada ya sheria ile kusainiwa na Mhe. Rais na Mhe. Waziri kuitangaza kwenye gazeti rasmi, basi pia tutapata nafasi ya kuanzisha mahkama hii ya biashara divisheni ya Mahkama Kuu.

Mhe. Naibu Spika, dhana hii ni nzuri, lakini tatizo linakuja kwenye utekelezaji wa dhana yenyewe. Kwa sababu tunazo mahkama nyingi pamoja na kwamba sio mahkama kuu ni mahkama za kawaida. Tunayo mahkama ya ardhi, tunayo mahkama ya kazi, tunayo mahkama ya manispaa inayoshughulikia kesi za manispaa kutoka mahkama ya mwanzo au vipi hatuelewi, kuna mahkama nyingi. Lengo la kuanzishwa mahkama hizi maalum zinazoshughulikia jambo maalum, ni kurahisisha shughuli ya utoaji wa haki katika maeneo yale na zaidi tukizingatia kwamba ni maeneo ambayo yanakuwa na misongamano ya kesi. Hilo ndio lengo kubwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini ukitizama lengo lenyewe na *practice* yenyewe basi ni tofauti. Kwa mfano sasa hivi Mhe. Naibu Spika, kumekuwa kuna msongamano mkubwa sana wa kesi zinazohusiana na masuala ya ardhi. Kuna kesi zaidi ya 300 ambazo zinasikilizwa na kuhitaji kutolewa hukumu. Mahakimu waliopo pale sasa hivi ni mahakimu nadhani ni wawili kama sikosei. Ukiangalia ugumu wa kesi zenyewe zinazohusiana na malalamiko ya ardhi, lakini na uzito zinazopewa mahkama hizi kwa kweli haulingani. Sasa badala ya kuanzisha mahkama hizi ili kutatua matatizo ya ardhi, matokeo yake sasa ule utatuzi uliokusudiwa unakuwa haufanyiki na yale madhumuni yalioanzishiwa mahkama ile yanakuwa hayawezi kutekelezeka.

Kwa hivyo, hilo kwa kweli ni tatizo na chombo chetu hiki cha mahkama kilione jambo hili, ili kuona kwamba yale makusudio ambayo tumekusudia kwa niaba ya wananchi wetu kusuluhishwa matatizo yao na migogoro iliopo basi iweze kufanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, tunaanzisha mahkama hii ya biashara, na kwa kweli mahkama hii na kwa mujibu wa maelezo yaliomo katika mswada huu wa sheria, tunategemea basi chombo hiki kitaendeshwa vizuri na hakitokuwa kama mahkama zile nyengine ambazo tayari zimeshaanzishwa.

Mhe. Naibu Spika, kwenye mswada wa sheria pana eneo moja hapa la kifungu cha 6 kinazungumzia muundo wa mahkama, ambayo inasema

Kifungu cha 6

"Mahkama itajumuisha

a) Jaji atakayeteuliwa na Jaji Mkuu miongoni mwa Majaji wa Mahkama Kuu,
b) Washauri wawili miongoni mwa watu walioteuliwa na kamati ya watumiaji wa mahkama ya biashara iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha sheria hii kwa kufuata utaratibu utakaowekwa na Waziri chini ya kifungu cha 41".

Lakini ukiangalia kifungu cha 7(1) kinaeleza kwamba kutakuwa na kamati ya watumiaji wa mahkama ya biashara ambayo itajumuisha majaji wa mahkama ya biashara, wakili mmoja anayeteuliwa na jumuia ya wanasheria wa Zanzibar, wakili wa serikali atakayeteuliwa na Mwanasheria Mkuu, mtu mmoja atakayeteuliwa na Jumuia ya Wafanyabiashara wenye viwanda na wakulima ya Zanzibar, na mwakilishi mmoja kutoka Wizara inayohusika na biashara. Hiyo ndiyo kamati ya watumiaji wa mahkama.

Sasa hapa kidogo Mhe. Waziri mimi nimechanganyikiwa nahitaji kupata ufafanuzi wakati utakapofanya majumuisho. Hii kamati ya watumiaji wa mahkama, kuna muundo wa mahkama, ambapo kwa mujibu wa sheria hii muundo wa mahkama hii utakuwa na watu watatu, Jaji Mkuu na hawa washauri wawili miongoni mwa watu walioteuliwa na kamati ya watumiaji. Hii kamati ya watumiaji, sijui lugha Kiswahili hakina utajiri wa maneno, lakini tunapozungumza kamati ya watumiaji ya mahkama katika sheria hii tunakusudiaje. Nimejaribu kuangalia kwenye *interpretation* huku mwanzo nikafikiri nitaikuta, lakini sikuiona.

Kwa hivyo, nilikuwa nahitaji kupata ufafanuzi juu ya hii kamati ya watumiaji ambayo ipo kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) ambayo imewajumuisha hawa watu ambao nimewazungumza hapa na ambao miongoni mwao wajumbe wawili ambao watakuwa washauri ndio watakaounda huo muundo wa mahkama. Sasa tunataka kujua hii kamati ya watumiaji ambayo itachukuliwa wajumbe wawili kupelekwa huku kwenye mahkama hii ya biashara, hawa watakuwa wanafanya kazi wakati gani, hasa inaposikiliza haya mashauri ni wakati gani, watakaa pamoja au watafanyakazi vipi, kwa sababu sijaona hasa hii kamati ya watumiaji ni kamati ipi na itafanya kazi wakati gani au itatoa ushauri wakati gani. Sasa nilikuwa nahitaji kidogo ufafanuzi juu ya mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ni kifungu cha 17(1) na (2) ambacho kinazungumzia uharakishaji wa kesi. Kesi zote za biashara zitasikilizwa na kumalizika ndani ya miezi 10 tokea kuanzwa, lakini hazitozidi miezi 12.

Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo zuri, kwamba mswada huu wa sheria unakusudia mahkama hii iwekewe muda wa kusikiliza kesi na hili ni jambo zuri kwa sababu litaweza kusaidia au kuharakisha kusikiliza hizi kesi zinazohusiana na biashara, na kwa sababu tumekuwa na mazoea kesi katika mahkama zetu zinachukua muda mrefu, miaka 2, 4, au 6 kesi hazijamalizika. Lakini tunapoweka muda wa kusikiliza kesi hizi za biashara naamini zitaharakisha kwa mujibu wa sheria hii kusikilizwa kesi na kupata maamuzi. Haidhuru kifungu cha 17(2) kinasema bila ya kujali sharti la kifungu cha 1 cha kifungu hiki, mahkama inaweza yenyewe kuongeza muda huo kulingana na mazingira ya kesi yenyewe, lakini kile kitendo tu cha kuweka muda naamini kitasaidia kuharakisha kesi hizi. Kwa sababu mbali ya kesi hizi za madai na kesi za jinai zinachukua muda mrefu. Wakati mwengine kesi zinaakhirishwa hata bila ya sababu yoyote ya msingi.

Mhe. Naibu Spika, unakwenda mahkamani unaambiwa hakimu wa kusikiliza kesi hii hayupo kasafiri, kwa hivyo, kesi inaakhirishwa mpaka siku nyengine, yaani kumekuwa na kawaida hiyo. Kwa kweli jambo hili linahitaji kuangaliwa kwa umakini. Dharura kwa binadamu inatokezea, lakini tuangalie na uzito wa mambo yenyewe na kwa sababu mwananchi anapofika mahkamani kusikiliza kesi, anakuwa na yeye amejizuia kufanya mambo mengine. Kama ni mkulima siku hiyo haendi kondeni, kama ni mfanyabiashara siku hiyo hawezi kufanya biashara kwa kesi inayomkabili. Sasa kama amethubutu kuacha shughuli zake nyingi na kwenda kusikiliza kesi, lakini anapofika pale pengine saa 3, 4, 5 au 6 anaambiwa kesi hii imeakhirishwa kwa sababu hakimu kasafiri, kwa kweli linakua sio jambo la kupendeza.

Kwa hivyo, wenzetu hawa wa mahkama wajitahidi kuona kwamba kesi zile siku zinazopangwa basi zisikilizwe, zaidi pale ambapo upelelezi umeshakamilika. Kwa sababu wakati mwengine huwa yanatokezea inaakhirishwa kesi kutokana na upelelezi kukamilika mara moja, mbili au mara tatu. Lakini wakati mwengine upelelezi unakuwa umeshakamilika, lakini tatizo linakuwa kwa chombo chenyewe. Kwa hivyo, mahkama hizi ziwasaidie wananchi katika kuona kwamba kesi zinaharakishwa kwa haraka zimalizike na uamuzi utolewe, ili kila mmoja ajue hukumu iliyotolewa na ni jambo gani ambalo sasa linamkabili mbele yake.

Kwa hivyo, kifungu hiki ambacho kiko kwenye mswada huu wa sheria ni kifungu kizuri na ni muhimu ambacho kitasaidia sasa kesi hizi kwenda kwa haraka. Pamoja na kwamba tutaona kuwa muda wa miezi 8 ni mingi, lakini angalau kuna *limit*, miezi 8 na isiyopungua miezi 12, angalau kuna *limit* kwa mwaka mmoja. Kwa hivyo, hii itasaidia kuharakisha kwenda kwa kesi hizi za masuala ya biashara.

Eneo jengine Mhe. Naibu Spika, ni kifungu cha 30 ambacho kinazungumzia lugha ya Mahkama. Naomba ninukuu inasema;

Kifungu cha 30

> "Lugha ya mahkama itakuwa ama Kiswahili au Kiingereza, isipokuwa kwamba mienendo yote ya mahkamani itanakiliwa kwa Kiingereza".

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar lugha rasmi ambayo itatumika nchi kwetu hapa ni Kiswahili, hiyo ndio lugha rasmi. Sasa kidogo mimi nimekuwa na mashaka ambapo inasema, kwamba mienendo yote. Nadhani mienendo sijui kama ndio *proceeding* au vipi wanakusudia nini, ya mahkama itanakiliwa kwa Kiingereza. Sasa kwa nini iwe kwa Kiingereza isiwe kwa Kiswahili, au iwe kwa lugha zote mbili kama tulivyotangulia kusema. Lugha ya mahkama itakuwa na hii "ama" ya mwanzo nadhani haikukaa pazuri. Ingekuwa lugha ya mahkama itakuwa ni Kiswahili au Kiingereza, sasa unasema ama Kiswahili au Kiingereza, sijui lugha zenu

za wanasheria maana miswada hii tokea jana tunaogelea miswada ya wanasheria. Lakini mimi ninavyoona katika lugha ya kawaida iseme kwamba lugha ya mahkama itakuwa Kiswahili au Kiingereza. Sasa unaposema ama Kiswahili au Kiingereza naona haijakaa sawa. Lakini zaidi ni hii mienendo ya mahkama ambayo inanakiliwa kwa Kiingereza basi iwe inanakiliwa kwa Kiswahili na Kiingereza au vinginevyo vyovyote itakavyohitajika. Kwa sababu kesi hizi zinaweza kuwa pamoja na za madai pamoja na wageni ni sawa, lakini na wenyeji ambao pengine hawafahamu Kiingereza vizuri na kwa sababu Kiingereza sisi sio lugha yetu. Wewe Mswahili utakapozungumza Kiingereza ni tofauti na utakapozungumza Kiswahili na kwa sababu Kiingereza sio lugha yetu ni lugha ya kigeni.

Kwa hivyo, hii Kiingereza iwe ni aula pale inapohitajika, lakini tujikite zaidi katika lugha ya Kiswahili inayofahamika. Wenzetu hawa wa mahkama wanapenda vizungu. Maneno ya Marehemu Mzee Karume, utakuta mkataba umeandikwa Kiingereza. Hivi juzi kulikuwa kuna *speech* yake ilikuwa inawekwa, ilikuwa mtu anaambiwa pale lete *document*, lete hivi na hivi. Hizi ni lugha tu za kujaribu kuwafanya watu wasielewe kile kilichokuwa kimekusudiwa mikataba kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza, wakati sisi wenyewe ni Waswahili, ni kuwafanya watu wasifahamu kile kilichopo. Kwa hivyo, lazima tubadilike tuandike lugha yetu kila mmoja aweze kuifahamu, sheria zetu ziandikwe kwa Kiswahili ili kila mmoja aelewe imekusudiwa nini, badala ya kuandika lugha za kigeni. Lugha za kigeni basi iwe ni aula pale inapohitajika, tusikimbilie zaidi lugha za kigeni. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hapa utakapokuja kufanya ufafanuzi basi nakuomba utuambie hizi lugha za kunakili zinakuwaje.

Lakini mwisho Mhe. Naibu Spika, kwenye jaduweli ya kwanza ya ada za mahkama. Mimi sina tatizo Mhe. Naibu Spika, viwango hivi ni *reasonable* ambavyo vitalingana na kesi zenyewe zinazolalamikiwa, sina tatizo ziko vizuri, zimezingatia hali halisi ya uchumi wa watu wetu na mambo mengine.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, mimi sina zaidi, namtakia kila la kheri Mhe. Waziri mswada huu uweze kupita vizuri, ni mswada wa kitaalamu wa kimahkama na wameutayarisha wao wenyewe kutokana na haja iliopo. Kwa hivyo, mimi sina mambo mengi zaidi humu. Naamini mswada huu umezingatia masuala mazima yanayohusiana na masuala ya kuendesha kesi za madai. Sisi sio wataalamu wa kesi, naamini hivyo. Kwa hivyo, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia na niwaombe wenzangu waujadili na baadae tuupitishe ili tupate nafasi ya kuanzisha mahkama hii ya biashara. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii. Lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kuwa katika hali ya afya na uzima, kwa mintarafu ya kujadili mambo yetu ya kila siku katika shughuli zetu za kiserikali.

Pia nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuuleta mswada huu ambao ni muhimu, ni mswada utakaomlenga mtafuta kula yake ya kila siku pamoja na familia yake. Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi kabla sijaingia kwenye mswada, nakuomba nizungumze machache ili huu mswada uweze kuchukua mkondo wake.

Mhe. Naibu Spika, tuna wafanyabiashara mbali mbali. Kwanza mimi nitamuomba Mhe. Waziri aje atufafanulie, maana hapa kumeandikwa tu biashara, lakini kuna biashara nyingi. Sasa nitamuomba Mhe. Waziri anifafanulie ni biashara ya duka, biashara ya mama ntilie, biashara ya kuuza uji au ni biashara ya nini. Maana biashara ina upeo mkubwa na ndio maana nikasema kwanza kabla ya kuchangia nitazungumza machache.

Mhe. Naibu Spika, tuna wafanyabiashara wetu hapa. Tuseme kama hapo Darajani tunawaita Jua Kali; wana biashara za mikononi wale watu, wengine wanatandika chini, lakini ukiiangalia hali halisi ya kuanzia Sokoni Marikiti ukaja zako kwenye daladala, kwa kweli ni jambo la kusikitisha, maana hata gari ukitaka kupitisha basi ujue ni namna gani ya kupitisha. Sasa mfanyabiashara yule kama mimi nimepita na gari yangu, nikavikanyaga vitu vyake vyote, si anatakiwa anishtaki. Sasa je, tumempangia mipango gani mfanyabiashara kama yule, ndio nikasema Mhe. Waziri aje anifafanulie hapa, biashara ina upeo mkubwa Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani tunapotaka kutunga sheria zetu au tukizipitisha hapa, basi taaluma iwe ni kitu muhimu. Tunapitisha sheria, kama mimi naweza nikaifahamu kwa hapa na pale, lakini kuna yule *layman* ambaye haifahamu ile sheria. Kwa hivyo, tutoe taaluma kwenye vyombo vyetu vya habari, ili kumsaidia yule mtu ambaye anataka kuijua hali yake ipasavyo. Kwa sababu sio kweli kwamba sheria hizi tutazigawa mpaka kwa watu wa maduka wote ili wajue haki zao ni kitu gani.

Mhe. Naibu Spika, huwa tunapiga kelele sana humu kwamba tunatunga sheria za kila aina, lakini kuisimamia sheria na utekelezaji wake na huo ndio wasi wasi wangu.

Mhe. Naibu Spika, amezungumza Mhe. Salmin Awadh Salmin kwamba tunayo Sheria ya Ardhi kuna kesi 300 na kuna wengine nadhani hao wanaodai haki yao wengine wameshafariki na hata watoto wao wameshafariki.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika ni imani yetu kwamba sheria hii itasimamiwa ipasavyo na hasa kile kifungu cha 17(1) ambacho wenzangu wamekitaja hapa na mimi nilikuwa tayari nimeshakichagua nikizungumze, ambacho naona nikinukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 17(1) kinaeleza hivi:-

> "Kesi zote za biashara zitasikilizwa na kumalizika ndani ya miezi kumi tokea kuanza, lakini hazitozidi miezi kumi na mbili".

Mhe. Naibu Spika, mimi naona mwenzangu na niungane naye mkono kwamba inaweza kutosheleza, maana ni mwaka, yaani kesi mwaka mzima pamoja na yote Mhe. Naibu Spika lakini nikubaliane kwamba isiyozidi miezi 12. Sasa hapa napo ni pahala muhimu Mhe. Naibu Spika, na ndio maana nikasema kwamba kwa kweli kuna haja hivi sasa kutilia mkazo hizi mahakama ambazo tunazitungia sheria tuhakikishe mahakama hizi zinafanya kazi zake ipasavyo.

Nikiendelea na mchango wangu naomba kidogo nirudi nyuma Mhe. Naibu Spika, maana yake ndio nikasema kwamba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anifafanulie vizuri ni biashara za aina gani kama ni za duka au mama ntilie narudia tena, kwa sababu kuna watu ambao kwa kweli na mimi nisifiche Baraza la Mji na maaskari wake wanawachukulia watu bidhaa zao.

Mhe. Naibu Spika mtu anatoka asubuhi anajua anakwenda pahala kuuza kitu ambacho cha kumuendeshea maisha yeye na familia yake na siku nyengine ni mwanamke na mimi namsemea sana mwanamke, ambaye ni mjane hana mume, watoto wake ni 6 na wote wanataka kusoma pamoja na kuangaliwa. Sasa mimi najiuliza sheria hii itachukua vipi mkondo wake, kwa sababu unapomchukulia mtu bidhaa yake, lakini imani yangu kwamba sheria hii ndiyo itakayomsaidia yule mtu ambaye amechukuliwa bidhaa zake.

Kwa hivyo, niseme Mhe. Naibu Spika, kwamba nimpongeze tena Mhe. Waziri kwa sababu kuna mambo mengine yanatendeka na hatuwatendei haki wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, mswada huu wenzangu wamechangia sasa na mimi kurudia yale kwa yale kama vile Mhe. Salmin Awadh Salmin amenifilisi kidogo sana nikasema kwa sababu nimeshaleta jina langu, basi na mimi nieleze mambo ya hapa na pale.

Baada ya kusema hayo, Mhe. Naibu Spika niutakie kila la kheri mswada huu, ili utakapotiwa saini na kukamilika basi uweze kuchukua mkondo wake na kuufanyia kazi ambazo zitaweza kumsaidia mfanyabiashara kufanya biashara yake bila ya uonevu wala matatizo. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuzungumza machache kuhusiana na Mswada huu wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Mahakama ya Biashara Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya njema, pia tumtakia rehema Mtume wetu Muhammad (*S.A.W*) zimfikie juu yake.

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu ambao ni muhimu kwa wananchi wa visiwa hivi vya Zanzibar, kwani watu wake asilimia kubwa ni wafanyabiashara katika kutafuta mahitaji yetu ya kila siku.

Kwa kweli mswada ni mzuri kwa sababu umetungwa na wanasheria ambao wenye uzoefu wa miaka mingi kuhusu sheria. Lakini hata hivyo tunataka baadhi ya wengine kutaka ufafanuzi zaidi kuhusiana na mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, nikianza moja kwa moja sehemu ya kwanza kuhusu utangulizi wa tafsiri kifungu cha 3, ambapo naomba kunukuu kidogo Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 3 kinaeleza hivi:-

> "Kesi ya biashara" maana yake ni kesi ya madai inayohusisha jambo linalochukuliwa na mahakama kuwa la kibiashara, ikijumuisha lalamiko lolote au ombi linalotokana na tendo la kibiashara lakini haifungiki na…"

Mhe. Waziri ameeleza hapa. Lakini hapa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje anipe ufafanuzi zaidi kuhusu hii kesi ya kibiashara, kwa sababu kama alivyosema Mhe. Asha Bakari Makame ni kuwa suala la kibiashara ni jambo ambalo lina uwanja mpana kabisa.

Kwa mfano, kuna biashara ya mtu mmoja mmoja, lakini kuna biashara za kampuni ambazo kuwa mahusiano yake ni hayo ya kimikataba, pia kuna wafanyabiashara wakubwa au wa nje wanaosema kwamba mtu wa nje kama vile wawekezaji pengine wanaotoka huko na kuja kufanya biashara hapa lakini hata na mabenki nazo pia zinaingia kwenye biashara.

Sasa hapa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja anipe ufafanuzi juu ya biashara gani ambazo zitahusika katika mahakama hii itakayofunguliwa ya biashara.

Mhe. Naibu Spika, zipo kero nyingi na kama tunavyosema kwamba wawekezaji ni watu wafanyabiashara wanapotoka kule wanakuja hapa kwa ajili ya kufanya biashara zao. Lakini hufikwa na changamoto mbali mbali na kesi zao hizi hazipatiwi ufumbuzi mpaka pengine mwekezaji yule afilisike atafute njia aondoke. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze kuhusu suala hili.

Vile vile kuna mabenki nazo zinafanya biashara, kwa sababu zinatoa mikopo kwa ajili ya kuwapa watu kwa lengo na manufaa yao wananchi, kwani benki lakini zinafanya biashara na wapo watu wanachukua mikopo na wala hawarejeshi. Je, mahakama hii itashughulikia matatizo yote hayo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba atakapokuja kufanya majumuisho, aje anipe ufafanuzi zaidi.

Jambo jengine ambalo nahitaji ufafanuzi ni kuhusu sehemu hii ya utangulizi, ambapo inaeleza juu ya migogoro ya kibiashara, maana yake ni migogoro inayojumuisha mambo ambayo yataonekana na mahakama kuwa yana umuhimu wa kibiashara kama inavyoonesha katika sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri itakuwa ni ile ile Mhe. Waziri, hivyo namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja hapa, ili niweze kufahamu vizuri.

Nikiendelea na mchango wangu sehemu ya pili kifungu cha 5 Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 5(1) kinaeleza hivi:-

5. "Mamlaka ya Mahakama;

(1). Bila ya kujali sharti lolote la Sheria hii, Mahakama ya Biashara haitakuwa na mamlaka ya kipekee katika kutatua migogoro ya kibiashara".

(2). Mahakama ya Biashara itakuwa na Mamlaka ya:

(a) Kusikiliza na kuamua kesi zozote za kibiashara kwa mujibu wa Sheria hii".

Mhe. Naibu Spika, sasa hapa pia nahitaji ufafanuzi kwa sababu huku imesema kuwa bila ya kujali sharti lolote la sheria hii, Mahakama ya Biashara haitakuwa na Mamlaka ya kipekee katika kutatua migogoro ya kibiashara.

Kifungu cha 3 naomba kunukuu kidogo Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 3 kinaeleza hivi:-

> “Mamlaka ya Mahakama ya Biashara yanaweza kutumiwa kwa malalamiko ya kibiashara”...

Mhe. Naibu Spika, hapa yanaweza au inaweza, yaani hiyo Mamlaka ya Mahakama ya Biashara au yanaweza. Hivyo, hilo pia nahitaji ufafanuzi Mhe. Naibu Spika.

Vile vile kifungu cha 7(1) ambacho naomba kunukuu kidogo Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 7(1) kinaeleza hivi:-

> “Kutakuwa na Kamati ya Watumiaji wa Mahakama ya Biashara ambayo inajumuisha Majaji wa Mahakama ya Biashara, Wakili mmoja anayeteuliwa na Jumuia ya Wanasheria wa Zanzibar, Wakili wa Serikali atakayeteuliwa na Mwanasheria Mkuu, mtu mmoja atayeteuliwa na Jumuia ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima ya Zanzibar na Mwakilishi mmoja kutoka Wizara inayohusika na Biashara”.

Kwa kweli sina matatizo na kifungu hichi, lakini kama kungelikuwa na maneno ya kuongeza hapa miongoni mwa wajumbe hao angalau kukakuwepo na mwanamke mmoja. Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi nadhani kingekaa vizuri, kwa maana hiyo namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba angalau pawe na mwanamke mmoja katika wajumbe watakaoteuliwa. *(Makofi)*

Sehemu ya nne Mhe. Naibu Spika, inayozungumzia kuhusu uwezo wa kutoa amri na maelekezo. Katika kifungu cha 13 na kwa sababu kwenye mahakama zetu nyingi haki za watu huchelewa. Kwa hivyo, katika kifungu hichi kwa ajili ya kuharakishwa kwa haki pamoja na kumaliza kesi kwa gharama nafuu.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri, kwa sababu katika mahakama nyingi tatizo la kurundikana kwa kesi ni kuchelewa kutolewa uamuzi wa kesi kwa haraka. Kwa mfano, kesi moja inaweza kuchukua hata miaka 10 na watu wanakwenda na kurudi na hatimaye watu kusamehe haki zao kutokana na kusumbuliwa nenda rudi. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri kuhusiana na kifungu hicho.

Jambo jengine la mwisho ambalo pia naomba kupata ufafanuzi kwenye sehemu ya sita kifungu cha 40(2), ambapo naomba kunukuu kidogo Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 40(2) kinaeleza hivi:-

> “Jaji Mkuu anaweza baada ya kushauriana na Kamati ya Watumiaji wa Mahakama ya Biashara kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi kuteua Jopo la Wasuluhishi wakishirikishwa katika hatua za usuluhishi, maadili na mahakama na watuma hati za mahakama”.

Mhe. Naibu Spika, tunajua kwamba binadamu yeyote anayo mapungufu yake. Sasa unapomwambia mtu kuwa Jaji Mkuu anaweza kwa kushirikiana na Kamati ya Watumiaji, kwa nini imeandikwa anaweza na asiambiwe kuwa Jaji Mkuu kwa kushirikiana na hao wanaokusudiwa kuteua Jopo la Wasuluhishi wa mahakama, kuliko kumwambia Jaji Mkuu anaweza na ukitizama kipengele hichi yeye ndio kazi yake.

Kwa mfano, hapa chini kinaeleza Waziri anaweza kwa amri atakayopitisha kwenye Gazeti Rasmi kutunga Kanuni, ili kuipa utekelezaji mzuri wa sheria hii. Sasa kwa nini isiwe Waziri atatunga Kanuni ambaye Waziri anaweza na akisema hawezi je. Kwa maana hiyo, sheria impe msisitizo mtu yule anayetakiwa kufanya suala lile kuliko kumwambia Katibu Mkuu anaweza, muainishe tu kuwa Katibu Mkuu atafanya jambo fulani kuliko kumwambia vile Jaji Mkuu anaweza. Mhe. Naibu Spika, Lugha ya Kiswahili ina tafsiri nyingi, kwa hiyo ni vyema kutuwekea Kiswahili ambacho kitatoa ufafanuzi zaidi katika suala lile hasa katika sheria.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache niseme tena kwamba ninampongeza sana Mhe. Waziri na naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia mswada uliopo mbele yetu, ambao ni Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mahakama ya Biashara.

Kwanza kabisa tumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* alioujaalia mchana huu kuwa katika hali ya uzima na afya inaruhusu.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuleta mswada huu katika kipindi muafaka. Vile vile niseme kwamba sheria hii ni muhimu sana kuwepo hapa Zanzibar kwani kutapunguza vitendo vya unyanyasaji wanavyofanyiwa baadhi ya wafanyabiashara wakubwa na wadogo hasa wajasiriamali, ambao shughuli zao ni za kubahatisha.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia katika visiwa vyetu vya Zanzibar wengi wanaishi kwa kufanya biashara na biashara zao watu wengi ni ndogo ndogo. Kwa mfano, pale Darajani ukizunguka upande wa pili wapo pale Kongo wanafanana sana, lakini ukiangalia hawa wafanyabiashara wadogo ni wengi sana kwa namna ya kutafuta riziki.

Kwa hivyo, ndipo pale niliposema ndani ya sheria hii wale watu tuwapangilie mipango mizuri, kwa sababu bila ya kuwapangilia mipango mizuri itakuwa hatujawatendea haki na hawa wenye mswada huu hata ukawajengea wapi lazima watarudi pale pale. Kwa mfano, pale Kongo wamejengewa katika upande wa Shaurimoyo soko zuri tu, lakini hawakai kwenye masoko yao na wanakuja zao pale Kongo na wanakuja na kufanya kama alivyozungumza Mhe. Asha Bakari Makame.

Lakini niseme hawa ni watu wa kuwapanga vizuri katika zile *section* zile wanazofanya biashara, kwa sababu hawa kuwafukuza ni kazi nzito sana. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu tumekusudia kufanya hii sheria, basi lazima tuwapangie mpango mzuri wa kuwafanya kuwa katika mpango mzuri na yule atakayekiuka taratibu za kukaa vizuri ndiye achukuliwe hatua, lakini hawa na wao ni binadamu kama binadamu mwengine wanatafuta mambo ya riziki kwa biashara ndogo ndogo hizi ambazo Mwenyezi Mungu alizowawezesha katika uwezo wao.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia katika mswada wenyewe mimi napata tabu sana kwenye sehemu hii ya pili kifungu cha 5(1) naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 5(1) kinaeleza hivi:-

> "Bila ya kujali sharti lolote la sheria hii Mahakama ya Biashara haitakuwa na mamlaka ya kipekee katika kutatua migogoro ya kibiashara".

Mhe. Naibu Spika, hapa imeelezwa kwamba Mahakama hiyo ya Biashara haitakuwa na mamlaka ya kipekee katika kutatua migogoro ya kibiashara. Lakini tukiangalia kifungu cha 5(2) pia naomba nikinukuu kidogo Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 5(2) kinaeleza hivi:-

> 5(2) "Mahakama ya Biashara itakuwa na mamlaka ya:
>
> (a) Kusikiliza na kuamua kesi zote za kibiashara kwa mujibu wa sheria hii".

Mhe. Naibu Spika, mimi napata tabu sana kwamba kule naambiwa itakuwa na mamlaka ya pekee, lakini huku itakuwa na utaratibu wa kuamua kesi yoyote kutokana na sheria hii. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, atufafanulie zaidi kwa ajili ya kupata uelewa.

Jambo jengine kwenye kifungu cha 14(1) na hapa naomba kunukuu kidogo Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 14(1) kinaeleza hivi:-

> “Mahakama inaweza, wakati wowote kabla ya kusikiliza kesi kuelekeza wadawa kuhudhuria katika mkutano wakaja kusikilizwa kesi kuhusiana na mambo yaliyojitokeza katika kesi au mwenendo”.

Mhe. Naibu Spika, huyu wadawa wametajwa sana humu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja hapa atueleze hawa wadawa na mimi sijui wadawa ni nani, lakini kwenye kila kipengele wapo hawa wadawa, kwa maana hiyo hapa tunahitaji maelezo ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, kama haitoshi na ingawa imezungumzwa na watu wengi katika kifungu cha 17(1) naomba nikinukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 17(1) kinaeleza:-

> “Kesi zote za biashara zitasikilizwa na kumalizika ndani ya miezi kumi tokea kuanza, lakini hazitozidi miezi kumi na mbili”.

Kwa kweli kifungu hiki nakiunga mkono sana na hata kingepunguzwa muda basi ingekuwa kheri na mafanikio mema kuliko huo muda wa mwaka mmoja, kwa sababu wafanyabiashara ni watu wanaofanya biashara na wengine wanadhulumiana vibaya sana. Lakini kuwepo kwa mahakama hii na kutoa uamuzi wa haraka basi kila mtu atajua haki yake ni ipi na kuweza kujiendeleza na biashara.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba huo muda wa miezi 10 mpaka mwaka mmoja, basi kama utapungua ni bora zaidi kiasi ndani ya miezi 6 iwe tayari yameshapatikana maamuzi kwa ushauri wangu.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 30 na Mhe. Salmin Awadh Salmin amekizungumzia sana, lakini na mimi nakiongezea nyama, ili kiwe na uzito zaidi, ambapo kinazungumzia lugha na naomba kunukuu kidogo Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 30 kinaeleza hivi:-

> “Lugha ya Mahakama itakuwa ama Kiswahili au Kiingereza, isipokuwa kwamba mienendo yote mahakamani itanakiliwa kwa Kiingereza”.

Mhe. Naibu Spika, si vibaya, lakini sisi Wazanzibari ni wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili sasa kama sheria hii itaandikwa kwa lugha ya Kiswahili basi itakuwa ni bora zaidi na watu wakapata uelewa.

Mhe. Naibu Spika, niseme mchango wangu si mkubwa ni huo. Vile vile napenda kumalizia kwamba elimu itolewe kwa wafanyabiashara, ili wajue kwamba jambo hili lipo kwa sababu sio wengi wanaofuatilia mijadala hii na kama kutakuwa kuna jambo fulani basi wengi hawatafahamu.

Kwa hivyo, ni vyema elimu itolewe kwa wafanyabiashara itolewe ni jambo muhimu sana na bila ya elimu basi hakuna mtu hata mmoja ambaye atafahamu kitu, lakini ikitolewa elimu itakuwa ni jambo la busara na watajua hivi sasa kuna kitu gani ambacho kimefanywa na kinatuongoza sisi wafanyabiashara.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nimshukuru sana na kumpongeza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa kutuletea mswada huu wa sheria ambao ni muhimu sana katika kipindi hichi tulichonacho na dunia ilivyo sasa.

Kwa hayo machache nasema ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi na wananchi wa Jimbo la Kojani naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia mswada huu ambao uko mbele yetu.

Vile vile nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa kutuletea mswada huu ambao ni muhimu unaolenga kwenye kuanzisha Mahakama ya Biashara.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli nchi hii inaendeshwa kwa misingi ya utawala bora na haki za binaadam kwa hivyo ni lazima iandae mikakati ile ile ya kisheria na sisi kama wananchi lazima twende kisheria, tutumie sheria ili tufanikiwe na mambo yetu mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye madhumuni ya mswada huu, niseme kwamba madhumuni yake ni mazuri sana na kwa sababu nimeona kwamba kufanya hivyo kuanzishwa kwa mahkama hii kutarahisisha mambo mbali mbali na vile vile kuondosha ule mrundikano wa kesi ambazo za mahkama kuu mambo yote kuyaweka pamoja.

Mhe. Naibu Spika, nishukuru sana kwa Mhe. Waziri kuanzisha mahkama hii kwa misingi ile ile, wenzangu wamesema hapa kutetea wafanyabiashara na hasa wafanyabiashara ndogo ndogo na niseme kwamba siku zote sheria ni msumeno unakwenda mbele na nyuma, na kwa hivyo nione kwamba wafanyabiashara sasa wanaamka kwa kuanzishwa kwa mahkama hii, wajue sheria na wao vile vile wazifuate kama ni mfanyabiashara basi afuate zile sheria za biashara ikiwa ni biashara ndogo ndogo kwa sababu kuna sheria ambazo zinamtaka kila mtu katika kila sehemu. Na leo Mhe. Waziri ametuletea mswada huu kwa sababu kutakuwa na mambo mbali mbali wewe kama mfanyabiashara basi unavyofanya biashara yako uwe katika sheria. Kuna biashara kama *smuggler*s wale wanaofanya biashara za magendo, kwa hivyo kwa upande na wao kama wanafanya magendo, kama magendo ni haramu basi atakapoifanya biashara yake ya haramu ajijue kwamba sheria itamkamata na anaweza akapoteza mali kwa kufanya biashara ile.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kwenye mswada huu sikuwa na mambo mengi ambayo nimetaka kuyachangia na kwa sababu wenzangu wengi wameshachangia lakini kuna vifungu ambavyo nilikuwa nimeviainisha, Mhe. Spika, nikienda na daftari la mahkama ni sehemu ya 3 ambayo inasema kutakuwa na daftari la mahkama linaweza kutunzwa daftari litakalojulikana kama daftari la kesi ya biashara kwenye mswada huu, kwa hivyo mimi nimpongeze tu Mhe. Waziri kwa kutuletea kifungu hicho ambacho kinaeleza kwamba kutakuwa kuna daftari maalum linalohusiana na kesi za biashara.

Mhe. Naibu Spika, nikienda na sehemu katika mswada huu kuna kifungu cha 21 kushindwa kuhudhuria kwa mdawa katika usuluhishi. Kwanza hili suala la mdawa kwa kweli ninamuomba Mhe. Waziri akija atufahamishe hili neno mdawa kwa kweli linanichanganya sijui maana yake tafsiri yake.

Lakini vile vile nikienda katika ukurasa 374 pembeni huku kuna usiri kama alivyosema Mheshimiwa mwenzangu aliyekaa Mhe. Bikame anasema Kiswahili kina maneno mengi na tafsiri ukiikosea basi unaweza ukaitafsiri vyengine. Ni sawa sawa na kusema kwamba hata ile *sound* utakayoitumia vile vile inaleta tafsiri tofauti tofuati aidha itakwambia kwamba umehamaki ama umekasirika au ulikuwa katika ile *sound* utakayoizungumza vile vile ikafanya kwamba umo katika furaha.

Kwa hivyo usiri mimi nikiitafsiri usiri nasema labda mtu katika dhohali, lakini hapa kuna usiri. Ninafikiri hapa ingekuwa siri labda nilivyosema mbele huko nimeona ni kitu ambacho kiko kwenye siri, lakini huku pembeni kuna usiri kwa hivyo usiri mimi nimetafsiri kwamba ni usiri kama kitu cha udhohali. Lugha ya mahkama ni kwamba itazungumzwa lugha ya Kiswahili au kingereza isipokuwa mienendo yote ya mahkama itanakiliwa kwa Kiingereza.

Halafu kuna ushahidi ambao utatolewa kwa njia ya video kifungu namba 2 ambacho kinasema endapo shahidi ameruhusiwa kutoa ushahidi chini ya masharti ya kifungu cha kwanza upande mwengine atapewa fursa ya kumhoji na kutumia njia hiyo hiyo. Hapa kidogo sijafahamu au kwa sababu sikusoma huku juu lakini hapo pia pananichanganya.

Vile vile nimeona kwamba kuna ushahidi kwa njia ya video, mimi nahisi ni sawa sawa kufanya hivyo lakini kuna ushahidi kwa njia nyengine hapa sijaiona kwenye *paper* hii lakini Mhe. Naibu Spika, ni kwamba mswada huu ni muhimu na kwa sababu umetenganisha mambo ya biashara kuwekwa katika mahkama ya peke yake, mimi nasema kutakuwa na ufanisi zaidi lakini kama nilivyoanza awali kwamba kuwe na ufuatwaji wa sheria kwa pande zote kwa wafanyabiashara sasa hivi wawe na muamko wa kujisajili au wa kufanya zile taratibu zote kama ni mfanyabiashara. Kwa sababu pia kama hawakujisajili wakajulikana kwamba wafanyabiashara wapo kihalali inaweza ikatokea kama hivyo ukaharibiwa mali yako au ukashtakiwa pengine au ukawa mtu umemkopesha lakini baadae ukakosa haki zako kutokana na kwamba hukufuata zile sheria.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono mswada huu mia kwa mia, na vile vile nawaomba Wawakilishi wenzangu mswada huu wauunge mkono. Ahsante.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunitaja nichangie na mimi kidogo nafikiri ulihisi kuwa ninayo mawazo naweza kutoa kidogo. Mhe. Naibu Spika, wenzangu wengi wametangulia kuchangia, na kwa hivyo wameshaanza kutangulia kusema maneno mengi ambayo pengine na mimi niliyaona niyaseme lakini hata hivyo nitajaribu kupembua yale ambayo hayakuelezwa kwa kina niweze kuyazungumza.

Kwanza kwa mawazo yangu au kwa maoni yangu mimi nahisi mswada huu una umuhimu mkubwa sana katika jamii yetu. Mhe. Naibu Spika, jamii yetu ya Zanzibar ni jamii ya wafanyabiashara wengi. Na katika biashara basi kuna mambo mengi yanafanyika, watu wanadhulumiana sana na biashara. Sasa serikali kufikiria mahkama *special* kwa biashara kwa kweli ni jambo la msingi sana. Lakini nilikuwa napata tabu kidogo kama alivyotangulia kusema mama yangu pale Bi. Asha Bakari kwamba biashara ina eneo pana sana, na nilipojaribu kuangalia kwenye kifungu cha tafsiri bahati mbaya neno biashara halikutafsiriwa iliyotafsiriwa ni kesi ya biashara, lakini biashara haikutolewa tafsiri.

Sasa wasiwasi wangu mimi unajua mambo mengi ya kibiashara kwa mfano hata nyumba ni biashara lakini kuna biashara ya bidhaa mbali, kuna biashara ya huduma, kuna biashara ya uvuvi, kuna biashara ya ufundi, kuna biashara ya dala dala. Biashara ni nyingi sana sasa kwa kuwa tafsiri ya biashara iliyoainishwa kuwa itashughulikiwa na sheria hii haikuainishwa napata wasiwasi kidogo kwamba kuna mambo yatafanyika ambayo ukiyatizama ni mambo ya kibiashara, lakini ukiangalia *nature* ile kesi yake inaingia moja kwa moja kwenye kesi ya madai ambayo inaongozwa na sheria nyengine na sio hii. Au mara nyengine inaweza ikajikuta ile *nature* ile kesi ilivyotokea pengine ni kesi ya jinai kabisa, ambayo pia inaongozwa na sheria nyengine siyo hii. Sasa kutotoa tafsiri ya neno biashara nahisi huko mbele inaweza kupelekea ugumu wa kuweza kutoa tafsiri kwamba eneo hili ni la kibiashara kweli au ni la madai au ni la jinai au vyenginevyo.

Sasa nilikuwa nahisi kungekuwa na umuhimu kwanza kutafsiri hiyo biashara yenyewe iliyokusudiwa ambayo itashughulikiwa na mahkama hii ni biashara za aina gani. Maana yake biashara kama tunavyosema ina wigo mpana sana.

Halafu jambo jengine Mhe. Naibu Spika, unajua ukisoma huu mswada utakutia kama una *stage* 2 au 3, maana yake hatuendi kwenye kesi moja kwa moja unaweza ukakutia mara nyengine kuna kifungu hapa kinaeleza kuna mkutano sijui kifungu cha ngapi kile cha 14 kuna mkutano kabla ya kusikilizwa kesi. Na ukisoma sehemu ya tano nzima ni ya usuluhishi. Sasa ukiisoma ile sehemu ya tano unaweza ukafikiria labda hiyo kazi ya mahkama yenyewe itakuwa ni hii ya usuluhishi maana yake imeeleza mambo mengi ya usuluhishi mpaka mimi nikafika pahali nikadhania kama huyu Jaji ndio huyu anayeitwa msuluhishi. Lakini nilipofanya mazungumzo na wenzangu wakaniambia hapana. Huyu msuluhishi atateuliwa na huyo Jaji pengine. Yaani huyu msuluhishi ni mtu mbali na huyu Jaji atakayesikiliza kesi ni mtu mbali.

Lakini mimi nimepata wasiwasi kidogo Mhe. Naibu Spika, kuweka hii sehemu ya tano ya usuluhishi maana usuluhishi una mambo yake, mimi ninapopeleka dai langu mahkamani nimefanya ubia na mfanyabiashara mmoja kanidhulumu, maana nataka nipate haki yangu yote, lakini ukishanipeleka kwenye usuluhishi kuna moja katika mawili yatatokea. Ili usuluhishi uwe basi inabidi lazima mimi ni-*release* baadhi ya haki zangu, jambo ambalo sio nia yangu ya kwenda mahkmani. Yaani ikiwa ni hivyo ingekuwa hakuna haja ya kwenda mahkamani ningemsamehe tu. Lakini nakwenda mahkamani kwa ajili ya kupata haki. Lakini ukiniambia kwanza tukae kwenye kikao cha usuluhishi, maana yake mimi haki zangu nyengine ili usuluhishi uwe basi lazima nizisamehe.

Sasa nahisi sawa kifungu cha usuluhishi kinaweza kikapoteza gharama za kesi, ikapunguza gharama za kesi, kikapunguza muda wa kesi, lakini hatimae pia kitapunguza haki ya mtu aliyokusudia mwenyewe kuidai. Sasa sijui Mhe. Waziri atatusaidia vipi au ataweza kutuhakikishia vipi kwamba ndani ya sehemu hii ya tano mtu atakuwa hapotezi haki zake kwa usuluhushi. Ingawa ana hiari ya kuukubali au kuukataa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, labda nije hapa kwenye kifungu cha 5, Kifungu cha 5 ukikisoma ni mamlaka ya mahkama. Kinasema bila ya kujali sharti lolote la sheria hii Mahkama ya Biashara haitakuwa na mamlaka ya pekee katika kutatua migogoro ya kibiashara.

Halafu ukija kifungu cha 2(a) yaani hapa kifungu cha 5(2) kinataja Mahkama ya Biashara itakuwa na mamlaka ya kusikiliza na kuamua kesi zote za kibiashara kwa mujibu wa sheria hii. Lakini hapa kifungu cha kwanza kinasema hakitakuwa na mamlaka ya pekee katika kutatua migogoro. Sasa nilikuwa nataka nipate ufumbuzi kidogo hapa.

Kifungu cha 5(1) kinasema mahkama hii haitakuwa na mamlaka ya pekee ya kutatua migogoro lakini ukisoma kifungu cha pili sasa hayo mamlaka yanakuja pale ya kusikiliza na kuamua kesi, sasa sijui inakuaje kusema hakutakuwa na mamlaka ya kipekee maana yake kutakuwa na chombo chengine kitakachosaidiana na mahkama hii au vipi, naona kama kuna *contradiction* kidogo ya maelezo hapa nilikuwa naomba Mhe. Waziri hapa aje atusaidie ufafanuzi kidogo.

Lakini ukisoma kifungu cha 5 hicho hicho 2(c) kinasema kwamba mahkama hiyo itakuwa na uwezo au itakuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi za rufaa au kusikiliza rufaa au marudio na kuwa mahkama ya marejeo ya migogoro ya kibiashara. Hapa nimezidi kuingia kwenye matata sasa kwa sababu nilivyozoea mimi nikienda katika mahkama ya mkoa mfano nikapeleka shauri langu kama sikuridhika maana yake nina-*appeal* Mahkama Kuu haitakuwa mahkama ile ile ya Mkoa nilipoanzia shauri langu ndio itakuwa mahkama ya rufaa, lakini na-*appeal* Mahkama Kuu ili nipate haki yangu. Yaani mahkama ile sikuridhika na uamuzi wake. Lakini hapa mahkama hiyo hiyo inayosikiliza shauri halafu inageuka, mahkama hiyo hiyo inakuwa ni mahkama ya kusikiliza rufaa. Hapa tupeni ufafanuzi kidogo nahisi pana mashaka kidogo kwa sababu mtu atakuwa na imani gani kwamba hakuridhika na uamuzi wa mahkama hiyo lakini aliposema haridhiki mahkama ile inageuka hasa kwa mahkama ya rufaa ile ile au utaratibu ukoje. Naomba Mhe. Waziri akija anisaidie ufafanuzi

Mhe. Naibu Spika, halafu niende kwenye kifungu cha 17, kifungu cha 17 kinasema kesi zote za biashara zitasikilizwa na kumalizika ndani ya miezi 10 tokea kuanza lakini hazitozidi miezi 12. Hiki kifungu Mhe. Naibu Spika, kimenifurahisha sana na nilikuwa naomba hasa tufanye marekebisho na hata katika kesi za jinai, kesi za madai, tuweke kifungu cha namna hii. Kwa sababu kuna mtindo sasa hivi mahkamani na mtindo huu unachezwa na wale wadau wote wa ile kesi. Siku nyengine Jaji anaweza akahusika au hakimu lakini wakili upande wa utetezi akahusika na wakili upande wa mdai akahusika, wanacheza dana dana katika kuzichelewesha kesi mpaka zinaweza zikafika kesi ya madai miaka 5 haijapata ufumbuzi. Wanapanga leo Wakili wa mdai asije mahkamani na huku keshaambiwa Jaji ikiwa wakili hakuna wewe akhirisha kesi miezi 2. Mara ya pili anapanga Jaji na yeye ana dharura hatasikiliza kesi. Kwa hivyo inapigwa dana dana wee kesi haimaliziki. Kuna kesi maalum zinakuwa hazimaliziki katika nchi yetu.

Sasa nasema kifungu hiki kimenifurahisha kwa sababu kimembana Jaji au kimeibana ile mahkama ndani ya mwaka mmoja lazima kesi iwe imemalizika. Sasa hii *wallahi* nashauri mimi na katika mahkama nyengine hata zetu za kawaida kuwe na kifungu kama hiki. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kadiri muda unavyokwenda ndani ya kesi ndio unavyozidi kupoteza haki za watu. Sasa ni muhimu kwa kila kesi kwa kweli ipangiwe muda na imalizike.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wenzangu wametangulia kusema maneno mengi na mswada huu kama nilivyotangulia kusema ni mswada muhimu sana kwa kuwa ndio mazingira yetu yalivyo ni mazingira ya kibiashara, na kwa hivyo lazima tuwe na utatuzi wa migogoro ya kibiashara ambao ufumbuzi wake utapatikana katika mswada huu.

Mimi nadhani sina mengi ya kusema huu mswada nauunga mkono lakini baada ya kupata ufafanuzi wa haya masuala machache ambayo nimeyaeleza. Ahsante.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii kuchangia kidogo huu mswada kwa vile watu wengi wameshauchangia na mimi naomba nichangie vifungu vitatu hivi nilivyoviona humu.

Ahsante Mhe. Naibu Spika, mimi nikija katika ukura wa 365 kifungu kinachosema rafiki wa mahkama maana yake ni mtu aliyeitwa na mahkama ili kuisaidia kuhusiana na shauri liliopo mbele ya mahkama. Hii Mhe. Spika, niseme kwamba mtu huyo aliyeitwa mahkamani kuisaidia kuhusiana kwa suala liliopo mbele ya mahkama niseme kwamba Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ahakikishe kwamba kuwa huyu mtu ni mkweli na ni muaminifu wa kuisaidia mahkama hiyo, isije kuwa Mhe. Naibu Spika, kuwa mtu huyu ana chuki binafsi ambazo zitakazokwenda kumtosa mwenzake pale katika mahkama hiyo.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, nije katika kifungu cha 366 sehemu ya 2 inayosema kwamba kuanzishwa Mahkama ya Biashara ambayo itakuwa ni Divesheni ya Mahakama Kuu ya Zanzibar kushughulikia migogoro ya kibiashara ya

kiwango kilichoelezwa na sheria hii. Hii Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba hii mahkama inayoanzishwa iangalie kosa la kibiashara lenyewe isije kuwa ni kosa dogo dogo tu ambalo la watu kusikilizana wenyewe mitaani ikawa ni kosa ambalo linapelekwa mahkamani. Liangaliwe kosa lenyewe ni la kweli na hilo kosa lisijekuwa la kubambikizwa, mahkama iwe makini Mhe. Naibu Spika, hasa katika hizi kesi za biashara.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nije katika ukurasa wa 367 kifungu cha 6 inayosema kwamba mahkama inaweza kumuita mtu yoyote kama ni rafiki wa mahkama hii. Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba mahkama inaweza kumuita mtu yoyote, hii Mhe. Naibu Spika, kidogo inanipa matatizo huyu mtu yoyote kuna watu wengine wana akili timamu, kuna watu wengine ni wendawazi. Sasa hii mahkama iangalie huyu mtu wa kumuita yeyote yukoje ili kuisaidia hiyo mahkama yenyewe. Ahsante Mhe. Spika, ninakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza ninawashukuru waliopata nafasi ya kuchangia na katika orodha yangu wamemalizika wachangiaji, kwa hivyo naona niakhirishe kikao hiki tumpe muda Mhe. Waziri akajiandae ili jioni aje afanye majumuisho na kupitisha vifungu.

(Saa 6.50 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)
(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe tumepata majina ya wachangiaji watatu, kwa hivyo yupo Mwanasheria atachukua *minutes* kwa niaba ya waziri na mchangiaji wa mwanzo ni Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu na pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kutoa mchango wangu mfupi juu ya mswada huu muhimu wa Mahkama ya Biashara.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu muhimu unafuatia ule mswada wa jana ambao tumeufanyia marekebisho wa kuanzisha Divisheni ya Mahkama Kuu na hii ni sehemu ya Mahkama Kuu. Kwa hivyo sababu ambazo zimependekezwa na Mhe. Waziri katika mswada huu ni sababu ambazo zinatilika akilini, ni sababu za msingi na mimi naunga mkono sababu zote ambazo Mhe. Waziri ametueleza kwa madhumuni ya mswada huu.

Sasa nikianza kuchangia mswada wenyewe nianze moja kwa moja na kifungu cha 5 naomba ninukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 5(1) kinasema kwamba:

> "Bila ya kujali sharti lolote kwa sheria hii, Mahkama ya biashara haitakuwa na mamlaka ya kipekee katika kutatua migogoro ya kibiashara".

Sasa naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu au Waziri aje anitolee ufafanuzi hili neno "haitakuwa", ambapo Mahkama hii haitakuwa na mamlaka pekee katika utatuzi wa migogoro ya kibiashara. Kwa nini na wakati hii ni sehemu ya Mahkama Kuu ni divisheni ya Mahkama Kuu lakini kifungu kinasema kuwa haitakuwa na mamlaka pekee ya kutatua migogoro ya kibiashara. Kaw hivyo, naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu labda anielimishe kwa nini isiwe na mamlaka ya kutatua migogoro ya biashara wakati hii ni sehemu ya Mahkama Kuu.

Lakini sehemu hiyo hiyo kifungu cha 5(2) (c) hiki naomba ufafanuzi kwamba kusikiliza rufaa marudio na kuwa Mahkama ya Marejeo kwa migogoro ya biashara. Kifungu cha 5(1) kinasema haitakuwa na mamlaka pekee lakini kifungu cha 5(2)(c) Mahkama itakuwa na uwezo wa kusikiliza rufaa, marudio na kuwa Mahkama ya marejeo kwa migogoro ya kibiashara. Sasa naomba nipate ufafanuzi, hii haitakuwa na mamlaka pekee sawa, lakini huku chini itakuwa ni Mahkama ya marudio hivyo naomba ufafanuzi wa kisheria ili niweze kuridhika kabisa katika kifungu hiki.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 7(1) kuna kamati ya watumiaji wa Mahkama ya Biashara, hapa kutakuwa na kamati ya watumiaji wa biashara ambayo itajumuisha Majaji wa Mahkama ya Biashara, wakili mmoja atateuliwa na Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar, Wakili wa Serikali atateuliwa na Mwanasheria Mkuu, mtu mmoja atakayeteuliwa

na Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye viwanda na wakulima wa Zanzibar na mwakilishi mmoja kutoka kwenye wizara inayohusiana na biashara.

Mhe. Naibu Spika, kamati ya watumiaji ni jambo zuri lakini naomba nipate ufafanuzi kwamba kamati hii itakuwa na majaji wa Mahkama ya Biashara ni wangapi mswada haukusema kama wawili, watatu au mia. Sasa naomba ufafanuzi ni majaji wangapi wataokuwa kwenye kamati hii ya watumiaji wa Mahkama ya Biashara.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, ninavyoona kwa maoni yangu ni kwamba wajumbe wa kamati hii ya watumiaji wengi ni wawakilishi wa serikali na wawakilishi wa sekta binafsi kwa maana ya wananchi wa kawaida ni mjumbe mmoja tu atakayeteuliwa na Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye viwanda na wakulima ndiye ambaye anahusika kuwakilisha wananchi wa kawaida. Sasa kwa mtazamo wangu kuwa kamati hii imebeba wafanyakazi wa serikali wengi na kwa hivyo wananchi wa kawaida watakuwa hawana uwakilishi ipasavyo. Mimi binafsi itanitia mashaka kuona kwamba kamati yenyewe ya watumiaji hii ndio itakayobeba mashauri ya Mahkama hii ya Biashara itakuwa zaidi imewakilisha serikali kuliko wananchi wa kawaida na wananchi ndio wafanyabiashara. Serikali imejitia kwenye wananchi wafanyabiashara lakini wawakilishi wao ambao wanawawakilisha ndani ya kamati hii ni wachache mno. Kwa hivyo, hii inatia mashaka kwamba wananchi hawatatendewa haki ikiwa kamati yenyewe wengi ni watendaji wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine kifungu cha 7(3) kinasema kwamba:

> "Itakuwa ni jukumu la Kamati ya watumiaji wa Mahkama ya Biashara kuishauri Mahkama ya Biashara kuhusu mambo ya utendaji ya Mahkama na kuwasilisha orodha ya watu wenye uelewa wa mambo ya biashara kufanya kazi kama washauri".

Mhe. Naibu Spika, ikiwa kamati yenyewe itakuwa na majaji wafanyakazi wa serikali zaidi kuliko wananchi na wao ndio ambao watateuwa ile kamati ya ushauri ni dhahiri kwamba wananchi wafanyabiashara wa kawaida hawatafanyiwa haki. Kwa hivyo, ningependekeza kwamba kamati hii ya watumiaji iwe ni nusu kwa nusu, iwe na majaji na wataalamu kutoka serikalini lakini iwe na wawakilishi sawa wananchi ili mashauri yale ambayo yatakwenda kibiashara basi yazingatiwe kwa upeo huo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ni kifungu cha 9(1), Mahkama inaweza kukaa katika wasaa na mahala kama shughuli za Mahkama inavyoweza (a) kuhitaji au kama Jaji Mkuu anavyoweza kuamua muda baada ya muda. Ningetaka kujua je, katika Mahkama zetu hizi za Zanzibar hakuna kalenda maalum ya Mahkama kwamba itafanya kazi kwa utaratibu huu na huu. Kwa sababu hapa ikiwa Mahkama itakaa katika vikao vyake kama Jaji Mkuu atakavyoona inafaa nadhani itakuwa ule utaratibu wa kuendesha kesi bado utakuwa na urasimu, ingawa huku chini kuna kifungu kimesema kwamba kesi hizi hazitazidi miezi 12, lakini kwa nini tulazimishe hivyo, kama kesi inaweza kuamuliwa ndani ya wiki moja kwa nini tupeleke miezi 12.

Kwa hivyo, nadhani kifungu hiki cha 9(1) kirekebishwe kisiwe kwamba kama Jaji Mkuu atakavyoona inafaa, tuzingatie kwamba muda wa kesi hiyo basi usizidi miezi fulani na tusimuachie jaji tu kwamba aamue vile anavyoona. Hili ndilo ambalo linasababisha hivi leo kuna kesi zina miezi mitatu, miaka mine, mitano, jambo ambalo tumeliachia mwanya. Sasa nadhani tuweke muda maalum wa kumaliza kesi ili tusiwape majaji kuamua vile wanavyoona inafaa.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 9(3) wakati shauri litakapofungwa mbele ya Mahkama jaji anayeongoza atataka na kunakili maoni ya kila mshauri waliokuwepo katika ufungaji wa shauri hilo. Lakini kifungu cha 9(4) jaji anayeongoza hatafungika na maoni ya washauri ila pale atakapotofautiana na maoni ya mshauri yeyote kati yao jaji atarikodi maoni ya mshauri huyo na sababu ya kutofautiana naye.

Kifungu cha 9(5) kinasema kwamba, "hakuna shauri litakalokuwa batili kwa sababu pekee ya kukiuka taratibu katika uchaguzi wa uteuzi wa mashauri hayo". Mhe. Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba kwa nini tumuwekee jaji washauri wakati yeye hafungiki na ushauri wowote, kwa nini tusiachie jaji akaamua kulingana na maelekezo ya sheria na kujengana na utaratibu wa kimahkama. Wasi wasi wangu ni kwamba tunaweka washauri kwa ajili ya kuongeza gharama za uendeshaji wa mahkama, hakuna haja ya washauri nadhani jaji kwa sababu amewekwa pale kwa misingi ya sheria anatosha kufanya maamuzi kwa kulingana na utaratibu wa kisheria na si vyema kuwekewa washauri ili kuongeza gharama za uendeshaji wa kesi.

Mahkama inaweza kumwita mto yeyote kama rafiki wa mahkama nadhani hiki kifungu cha 9(6) kingetosha kumuachia jaji akamwita rafiki wa mahkama pale atakapoona inafaa na hili ndio jambo ambalo lingewafanya hao washauri wa mahkama wakawasili katika kesi mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, lakini naona kifungu chengine kwamba Mahkama hii itashughulikia kesi ambazo mtaji wake ni kuanzia shilingi 30 milioni. Sasa mimi napendekeza kwamba tuangalie Wazanzibari, Wazanzibari wengi wanafanya biashara wakiwa na mtaji mdogo, sasa kuamua kwamba shilingi 30 milioni ndio kiwe kianzio cha kufungua kesi ni kusema kwamba wale wenye mtaji mdogo kama shilingi milini tano, kumi, kumi na tano mpaka ishirini watakuwa hatuwafanyii haki. Sasa mimi napendekeza kwamba Mahkama hii ianze kusikiliza kesi kuanzia mtaji wa shilingi milioni kumi badala ya milioni thalathini ambazo zimependekezwa. Wazanzibari wengi ambao ni wananchi wetu hawana uwezo huo mitaji yao ya fedha ni kidogo sana kwa hivyo shilingi milioni thalathini itakuwa inawalinda wale tu wenye uwezo mkubwa na hivyo Wazanzibari wengi wenye uwezo mdogo itakuwa hatuwafanyii haki.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine kifungu cha 10(2) (b) mashauri ambayo hakuna uwezekano wa dai lolote la msingi la matukio isipokuwa kama mdai katika mwenendo huo anakusudia kuwaomba hukumu chini ya amri ya 16 ya Sheria ya Mwenendo wa Madai au kwa sababu nyengine yoyote anaona mwenendo huo ni muwafaka zaidi kufunguliwa kwa hati ya madai. Mhe. Naibu Spika nadhani hapa ni jambo zuri lakini tuwe makini sana katika kusimamia utaratibu huu.

Kifungu cha 11 Daftari la Kesi. Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki kinasema kwamba, “Mahkama itawezesha kutunza daftari likajulikana kama Daftari la Kesi za Biashara, ambalo maelezo kuhusiana na kesi kama inavyoweza kupelekwa na Mrajis kwa ajili ya kufunguliwa kitaingizwa”. Mimi kwa ajili yangu hapa ni kwamba ziko taasisi kwa kutumia ule msingi wa rushwa basi hupoteza kumbukumbu muhimu, unaweza kuambiwa ofisi imeingia moto, panya wamekula kumbukumbu au yamenyeshewa na mvua.

Kwa hivyo, tujaribu ku-*deal* na wafanyabiashara wenye uwezo, hivyo ofisi hii ya mrajis huyu lazima iwe makini isije ikapotezsa kumbukumbu kwa sababu ya mkono wa fedha; lazima tuweke watu wenye uwezo, walio makini na wanaojali kazi yao kwa maslahi ya wananchi ili kuwaacha wale wafanyabiashara wajanja wachache kuja kutumia ofisi hii kupoteza kumbukumbu kwa maslahi yao binafsi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nadhani Mwanasheria Mkuu hapa ahakikishe kwamba anatuwekea Mrajis mwenye uwezo na utashi wa kufanya kazi yake kwa madhumuni ya kujenga nchi yetu na kutoa haki kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ni kifungu cha 17(1), Kesi zote za kibiashara zitasikilizwa na kumalizika ndani ya miezi kumi tukea kuanza lakini hazitozidi miezi kumi na mbili. Hili nimelisema mwanzo kwamba si lazima tuweke miezi kumi, kama kesi inaweza kumalizika ndani ya siku tatu tumalize siku tatu, kama inaweza kumalizika ndani ya mwezi mmoja basi tumalize mwezi mmoja ili kupunguza mkusanyiko wa kesi nyingi na kupunguza gharama za utumiaji wa kesi kwa upande wa Mahkama. Jambo hili Mhe. Naibu Spika, limekuwa likisababisha matumizi makubwa ya fedha za umma kwa kurundika kesi bila ya kuwa na sababu za msingi.

Mhe. Naibu Spika, kimsingi mswada wenyewe mimi naunga mkono lakini ninachotoa tahadhani ni kwamba, tuzingatie wafanyabiashara wetu wadogo, tuwalinde wafanyabiashara wadogo hawa ndio wanaodhulumiwa, tajiri mwenye fedha zake si rahisi kudhulumiwa, anakuwa mjanja na anakuwa na uwezo mkubwa. Kwa hivyo, hawa wenye kipato kidogo ndio hasa wangepaswa kulinda na sheria hii kwa ajili ya kusaidiwa maslahi yao.

Vile vile tungewashauri zaidi wafanyabiashara wadogo wadogo kwamba wanapojiingiza katika mikopo na mabenki basi nadhani mswada huu ungewawekea masharti mazuri ili wasiingize mikopo ambayo hatimae inawafilisi nyumba zao na mali zao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo mdogo mimi naunga mkono mswada huu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii jioni ya leo niweze kutoa mawili matatu au mchango wangu juu ya mswada huu wa sheria ya Kuanzishwa Mahkama ya Biasara Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuandalia mswada huu. Mswada huu kwa kweli ni muhimu sana kwa sababu kulikuwa kuna kilio kikubwa sana cha

wafanyabiashara namna wanavyopata tabu katika kupata suluhu au haki zao inapotokea migogoro au migongano sehemu za biashara. Kwani kama unavyojua wanapokwenda kwenye Mahkama hizi za kawaida huwa inawachukua muda mwingi sana katika kupata suluhu ya yale matatizo waliokuwanayo. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Naibu Spika, mswada huu ukishapita na kuwa sheria utasaidia sana kwa wafanyabiashara wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa kweli kwenye mswada huu sina mengi sana ya kuchangia nina mawili matatu tu ambayo nimeyaona kama na mimi nitoe mchango wangu kwenye maeneo hayo.
Mhe. Naibu Spika, mimi nianze mchango wangu kwenye kifungu cha 5 kwenye Mamlaka ya Mahkama, panaposema bila ya kujali sharti lolote la sheria hii Mahkama ya Biashara haitakuwa na mamlaka ya kipekee katika kutatua migogoro ya kibiashara. Mahkama ya Biashara itakuwa na mamlaka ya kusikiliza na kuamua kesi zote za kibiashara kwa mujibu wa sheria hii. Sasa hapa kidogo nilikuwa nataka ufafanuzi Mhe. Waziri atapokuja hapa anisaidia katika zile biashara zitakazokuwa zinakwenda kwenye Mahkama hii, kwa sababu biashara ziko za aina nyingi sana, ingawa huku wameonesha kiwango cha biashara kuanzia kiasi gani mpaka kiasi gani. Lakini kuna biashara nyengine zinaitwa haramu kabisa nao pia wanapokuwa wameingia kwenye migogoro watakwenda kwenye Mahkama hii? Kwa sababu biashara zenyewe zinakuwa haramu. Sasa nataka kujua kwamba hawa nao pia watakwenda au wataruhsika kwenye Mahkama hizi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nisogee kwenye kifungu hicho hicho cha 5 lakini kwenye aya ya tatu inayozungumzia Mamlaka ya Mahkama ya Biashara inaweza kutumiwa kwa malalamiko ya biashara ambayo yanazidi shilingi 30 milioni, pale ambapo jambo lililobainishiwa ni mali inayoondosheka na mali isiyoondosheka inayozidi shilingi 20 milioni.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi hapa nilikuwa na wazo kidogo kwa sababu nikiangalia hiki kiwango ambacho kimewekwa nahisi ni kikubwa kutokana na wafanyabiashara wetu, mana hapa tutakuwa tumewagawa katika tabaka kubwa sana. Tunao wafanyabiashara sisi hawafiki kiwango hiki, sasa nilikuwa nashauri tupunguze kidogo ile kuwa malalamiko ya biashara ambayo yanazidi shilingi 30 milioni pale ambapo jambo linalobishaniwa ni mali ya inayoondosheka.

Mimi nilikuwa naomba hapa tupunguze kidogo, kutoka 30 milioni tuweke 20 milioni kwa mali inayoondosheka na ile mali isiyokamatika inayozidi shilingi 20 milioni tupunguze tuweke milioni kumi, ili kufanya kwamba wale ambao watakuwa na malalamiko wengi na pengine mtu ana biashara yake ambayo haifiki kiwango kile basi tukikipunguza hiki kiwango tutapata kwamba hii Mahkama itakwua inaweza kufanya kazi zake vizuri zaidi kwa sababu wafanyabiashara wetu wengi si wenye uwezo kiasi hicho. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri aliangalie tuweze kupunguza hii *amount* kutoka ile ya 30 tukaweka 20 na 20 tukaweka 10.

Mhe. Naibu Spika, nikisogea mbele niende kwenye kifungu nambari 7 Muundo wa Mahkama. Mchangiaji mwenzangu aliyepita alilizungumza hili mimi nimekuwa kidogo nina jambo hapa nishauri, kwenye huu muundo nataka niangalie kwenye ile Kamati ya Watumiaji wa Mahkama ya Biashara. Kutakuwa na Kamati ya Watumiaji wa Mahkama ya Biashara ambayo itajumuisha Majaji wa Mahkama ya Biashara. Hapa wamezungumzwa majaji lakini ile idadi haikuwa imeoneshwa kama walivyooneshwa hawa wengine, ambapo kama huku wakili mmoja anayeteuliwa na Jumuia ya Wanasheria wa Zanzibar, Wakili sa Serikali anayeteuliwa na Mwanasheria Mkuu. Sasa na hapa nilikuwa nataka tuone wale majaji nao watakuwa wangapi katika mahkama hii, kwa sababu tukiangalia huko mbele tutakuta namna ambavyo zimepangwa zile kesi zitakavyokuwa zinakwenda na muda wa kumaliza kesi hizo. Sasa tuone ule umuhimu wa kuwa na majaji wengi kiasi gani wa kuweza kumaliza zile kesi ndani ya ule wakati ambao umepangwa.

Nikiendelea hapa kifungu hiki hiki cha 7 kwenye 7(2) kinazungumza kuwa Jaji dhamana wa Mahkama ya Biashara atakuwa Mwenyekiti na Mrajis atakuwa Katibu wa Kamati, mimi nataka kujua huyu Mrajis ni yupi, kuna Mrajis Mahkama Kuu sasa sijui yule ndiye ataekuwa Katibu katikahii kamati au mrajis yupi. Kwa hivyo, nilikuwa nataka ufafanuzi hapa kumjua yule mrajis wa Mahkama hii atakuwa anatokea upande upi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele niende kwenye kifungu cha 12 kupangiwa kwa kesi. Kifungu kinazungumzia kwamba Jaji dhamana wa Mahkama au jaji mwengine yeyote atakaekasimu uwezo huo isipokuwa kama mazingira hayaruhusu ambapo atanakili hivyo ndani ya siku zisizozidi tano za kazi baada ya kufunguliwa kesi atawezesha kesi hiyo kupangiwa jaji maalum kwa njia ya kawaida au kwa njia ya kieletroniki. Sasa hapa pamezungumziwa kama mazingira hayaruhusu, mimi kidogo hapa nimepata shaka kwa sababu haya mazingira yenyewe hayakuelezwa yepi,

nafikiri ni vyema kama tutafafanuliwa vizuri aina au mazingira yenyewe yaweje ili yaweze kukasimiwa. Kwa sababu hofu yangu isije ikachukuliwa hii ikawa tena kila kinachokwenda kinaonekana ndio mazingira hayaruhusu kwa hivyo yakawa yanakwenda hivyo.

Lakini jambo jengine Mhe. Naibu Spika, hasa kwenye hii sehemu ya nne kupanga kesi kabla ya kusikilizwa na mkutano, kuna maneno yametumika kidogo mimi nilikuwa nataka nipate ufafanuzi hapa, sijui kama ndio Kiswahili changu tu cha Mkwajuni nakuwa sifahamu vizuri. Ukiangalia humu mna 'wadawa', 'mdawa' saas kidogo hili neno nataka ufafanuzi ni wadawa/wadaiwa au mdai/mdaiwa. Kwa mfano, hiki kipengele nambari 14 mkutano wa kabla ya kusikiliza kesi anasema "Mahkama inaweza wakati wowote kabla ya kusikiliza kesi kuelekeza wadawa kuhudhuria katika mkutano wa kabla ya kusikilizwa kesi kuhusiana na mambo yaliyojitokeza katika kesi au mwenendo. Sasa wadawa maana yake ni wadau wa ile kesi au vipi, hapa pamejitokeza vitu kama hivi katika maeneo mengi sana ndio maana nikasema niombe nipate ufafanuzi au tafsiri ya maneno haya ambayo yametumika hapa yachanganuliwe katika Kiswahili sanifu zaidi.
Jengine niende katika uharakishaji wa kesi kifungu nambari 17 sehemu ya nne. Kifungu kinasema "kesi zote zitasikilizwa na kumalizika ndani ya miezi kumi tokea kuanza, lakini hazitozidi miezi kumi na mbili, isipokuwa kwamba: (a) kuna uwezekano wa kuongeza muda huo mdawa atafanya ombi Mahkamani siku thalathini kabla ya kumalizika miezi kumi na mbili na Mahkama inaweza kuongeza muda huo kwa kuzingatia ugumu wa kesi hiyo".

Sasa mimi hapa Mhe. Naibu Spika nimepata shaka, kwa sababu mdawa huyu yeye ndo kapeleka kesi hii kesi ndio inaendeshwa na Mahkama kule, Mahkama ndio inayojipangia muda wa kumaliza kuhakikisha kuwa shauri lile litakuwa limemalizika ndani ya miezi kumi au kumi na mbili, sasa unamwambia mdai yeye mwenye ile kesi atapoona kesi ile haikamiliki pale ndio apeleke maombi ya kwamba ile kesi sasa iendelee zaidi ya kipindi kile, kidogo mimi naona kama iko kinyumenyume. Maana yeye kapeleka ile kesi wenye kumaliza nyinyi mnaopanga kwamba tutaisikiliza tena baada ya wiki au wiki mbili, sasa hii inawezekana ikawa kesi zote zikawa zinafanyiwa maombi.

Mhe. Naibu spika, kwa sababu haya maombi nayo yanahitaji kulipiwa kama nimeona vizuri kule mbele yanalipiwa, sasa naona kama itakuwa biashara hii, kwamba kila kesi itakuwa haimaliziki katika ule wakati uliopangwa wa miezi kumi au kumi na mbili sasa itakuwa kesi zote hizi zitavuka muda ule na mimi kama ndio mwenye ile kesi natakiwa kupeleka maombi na nikipeleka maombi inabidi lazima nifanye malipo.

Sasa hapa nimepata shaka kidogo hebu Mhe. Waziri atapokuja hapa anisaidie kunitoa huu wasi wasi wangu, huu utaratibu wake utakuwakuwaje. Kwa sababu anayedai ndiye atakayeleta malalamiko pale huko kufungua hiyo kesi yenyewe kulipa na inapokuwa niongezewe muda nilipe, lakini mtendaji wenyewe mimi sina mamlaka ya kumwambia maliza kesi, sasa ile miezi iliyowekwa kumi mpaka kumi na mbili haikwisha yeye ndiye anayefanya vile halafu mimi niombe na nilipe. Hii kidogo mimi nahisi sio sawa, lakini atapokuja Mhe. Waziri ufafanuzi wake labda utatusaidia ili kuweza kujua zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele nasogea mpaka kwenye ukurasa wa 375 kifungu cha 30, kifungu hiki kinseama, "Lugha ya Mahkama itakuwa ama Kiswahili au Kiingereza, isipokuwa kama mienendo yote ya Mahkamani itanakiliwa kwa Kiingereza". Mimi nataka hapa Mhe. Waziri abadilishe lugha ya Mahkama atwambie itakuwa Kiswahili au Kiingereza, mana hiki Kiingereza iwe tena kama ndio Kiswahili kimeshindikana basi ndio tunachukua hicho Kiingereza, lakini kwa lugha aliyotumia hapa kaianza kwa ama Kiswahili maana yake ni kuwa kuna lugha nyengine au vipi.
Kwa hivyo, nilikuwa nataka ufafanuzi kidogo hapa atusaidie ama hili neno 'ama' aliondoshe ibakie 'itakuwa Kiswahili au Kiingereza; maana yake ni vitu viwili tu tunachagua mbadala wake kama haikuwezekana Kiswahili basi twende kwenye Kiingereza. Lakini ikianza na ama maana yake kuna kitu chengine huku nyuma kinatufuata au vipi, nilikuwa nataka hili tusaidiwe kupatiwa ufafanuzi atapokuja Mhe. Waziri kufanya majumuisho yake.
Mhe. Naibu Spika, mimi naendelea tena mbele kutoka hapo kifungu cha 30 naingia kwenye ukurasa wa 377 kwenye fungu kifungu nambari 40 nitakuja na 41 maana yake vinafanana, "Uwezo wa Jaji Mkuu kutunga Kanuni za Mahakama", hiki ni kifungu nambari 40. Maana Jaji Mkuu kwa kushauriana na kamati ya watumiaji Mahakama atakuwa na uwezo wa kuunda Kanuni bila ya kufanya mapitio ya ada za Mahakama. Kifungu (b) "Kufanya mapitio ya mamlaka ya kifedha ya Mahakama". (c) "Kuweka sifa za wasuluhisho wasiokuwa Majaji na Naibu Mrajis (b) Maslahi ya Washauri na wasuluhishi wasiokuwa Majaji na Naibu Mrajis (e) Maelekezo mengine yoyote kwa ajili ya kuharakikisha utaratibu wa usikilizaji na kujaza mapungufu yoyote katika utendaji wa Mahakama.

Sasa ukija kwenye kifungu nambari 41 unakuta uwezo wa Waziri kuunda kanuni:

> "Waziri anaweza kwa amri iliyochapishwa katika gazeti rasmi kutunga kanuni ili kuleta utekelezaji mzuri wa sheria hii".

Sasa nahisi Jaji Mkuu yeye anatunga kanuni na Waziri na yeye anatunga kanuni huku. Sasa si kutakuwa migongano hapa. Maana yake Waziri anaweza akatunga za kwake na Jaji Mkuu akatunga za kwake zote zikapelekwa kwenye Mahakama hiyo hiyo, ipi itakuwa inafanya kazi. Sasa mimi nafikiria hapa kwa sababu huu ni muhimili tungemuachia kazi hii akaifanya Jaji Mkuu kama ambavyo imeainishwa hapa. Huyu Waziri tukamuondosha kabisa hapa asitunge kanuni hapa kwenye hii Mahakama, tumuachie Jaji Mkuu kwa sababu Mahakama ipo kwenye kitengo chake na yeye ndiye muhimili wa Mahakama zile akatunga kama ambavyo ameonesha kwenye aya ya 40, hii ya 41 tukaiondosha kwa sababu tukimpa mamlaka Waziri hapa akatunge kanuni tena kule na Jaji Mkuu anatunga kanuni, sasa mimi ninahisi hapa kutakuwa na migongano.

Kwa hivyo nilikuwa naomba sana hili Mhe. Waziri aliangalie vizuri asihisi kwamba tunamnyima uwezo wake kwa kuwa ni Waziri, uwaziri wake utabakia lakini na yeye tumpe mamlaka yake yule Jaji Mkuu pale. Maana ndiye vyombo anavisimamia pale. Sasa tumuachie avitungie kanuni kwa sababu hata ukitizama hizi kanuni kwa haya mambo atakayoyasimamia tayari hiyo Mahakama itakuwa imenyooka vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu ulikuwa ni huo na baada ya kusema hayo kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mkwajuni tunauunga mkono mswada huu asilimia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika mswada wetu wa sheria wa kuanzisha Mahakama ya Biashara Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, tukija kihistoria hili jambo la kuanzishwa Mahakama ya Biashara Zanzibar ni jambo lenye kuleta faraja kwa upande wa Zanzibar, hususan ukitilia maanani kwamba Zanzibar ni visiwa, na ili tuweze kwenda na visiwa basi nafikiria biashara katika visiwa ndio jambo la msingi hasa linaloweza kusababisha uchumi wa eneo hili ukaweza kunyanyuka na kuonekana kama una umakini fulani.

Mhe. Naibu Spika, mimi nichukue fursa hii vile vile kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria kwa mswada wake huu kwa kushirikiana pamoja na watendaji wa wizara yake kwa kuona kwamba kwa sasa tumefikia pahala Zanzibar tuweze kuwa na Mahakama ya Biashara Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika mtandao wa biashara tunapozungumza kwa Zanzibar, ukiangalia wakaazi wa Zanzibar ni watu ambao wasiozidi milioni moja na laki tatu na kidogo. Lakini uingiaji wa mizigo ndani ya Zanzibar, mizigo inaingia inaweza kuhudumia Watanzania zaidi ya milioni mbili. Kwa hivyo basi katika utaratibu huo Mhe. Naibu Spika, mizigo mingi ambayo inaingia katika visiwa vya Zanzibar inabidi mizigo ile iweze kutafutiwa masoko.

Masoko haya kwa wafanya biashara wengi wa Zanzibar tumezoea kutumia njia za kuhaulisha mzigo eneo moja la muungano kupeleka eneo jengine la muungano. Lakini sasa katika utaratibu wa kupeleka mizigo hii Mhe. Naibu Spika, wafanya biashara wetu wamekuwa wakipambana na vikwazo vya aina nyingi kabisa. Vikwazo ambavyo Mhe. Naibu Spika, vipo vya kisheria na vipo ambavyo si vya kisheria. Sasa kwa kuanzisha utaratibu wa kuweka Mahakama hii ya Biashara, nafikiri itakuwa ni njia mwafaka ya kuwasaidia wafanya biashara wetu ambao wanaondosha mizigo yao na wanapofika upande mwengine wakaweza kuona kwamba pale panapotokezea matatizo ya kisheria, Mahakama hii iwe na uwezo sasa wa kuweza kusaidia wafanya biashara wale ili waweze kuona kuwa haki inatendeka katika masuala mazima ya kuendeleza biashara katika maeneo yao.

Jambo jengine ambalo linaleta utata katika upande wa biashara ya Zanzibar ni hawa ndugu nao ambao wanao kuja hapa kwa mitarafu ya kufanya biashara katika visiwa vyetu. Wanakuja hapa wanafunga mikataba na watu wengine ambao ni Wazanzibari wenyewe hapa wakakubaliana katika misingi ya kuendeleza biashara zao, lakini baadae kwa ujanja tu wa kukimbia baadhi ya kodi kwenye serikali yetu, wafanya biashara hawa wakafika pahala wakaweza kubadilishana aina ya biashara baina ya mkono mmoja kwenda mkono mwengine bila ya kuweza kutatua matatizo ambayo yapo kwa wafanya biashara ambao walikuwa wakishirikiana nao hapo mwanzo walipokuwa wakifanya biashara zao.

Sasa kwa kuja sheria hii ni matarajio yetu kwamba sasa amani itapatikana na haki za kuwalinda wananchi wetu za Zanzibar juu ya masuala haya ya kufanya biashara iwe na wageni, iwe na watu wengine wote ambao tunaingia nao mikataba, haki ya Mzanzibari itakuwa inalindwa kwa mujibu wa sheria.
Mhe. Naibu Spika, ukiondoa haya maeneo ya uwekezaji pamoja na mizigo ambayo inakuwa inaondoshwa kupelekwa upande wa pili wa muungano, vile vile tuna utaratibu wa biashara hizi baina ya wale wanaosafirisha mizigo na wasafirishaji vile vile wa mizigo.

Aina ya watu wetu Mhe. Naibu Spika, wanaofanya biashara katika visiwa vyetu vya Zanzibar ni watu maskini sana. Wanakwenda kutafuta mikopo, wengine wanakwenda kuekeza mali zao katika nyanja tofauti ilmuradi tu wahakikishe kwamba wanaweza kufanya biashara ambazo zinawasaidia kuweza kupata maslahi na kuweza kuendeleza maisha yao kwenye visiwa vyetu hivi.

Lakini kunakuwa kuna matatizo ambayo yanakuwa yanatokezea kwa hawa waletaji na wasafirishaji wa mizigo ya hawa wafanya biashara, kwa mfano kama juzi tu hapa palitokezea mtihani wa wafanya biashara kwa mizigo yao na wakapata mtihani mkubwa ndani yake.

Sasa kwa sheria hii ambayo tunaipitisha sasa hivi, tunataka tuhakikishe kwamba sheria hii inafikia mahali mpaka watu wa aina hii vile vile wanadhibitiwa na kuhakikisha kwamba wale watu wanaotaka kuja kufanya biashara ambao shughuli zao zinatokea nje, kuna utaratibu maalum ambao unakuwa unatayarishwa na sheria zetu hizi ambazo tunazotaka kuzipitisha hapa, tuone kwamba namna gani Wazanzibari ambao wanakuwa wanatumia meli hizi waweze kupata uhalali wa kuona panapotokezea matatizo ni njia ipi ya kisheria ambayo itakuwa inatumika ili waweze kupata haki zao bila ya matatizo ya aina yo yote.

Lakini kama hiyo haitoshi Mhe. Naibu Spika, hata mabenki ambayo tunatumia, yapo mabenki ambayo mtu anakwenda pale kufanya mkataba na wale wenye mabenki na baada ya kufika pale kuingiza fedha inakuwa sio tatizo kwao, unapotaka kwenda kutoa fedha zako sasa inakuwa ni mtihani mkubwa, tunaanza kutafuta vielelezo na kutafuta ripoti za Polisi na kutafuta pesa hizi umezipata vipi, wakati huyu mwanzo alipokuwa anakuja kufanya biashara na wewe, mambo yote haya hukuyatafuta. Inakuwa ni mbinu tu ya kufanya ujanja kumnyang'anya yule haki yule mtu ambaye amekuja pale kwa visingizio vya kibenki.

Sasa ni matarajio yetu kwamba sheria hii tunayoipitisha itasaidia na kuhakikisha kwamba nyanja zote zile ambazo tunahisi pana mbinu za ujanja ujanja kuweza kuwataabisha na kuweza kuwanyima uwezo wao wafanya biashara wetu, sheria hizi zitakuja kupambana nazo na kuweza kuona kwamba wanalindwa kwa mujibu wa sheria.
J
engine ambalo nilikuwa nataka kuzungumzia Mhe. Naibu Spika, ni hapa katika kipengele cha 17, wenzangu wote waliokuwa wametangulia walikifurahia hiki kipengele cha 17, naomba nikinukuu kinasema kwamba "Kesi zote za kibiashara zitasikilizwa na kumalizika ndani ya miezi 10 tokea kuanza lakini hazitozidi miezi 12".

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi ningependa nipate maelezo ya zaidi hapa. Kipindi hiki cha kutumika kwa ajili ya kutafuta muskabali wa kesi hii, kwa kesi za ndani ambazo tunazimiliki sisi ni sahihi. Sina matatizo nacho lakini kwa kesi ambazo zitakuwa zinagusa maeneo mengine, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie ufafanuzi ni utaratibu gani unaweza kutumika kuhakikisha kwamba tunakwenda sambamba na sheria yetu ambayo tumejiwekea wakati kuna matatizo ambayo yanagusa nje ya nchi yetu na sheria zitakazotumika sio tena za ndani, zitakuwa ni sheria za nje. Kwa mfano kama utakapokuja kutumia mashirika ya meli haya, ndege na kadhalika.

Sasa ningelimuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie tuweze kuona kwamba ni namna gani wafanya biashara hawa wataweza kulindwa pale ambapo wanaingia mikataba ya kimataifa na tayari sheria yetu imeshakuwa inaelekeza kwamba ndani ya kipindi hiki suala hili litakuwa limekamilika, wakati wenzetu wao wana taratibu nyengine za kuweza kuendeleza kesi kama hizi.

Nalizungumza hili Mhe. Naibu Spika, kwa sababu nina uzoefu wa kesi ambazo zinahusu upande wa Zanzibar na nchi nyengine zinachukua muda mrefu sana, wakati sheria yetu tunayosema hapa tunayotaka kuipitisha tunasema kwamba ndani ya miezi 10 au 12 sakata hili au tatizo hili litakuwa limemalizika na hii itakuwa ni kwa mujibu wa sheria.

Sasa kwa yale mambo ambayo yatakuwa hayapo katika uwezo wetu tutakuwa tuna utaratibu gani ambao tunakuwa tunautumia. Baada ya maelekezo hayo Mhe. Naibu Spika, mimi ninakubaliana na mswada huu. Mswada ni mzuri, ni mswada ambao unaweza kuwasaidia Wazanzibari wote kwa ujumla na Watanzania pia, na kwa niaba yangu na wananchi wa jimbo langu naunga mkono hoja baada ya kwisha kupata ufafanuzi wa mambo ambayo nilikuwa naomba ufafanuzi wake. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuchangia mswada huu wa Mahakama ya Biashara.
Kwa kweli umekuja wakati mzuri mswada huu hasa kwa vile Mahakama hii ni mara ya kwanza kuweza kusikiliza kesi hizi za wafanya biashara ambao wanasumbuka sana, hawajui kesi zao zitachukuliwa hatua au zitahukumiwa kisheria.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa wakati huu mzuri wa kulifikisha suala hili mbele ya Baraza hili tukufu ili kulichangia liweze kuhakikisha kwamba mswada huu unatekeleza kisheria na kwa haki na kwa kila mmoja ambaye anafika katika Mahakama ili kusikiliza shughuli ya hukumu ya biashara ambazo wananchi wengi hivi sasa wanasumbuka sana, kuweza kupata haki zao za msingi hasa wafanyakazi wa ndani ya nchi ambao wanahangaika sana kule na kule na hawajui wapi watapata hukumu ya matatizo yao. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, nikiangalia kwenye ukurasa huu 369 kifungu cha 2, kwa madhumuni ya kufanya kazi zake chini ya sheria hii. Mahakama itakuwa imekamilika iwapo itakuwa na Jaji anayeongoza na Washauri wawili.

Kwa kweli kama Mahakama haitokuwa sahihi kama itakuwa haina Washauri, kwa vile Jaji peke yake asiwe na uwezo wa kuhukumu kesi hii hadi tu apate Washauri wawili na ndivyo itakavyokuwa haki hizo zimefanyika. Kwa vile kama tutakosa Washauri katika Mahakama ni afadhali kesi hiyo iakhirishwe ili ipangiwe kipindi chengine ili iweze kusikilizwa kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, hali ya sasa katika Mahakama zetu zinazidi muda ambao umepangwa miezi 10 au miezi 12. Sasa namuuliza Mhe. Waziri atakapokuja aweze kunifafanulia. Wakati Mahakama yetu hii hivi sasa haijaanzishwa itafuta sheria labda kwa miezi miwili au miezi mitatu hadi mwaka mmoja. Jee, ikiendelea kesi baada ya miezi 12 imefika na muhusika hakukata appeal yoyote, jee, kesi hiyo mshtakiwa ataachiwa huru au itarudia tena kuanza upya kusikilizwa kama itakatwa appeal nyengine.
Kwa sababu najua kwamba Mahakama zetu imekaa angalau imefikisha kwa wakati imemaliza miaka miwili na miaka mitatu. Sasa kuniambia kwamba Mhe. Naibu Spika, kuwa kesi zetu zitakuwa miezi 10 hadi miezi 12, hapo itakuwa ni nafuu sana kwa wafanya biashara kuweza kupata haki zao kwa wakati.

Kama Mahakama zitakuwa kiasi hicho kwa kweli itakuwa ni mfano ni Mahakama ya kwanza inakwenda kisheria hapa nchini, lakini Mahakama zilizobaki mpaka sasa kwa ufahamu wangu zinachukua kuanzia miaka miwili hadi miaka mitatu, hasa zile zinazofanana na biashara. Kwa sababu Mahakama ya Ardhi miaka kidogo imepungua ujue una miaka mitano. Sasa ndio kusema kwamba hii Mahakama yetu ya Biashara itaanza kwa wakati kama huu inafaa kupongezwa sana na kuweza kufanyiwa mfano kwamba hivi sasa tuna.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, nikiangalia ukurasa wa 371 kifungu cha 15, pande zote zitajuulishwa tarehe na muda ulioteuliwa kwa ajili ya kufanya mkutano kabla ya kusikilizwa kwa njia ya notice katika *form number* moja kwenye jadweli la pili la sheria hii na kila upande utatii maelekezo yoyote yaliyotolewa kwa njia ya mdomo au katika notice, hiyo kama hali iwezekanavyo kuwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kifungu hiki cha 15 kinanieleza kwamba kesi yoyote kama haitokatiwa notice kujadiliwa kwa muda inawezekana kesi hiyo ikawa batili. Na kama imekuwa batili, ina maana kesi nyingi zitabidi kwa wakati mwengine mshtakiwa aweze kuachiwa huru kwa sababu mtu akipotea tu kukata *notice* kwa muda ina maana mshtakiwa atakuwa hana hatia, na kama mwenye kesi ambaye hakuweza kwenda kwenye Mahakama kuzungumza kwa njia ya mdomo akipeleka barua bubu ambayo si ya kisheria wala hakulipiwa *notice*, ina maana vile vile mshtakiwa hana hatia na hivyo kusema kwamba washtakiwa inawezekana wakaachiwa huru wengi kwa sababu watu wetu ni mara nyingi huwa wanasahau kufuata sheria inayotakiwa na kila mtu anafuata kienyeji.

Sasa tuelewe wananchi wetu kwamba sheria hizi hivi sasa zitakuwa sio sheria zile za kubuni au za kumsaidia mtu kwamba fulani nafahamiana naye, kwa sababu hili suala la biashara ni uti wa mgongo wa wafanyakazi au wafanyabiashara.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, vile vile ninakwenda katika kwenye ukurasa wa 371 kifungu cha 4 baada ya kuakhirishwa kwa mara ya kwanza iwapo pande zote zimeshindwa kuhudhuria mkutano wa kabla ya kusikilizwa Mahakama itafuta kesi hiyo.
Hapo nikirejea Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri akija anieleze kama kesi hiyo itafutwa itakuwa ni mara ngapi washtakiwa zinakuwa hazipo sahihi na zitakuwa zinafutwa na itakuwa mwisho kesi zote zinafutwa bila ya wakati au bila ya msimamo. Kwa sababu hapa amepewa uwezo mshtakiwa yeye mwenyewe tu amekwenda mara mbili au tatu, mshtaki kama kadhadhurika au kaumwa akakosea kupelekea barua au kakosa kupeleka *notice*, ina maana washtakiwa watakuwa mara nyingi wanasalimika na Mahakama hii.

Kwa kweli naomba Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hili suala alipange vizuri kwamba washtakiwa au mshtaki apewe muda wa kuweza kukata notice kisahihi na isiwe kama siku moja ile ile tu hakufika kwamba kesi yake imefutwa, hivyo itakuwa washtakiwa wengi wanaondoka pale bila ya kushtakiwa na bila ya kupata haki ya mshtaki kwamba mshtaki hakupeleka *notice* kwa wakati na inakuwa aachiwe huru.

Mhe. Naibu Spika, ninaipongeza sana Mahakama hii ya Biashara itakapoanza kazi zake na kusainisha na Waziri ianze kwa mujibu wa sheria na mujibu wa haki kwa wananchi wote, isiwe tu mwananchi ambaye wa chini anadaiwa pesa ndogo tu Mahakama inachukua hatua kubwa ili mwananchi akidaiwa apewe muda wa kuweza kutafuta madeni yale na kuyasawazisha Mahakamani, kwa sababu kudaiwa sio kuiba.

Mdaiwa anakuwa hawezi kulipa kwa wakati kwa sababu ya hali ya maisha anajua kwamba anadaiwa lakini kutokana na maisha yalivyomtanda ina maana Mahakama ichukue muda wa kumpa mshtakiwa muda wa kujipinda tena ili arudi tena Mahakamani kuweza kutoa ahadi ambayo ataiahidi pale Mahakamani, sio tu kwamba amefika pale Mahakamani na sheria siku hiyo hiyo inamchukulia kwamba kwa vile unadaiwa shilingi laki moja na leo hukuja nayo, Mahakama inachukua kumpeleka kwenye kizimba cha jela muda wa miezi mitatu, hivyo itakuwa hatuwafanyii haki wale watu wanaodaiwa.

Wadaiwa kwa kweli lazima wapewe uhuru mkubwa sana wa kujitetea ili waweze kutafuta ile haki ile ambayo inadaiwa, kwa sababu alipokwenda kukopa au kuchukua kitu kile alikwenda kwa nia nzuri tu, lakini mabadiliko ya maisha ni sawa sawa na mabadiliko ya upepo huwa unatokezea wakati wowote. Kwa vile mshtakiwa alijua baada ya siku moja mpaka kufikia siku kumi tayari atakuwa amesawazisha deni, lakini siku ile anapokwenda kusawazisha deni kwa mdai akimuomba kwamba bwana vipi mimi sikuweza kupata ile siku ya kumi, naomba hili suala mahakamani twende tukaombe radhi kwa Hahimu ili suala hili lizidishwe mwezi mmoja lisiwe geni, kwa sababu ni hilo ni suala la kijamii.
Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa sana kwa vile wenzangu wamekwishakukchangia suala hili, isipokuwa ninaiomba Mahakama ianze kwa kutimiza ahadi zake za mwezi 10 hadi 12 kuweza kuzimaliza kesi zote za Mahakamani hapo. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunisikiliza.

TAARIFA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kesho tarehe 10/4/2013, wakati wa asubuhi kutakuwa na sherehe kubwa za uzinduzi wa umeme wa waya wa pili kutoka Ubungo Dar es Salaam hadi Mtoni Zanzibar zitakazofanyika katika Uwanja wa Amaan;

Na kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu wote wamealikwa kushiriki katika uzinduzi huo wa umeme ambao ni wa kihistoria kutokana na umuhimu wake;

Na kwa kuwa michango ya Wajumbe kwa siku ya leo imemalizika katika hoja iliyo mbele yetu inayohusu sheria ya kuanzishwa Mahakama ya Biashara;

Na kwa ajili ya kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wajumbe ili waweze kujitayarisha kwa ajili ya shughuli ya kesho ya uzinduzi wa umeme;

Hivyo, Mhe. Naibu Spika, naliomba Baraza lako tukufu uliahirishe kikao chake kabla ya wakati kuanzia hivi sasa hadi kesho tarehe 10/4/2013, saa 11.00 jioni ili tupate muda wa kukamilisha shughuli yetu hiyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa michango yenu tangu asubuhi hadi hivi jioni na ushirikiano mulionipa katika kazi hii ya kuongoza Baraza, hivyo basi natamka rasmi kwamba kikao chetu tunakiakhirisha hadi kesho siku ya Jumatano tarehe 10/04/2013 saa 11.00 jioni.

(Saa 12.00 jioni Baraza liliakhirishwa haditarehe 10/04/2013
Saa 11.00 jioni)